**4 FEBRUARI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA PILI

### Kikao cha Saba – Tarehe 4 Februari, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wa Pili, Kikao cha Saba.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, Mbunge wa Mbagala, aulize swali lake.

Na. 109

### Ujenzi wa Barabara Chini ya *DMDP – II*

**MHE. KAKULU B. KAKULU** aliuliza: -

Je, barabara zipi na zenye urefu wa kilometa ngapi zinazotarajiwa kujengwa chini ya Mradi wa *DMDP – II* katika Jimbo la Mbagala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, Mbunge wa Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *DMDP* - Awamu ya Pili ni mwendelezo wa Mradi wa *DMDP* Awamu ya Kwanza na unazinufaisha halmashauri zote tano za Dar es Salaam, (Jiji la Dar es Salaam na Manispaa za Ubungo, Kinondoni, Kigamboni pamoja na Temeke) kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Lengo kuu ni kuzijengea halmashauri uwezo wa kutoa huduma bora kwa wananchi kupitia uboreshaji wa miundombinu muhimu na kuimarisha uwezo wa kitaasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zinazotarajiwa kujengwa katika Jimbo la Mbagala zina urefu wa kilometa 18.48 kwa gharama ya shilingi bilioni 52.3. Barabara hizo ni Kilimahewa - Toangoma kilometa 6.17 na Masuliza kilometa 4.04 ambapo ujenzi wake umefikia 16% hadi sasa. Barabara zingine ni pamoja na Maandazi kilometa mbili, Masaki kilometa 3.91, Kipati kilometa 0.72, Ndunguru kilometa 1.64 pamoja na madaraja mawili ya watembea kwa miguu ambayo yanajengwa na ujenzi wake umefikia 34%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu.

**MHE. KAKULU B. KAKULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ninafahamu kwamba kama tunavyofahamu na TAMISEMI mnafahamu kwamba kuna mfereji maarufu sana unaitwa Mfereji wa Kwashego, ule mfereji Serikali ilishajenga kwa sehemu fulani ila kuna kipande kimebaki kama cha kilometa mbili kasoro kidogo,

sasa pale yanatokea maafa kila wakati hasa wakati wa majira ya mvua nyingi. Serikali ina kauli gani kuhusu umaliziaji wa kipande kilichobaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kuambatana nami kwenda kuangalia maeneo hayo ili ujiridhishe na kushuhudia madhara yanayotokana na mfereji huo pamoja na miundombinu iliyoko katika hiyo kata? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi la swali la msingi, Mradi wa *DMDP II* ni mwendelezo wa Mradi wa *DMDP* Awamu ya Kwanza. Kwenye ile awamu ya kwanza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuwaondolea wananchi wa Dar es Salaam adha ya mafuriko yanayotokana na mvua alijenga mifereji yenye urefu wa kilometa 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huo ujenzi wa awamu ya kwanza mfereji huo alioutaja Mheshimiwa Mbunge, mfereji wa Kwashego Mheshimiwa Rais alijenga kilometa 3.15. Hivi sasa kwenye *DMDP II* Serikali imetenga dola milioni 438 na itajenga mtandao wa barabara upatao kilometa 257, tutajenga mtandao wa mifereji mikubwa ya maji yenye urefu wa kilometa karibu 90, tutajenga masoko 18 na tutajenga *stand* tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tutakwenda kujenga miundombinu ya taka ngumu madampo matatu. Sasa kwenye hizi kilometa 90 za mifereji Serikali inakwenda kujenga, kumalizia kipande hicho cha mfereji kilichobaki kilometa 1.4 za mfereji wa Kwashego.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kuona madhara yaliyotokea kutokana na mfereji huo wa Kwashego, mimi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI niko tayari mara Bunge hili

litakapokamilika tutapanga ratiba na Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaurembo nilikuona.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mzambarauni – Mkoroshoni hadi Saku mwisho kwenda Daraja la Kilungule ambao upo katika mradi huu wa *DMDP* ili kuondoa adha ya wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge wa Chamazi ipo kwenye huu mpango wa ujenzi wa *DMDP II* na maeneo mengi kwenye mradi huu kwenye hizi halmashauri zote tano za Mkoa wa Dar es Salaam tumeshakamilisha usanifu na maeneo mengi tumeshasaini mikataba. Tumesaini mikataba zaidi ya 22. Kwa hiyo, ujenzi wa barabara hiyo utakwenda kuanza mapema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa za Serikali ambazo ninazipongeza sana, sana, sana kutuletea miradi hiyo ya *DMDP,* lakini bado kuna changamoto kubwa ya miradi hiyo wakandarasi kutofanya vizuri sana. Je, nini kauli ya Serikali kwa wakandarasi hawa waifanye kazi hiyo kwa muda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya ziara kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwenye huu Mkoa wa Dar es Salaam. Pamoja na miradi

mingine nilikagua miradi hii ya barabara ya *DMDP II,* nimeona kasi ya wakandarasi na kwa kweli Serikali ilichukua hatua kali sana kwa wakandarasi wanaochelewesha kazi ninyi mliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii tena kuwaelekeza wakandarasi wote pamoja na wasimamizi wa miradi hiyo ambayo Serikali imewaweka kusimamia miradi hiyo watekeleze wajibu wao kwa kadri mikataba inavyoelekeza. Nje ya hapo tutaendelea kuchukua hatua kali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, Mbunge wa Igalula.

Na. 110

**Ujenzi wa Barabara Jimbo la Igalula**

**MHE. JUMA R. MUSTAFA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti ya ujenzi na ukarabati wa barabara za Jimbo la Igalula ili ziweze kupitika muda wote?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni unasema, "naomba sasa swali langu namba fulani lipate majibu."

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Mustafa, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuongeza bajeti mwaka hadi mwaka kadri ya mahitaji ya matengenezo na upatikanaji wa fedha kutoka shilingi bilioni 1.12 mwaka 2020/2021 hadi kufikia shilingi bilioni 4.26 mwaka 2021/2022. Hii imesaidia

sana kuboresha miundombinu katika Wilaya ya Uyui likiwemo Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.31 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za matengenezo ya barabara zifuatazo katika jimbo la Igalula; Barabara za Isuli – Miyenze, Mwisole – Miyenze – Nyahua, Iyombo – Mwisole – Lutende, Mabeshi – Loya, Malongo – Mabeshi, Miswaki – Loya, pamoja na Miswaki – *Igunga Border*. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha bajeti kila mwaka kuhakikisha changamoto za barabara katika Jimbo la Igalula zinatatuliwa na barabara zote ziweze kupitika muda wote bila vikwazo kwa misimu ya mvua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba.

**MHE. JUMA R. MUSTAFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali na ninapenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula lipo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ni moja ya halmashauri tano ambazo zina mtandao mkubwa wa kibarabara. Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ina kilometa 1,806.76 lakini tunapokea bajeti ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Sasa Serikali haioni umuhimu wa kutuongezea bajeti kutoka hiyo shilingi bilioni nne mpaka shilingi bilioni 12 kama wanavyopokea halmashauri zingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa Barabara za Mabeshi – Loya kilometa 45, Loya – Miswaki kilometa 26, Miswaki hadi Lutende hadi mpakani Nsimbo zenye jumla ya kilometa 158; lakini kuna barabara kutoka Kigwa – Itundaukulu hadi Goweko kilometa 26, kuna Barabara ya Goweko – Igalula hadi Mto Wala kilometa 65, Mabeshi – Malongwe kilometa 10, Tula – Mwamlela kilometa 35, Mwisole – Miyenze kilometa 41? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba jimbo hili analotoka Mheshimiwa Mbunge la Igalula halmashauri yake ina mtandao mpana wa barabara wenye urefu wa kilometa 1806.76. Kama nilivyotangulia kusema kwenye jibu la msingi, Serikali imefanya jitihada za makusudi mwaka 2020/2021 bajeti ilikuwa shilingi bilioni 1.12 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyoingia madarakani kwa kutambua mtandao mpana huu wa barabara uliopo kwenye jimbo la Mheshimiwa Mbunge aliongeza bajeti hii na kufikia shilingi bilioni 4.26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, jimbo la Mheshimiwa Mbunge, makao makuu yake yako kwenye Wilaya ya Uyui, Serikali iliona umuhimu wa kuanza pia kuboresha miundombinu makao makuu ya wilaya ambako ndiyo makao makuu ya wilaya ya Mheshimiwa Mbunge pia. Tumeanza ujenzi wa lami na tayari tumeshakamilisha kipande cha mita 400 kwenye huo Mji wa Isikizya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni lini barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge; barabara alizozitaja ziko katika makundi mawili; zipo ambazo tumepanga kuzitekeleza kwenye mwaka huu wa fedha 2025/2026 na ambazo haziko kwenye kundi hili. Nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa aweze kuangalia mpango wetu unasemaje ili waweze kuingiza barabara hizo kwenye maandalizi ya bajeti hii ambayo tunaiandaa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, nimekuona.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kwamba uwiano wa bajeti kwa Majimbo umetofautiana sana. Makete tuna mtandao wa barabara za *TARURA* wa kilometa 680.3 na bajeti yetu ni shilingi bilioni 3.2. Hata hivyo kuna majimbo ambayo yana chini ya kilometa hizo na yana zaidi ya bajeti ya shilingi bilioni saba hadi

shilingi bilioni 10 na sisi Makete tumeleta andiko kwako la kukuomba fedha/kuongezewa bajeti hii kwa kujua kwamba Makete ni wilaya ya uzalishaji. Ipi kauli ya Serikali kwa Wana-Makete kuhusu ongezeko la bajeti kwa barabara za *TARURA* kwenye wilaya yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyoeleza Mheshimiwa Mbunge wa Makete kwamba tumeshapokea maombi mengi ndani ya Serikali kutoka majimbo tofauti tofauti wakiomba ongezeko la bajeti, lakini na wengine wakihoji namna mgawanyo unavyofanyika. Serikali imeshaona umuhimu wa kufanya mapitio upya ya *formula* namna ya kugawanya fedha za matengenezo ya barabara kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, Mbunge wa Ngara.

Na. 111

**Ujenzi wa Stendi Ngara Mjini**

**MHE. DOTTO J. BAHEMU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi ya Ngara Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara inayo stendi ndogo inayotumika kwa sasa. Hata hivyo, stendi hiyo haikidhi mahitaji ya huduma za usafiri kwa Mji wa Ngara unaoendelea kukua. Kwa kuwa eneo la stendi iliyopo sasa halitoshelezi ujenzi wa stendi ya kisasa, halmashauri inaendelea na utaratibu wa kufanya tathmini ili kutwaa eneo lingine kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 halmashauri imepanga kutenga shilingi milioni 150 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kulipa fidia ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kukamilika kwa taratibu za utwaaji wa eneo, halmashauri itajumuisha mradi wa ujenzi wa stendi ya Ngara Mjini katika mipango na bajeti zake ili kuanza utekelezaji wa ujenzi huo, kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ambayo yanatia moyo, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ngara limepakana na nchi mbili (Burundi pamoja na Rwanda), kama unatokea Rwanda kuja Ngara, kuja Tanzania mji wa kwanza kukutana nao ni Mji wa Rusumo ambao pale kuna mpaka mkubwa na unafanya kazi kwa saa 24 lakini pale pia hakuna stendi, wametafuta tu kisehemu kama kichochoro wamejibanza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitokea Burundi kuja Tanzania mji wa kwanza kukutana nao ni Mji wa Kabanga, ule Mji wa Kabanga ni Mji ambao kwa sasa hivi katika Jimbo letu la Ngara unafanya vizuri sana katika makusanyo. Hata robo ya pili uliopita wao ndiyo walikuwa wa kwanza wamekusanya zaidi ya shilingi milioni 733 lakini pale pia hapana stendi, mabasi yana-*park* nje na mabasi kutoka Ngara kwenda katika maeneo mengine Tanzania yote yanaanzia katika Mji wa Kabanga, lakini pale pia hakuna stendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kujua Serikali ina mpango gani kuhakikisha katika hii miji miwili Rusumo pamoja na Kabanga pia napo kunakuwa kuna stendi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mji wa Rusumo na Mji wa Kabanga ni miji inayokua kwa haraka, lakini ni miji ambayo ipo kimkakati kulingana na jiografia mahala ilipo. Ninatambua pia kwamba pale Kabanga pamoja na Rusumo Serikali imejenga masoko makubwa, masoko ambayo kwa kiasi kikubwa yatachangia sana kuendeleza ukuaji wa mji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ngara kwenye *strategic plan* wanazoziandaa kwa ajili ya kutekeleza dira ambayo tumeendelea kuijadali hapa na mipango ya maendeleo ya miaka mitano ambayo tunaendelea kuijadili hapa na mpango wa bajeti wa mwaka huu unaofuata wa fedha, aende aangalie uwezekano wa kuiangalia miji hii kuwa na maboresho ya stendi zilizopo, lakini na kwa muda mrefu kuangalia uwezekano wa kujenga stendi za kisasa kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Khambay.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri tuna Barabra ya Ngarenaro – Nakwa yenye urefu wa kilometa saba, Serikali imekwishakujenga kwa kiwango cha lami kilometa tatu. Je, ni lini Serikali itamalizia kipande cha kilometa nne kilichobaki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anatokea Babati mahali ambapo tunatekeleza Mradi wa *TACTIC*. Pamoja na uhitaji wa maeneo mengi ya kuweza kuendelezwa kwa mitandao ya barabara ukiwemo mji wake mwenyewe, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tafadhali maswali ya nyongeza yaendane na swali la msingi ili Mawaziri waweze kujibu kwa usahihi zaidi. Kwa sababu tunapotoka nje kabisa ya swali tunaweza kuwapa taabu Waheshimiwa Mawaziri kujibu ingawa wanajua mambo mengi, lakini watakosa kujibu kwa usahihi halafu badaye tutalalamika kwamba jibu halijajibiwa kwa usahihi.

Kwa hiyo, ninaomba turudi sana kwenye swali la msingi kama kuna eneo linahusika na hilo jambo basi tuulize hivyo ili Mawaziri wapate kujibu kwa vizuri zaidi.

Haya tuna Mheshimiwa Abdallah Chikota. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ina mradi wa ujenzi wa stendi chini ya Mpango wa *TACTIC Tier 3*. Je, ni lini ujenzi huo utaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Nanyamba tunatekeleza Mradi wa *TACTIC* Awamu ya Tatu na kama ambavyo nimekuwa nikijibu hapa, maeneo yote ambayo yapo kwenye Awamu ya Tatu ya Mradi wa *TACTIC*, miji 18, mwezi huu wa pili tunakamilisha usanifu na baada ya hapa tunakwenda

kutangaza zabuni ili kupata wakandarasi wajenzi na wakandarasi wasimamizi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. George Venance.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa pale Maswa Mjini kunahitajika ujenzi wa stendi. Ninaomba kujua stendi hii itajengwa lini Mheshimiwa Waziri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia ameuliza stendi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Venance, Mheshimiwa Waziri anauliza umeuliza swali la stendi? Anataka kwa usahihi zaidi.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, stendi ya Mji wa Maswa katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa ni lini itajengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Maswa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa stendi katika maeneo mbalimbali, lakini miradi yote ambayo tunaitekeleza ndani ya Serikali inazingatia mipango ya Serikali na Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi. Hivyo, ninamuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri husika waangalie mipango yao ilivyo na kama inagusa ujenzi wa stendi waanze kutenga fedha na kujenga stendi hiyo mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Jimbo langu la Mchinga halina stendi hata moja na kwenye jimbo lile magari makubwa sana yanapita kutokea nje ya nchi, nikiwa na maana ya Mozambique, Ruvuma na Mtwara. Magari haya makubwa yana-*park* kwenye eneo dogo tu ambalo limetengwa kwa ajili ya shughuli za palepale yaani jimboni.

Je, ni nini kauli ya Serikali kutujengea stendi katika eneo hilo la Jimbo la Mchinga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafanya mapitio pamoja na kutathmini hali ilivyo pale Mchinga. Ni muhimu sana mji huu uwe na stendi hivyo sisi ndani ya Serikali tutaenda kufanya mapitio na kuainisha hatua inayofuata ya kufanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Biharamulo tunahitaji kubwa sana la stendi na tayari katika Bunge lililopita nilielekezwa kuleta andiko, tukaleta andiko ambalo lilipita TAMISEMI kwa maelekezo ya Katibu Mkuu wa CCM alipokuja Biharamulo na limeshaenda mpaka Tume ya Mipango. Katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi hii ambayo tumeinadi safari hii, stendi hii imeahidiwa kujengwa.

Sasa ni lini ujenzi wa stendi hii ya Biharamulo utaanza ili wananchi hawa waweze kupata huduma ambayo wameisubiri kwa muda mrefu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi maandiko yanapopelekwa Tume ya Mipango, tume hufanya uchambuzi wa maandiko yote na kuangalia mipango ya eneo husika pamoja na mpango mkubwa wa Kiserikali na kutoa ruhusa ya kuendelea na ujenzi wa mradi husika kwenye eneo la halmashauri husika. Kwa sababu tayari andiko limekwishakwenda Mipango, litakaporejea TAMISEMI tutaendelea nalo kwa utekelezaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, Mbunge wa Mbulu Vijijini.

Na. 112

**Ujenzi wa Vituo vya Afya - Mbulu Vijijini**

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Haydom, Msetadu na Gakesh Jimbo la Mbulu Vijijini?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Karibu Mheshimiwa Waziri kwa jibu la swali la Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas wa Jimbo la Mbulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia mwaka 2024/2025 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya Eshkesh, Haydom na Maretadu. Vituo vya Afya Kata za Eshkesh na

Haydom ujenzi wa baadhi ya majengo umekamilika na huduma zimeanza kutolewa kuanzia mwaka 2023. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Afya Maretadu umefikia 90%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu imepeleka jumla ya shilingi milioni 106; kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Eshkesh shilingi milioni 10, Haydom shilingi milioni 66 na Maretadu shilingi milioni 30. Kituo cha Afya Maretadu kinatarajiwa kukamilika na kuanza kutoa huduma za wagonjwa wa nje yaani *OPD* kuanzia mwezi Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya majengo katika vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini ikiwemo Kata ya Gakesh.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kwa vituo hivi na ninashukuru kwa kazi nzuri ambayo inafanyika. Tuna vituo viwili ambavyo vinaendelea, kimoja cha mkakati katika Kata ya Dinamu ambayo imepokea shilingi milioni 250. Huduma moja ya muhimu sana ni huduma ya mama na mtoto.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha katika kituo hicho ili kuweza kutoa huduma hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza; tuna Kituo cha Masieda ambacho kipo kilometa 80 kutoka hospitali ya halmashauri na tuna wananchi wengi ambao wanakitegemea kituo hiki. Je, Serikali itakuwa tayari kupeleka gari la wagonjwa yaani *ambulance* kitakapokamilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Nuwas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza kwa ufuatiliaji na kuuliza maswali ya msingi kuhusu Jimbo hili la *Mbulu DC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali ilipeleka fedha katika Kituo cha Kimkakati cha Dinamu, Halmashauri ya Wilaya ya *Mbulu DC* na kituo hiki kilianza ujenzi mwezi Julai, 2025. Majengo ya kuchomea taka na miundombinu mingine imeshakamilika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa kuanzia mwezi ujao kituo hiki kitaanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninamhakikishia Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji miundombinu inayotakikana katika kituo hiki. Pia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine, suala la *ambulance* tunaamini kabisa kulingana na jiografia ya Jimbo la *Mbulu DC* kuna uhitaji mkubwa wa *ambulance*. Tunalichukua hili na tutalifanyia kazi kulingana na tunavyozidi kupata bajeti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya afya katika Kata za Mwenge na Kitumbikwera katika Jimbo la Lindi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mussa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wa kuainisha maeneo yenye uhitaji hasa wa vituo vya afya vya kimkakati. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya kwa sababu kuna uhitaji mkubwa wa wananchi katika jimbo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nuru Issa.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Nguruka kinachopatikana Wilaya ya Uvinza katika Jimbo la Kigoma Kusini ni moja ya vituo vya afya vinavyohudumia wananchi wengi. Kwa takwimu wananchi wanaohudumiwa na Kituo cha Afya cha Nguruka ni zaidi ya 300,000. Je, Serikali ina mpango gani wa kukipandisha hadhi kile kituo cha afya kuwa hospitali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kama unayo majibu yake unaweza kujibu hilo swali kwa sababu ni nje ya hili swali, ni mbali huko.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kupitia tathmini na maandiko katika halmashauri zote nchini hasa katika vile vituo vya afya ambavyo vina idadi kubwa ya wagonjwa. Tunawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Afya ili kuweza kutoa vibali vya kupandisha vituo hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, ninapenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa kuendelea na ujenzi wa vituo vya afya katika Jimbo la Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali, Kituo cha Afya cha Tawa na Dutumi ni vituo vya afya vikongwe katika jimbo letu na kwa sasa vina hali mbaya ya majengo pamoja na vifaa. Je, ni lini sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, itafanya ukarabati wa vituo hivi vya afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mfaume kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka katika Bunge lako Tukufu Serikali tayari imeshaweka mpango wa bajeti ya shilingi bilioni 102.08 kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo hivi vya afya pamoja na vituo ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameviainisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Arif Suleiman Premji.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa vituo vya afya kwenye Kata za Ndumbwe na Mangopachanne Mtwara Vijijini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Premji amevianisha ni vile vituo ambavyo tayari Serikali iliona ni vya kimkakati na viko katika mpango wa pili wa ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, wananchi wa Kata ya Ihembe, Wilaya ya Karagwe kwa kushirikiana nami Mbunge wao pamoja na halmashauri

tumejenga kituo cha afya hadi ngazi ya boma. Je, ni lini Serikali itatusaidia kukamilisha kituo hicho cha afya katika Kata ya Ihembe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bashungwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliainisha zaidi ya vituo 500 kote nchini ambavyo vimeshatengewa bajeti kwa ajili ya maboma hayo kwa ajili ya ukamilishaji. Ninamhakikishia Mheshimiwa Bashungwa, boma hili linakwenda kukamiliswa kwa wakati ili lianze kutoa huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimemwona Mheshimiwa *Engineer* Johnston.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika hospitali yetu ya Wilaya ya Nshambya katika Jimbo la Bukoba Mjini, majengo ya *radiology* yameshakamilika, je, ni lini Serikali sasa itapeleka vifaa kama *x-ray* na vingine katika hospitali hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vyote vya afya ambavyo vimeshakamilika pamoja na hiki ambacho Mheshimiwa Mbunge amekiainisha cha Bukoba Mjini tayari tumeshawasilina na *MSD* kuwahisha vifaa hivyo katika vituo hivyo ili kuanza kutoa huduma. Kwa maana ya kwamba sasa tunapoelekea kwenye Bima ya Afya kwa Wote, wananchi wetu waweze kupata huduma za uhakika katika vituo vyetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moses Ludovico.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Kate kina majengo mawili ambayo bado hayajakamilika, jengo la mama na mtoto, lakini pia jengo la upasuaji. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa majengo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moses kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhitaji wa majengo haya hasa *maternity complex* na jengo la mama na mtoto, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu hii ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi kote nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu mafupi na sahihi na Waheshimiwa Wabunge ninawapongeza kwa maswali mafupi ya kibunge, mwendelee hivyo hivyo.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 113

**Kipaumbele cha Ajira kwa Vijana Wanaofanya Vizuri *Field***

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuwapa kipaumbele cha kupata ajira vijana watakaofanya vizuri wakiwa *field* hasa kwenye miradi ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la Pili la mwaka 2008, ikisomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298, ajira katika utumishi wa umma hupatikana kwa ushindani na uwazi. Kujitolea katika utumishi wa umma huwezesha vijana kujipatia ujuzi wa ziada pamoja na kuwapa uzoefu na uwezo wa kushindana pindi ajira zinapotangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kupata mafunzo kwa vitendo ili kujipatia sifa za ajira katika utumishi wa umma pindi nafasi za taaluma zao zinapotangazwa na Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kutia moyo, lakini ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ajira alizozitoa katika kada ya afya na elimu. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, Mheshimiwa Waziri unaweza kuungana nami kwamba kumekuwa na baadhi ya malalamiko ya baadhi ya vijana ambao tayari wameshafanya

*interview*, lakini bado hawajapangiwa vituo na hasa katika kada ya ualimu ya msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri ni nini kauli ya Serikali juu ya vijana hawa ambao tayari wameshafanya *interview* na bado hawajapangiwa vituo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali ina mpango gani wa kuwapa vipaumbele vijana ambao wana umri mkubwa ambao wanaenda kufanya *interview* na ukizingatia wakikaa zaidi ya miaka miwili hawawezi kuingia katika soko hilo la ajira? Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Latifa Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali ilitoa kibali cha ajira 4,018 ambapo ajira hizo ni kwa walimu wa shule za msingi, walimu 3,018 ni walimu ngazi ya cheti na walimu 1,000 ni walimu ngazi ya stashahada. Hata hivyo, Sekretarieti ya Ajira itakwenda kuwapangia vituo vya kazi walimu hawa ambao tayari wameshafanya usaili kuanzia tarehe 01 Aprili, 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ajira hizi ni tofauti na zile ajira ambazo Mheshimiwa Rais alitoa kipindi cha uchaguzi, zile ajira 12,000 ambapo tayari ajira 7,000 kwa elimu na ajira 5,000 wameshapangwa na wanaendelea na kazi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ninakuhakikishia ifikapo tarehe 01 Aprili, 2026 walimu hawa wa shule za msingi watakwenda kupangwa kwenye vituo vya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la Pili la mwaka 2008 imeeleza wazi kwamba ajira zitatolewa kwa ushindani. Hata hivyo, kigezo cha umri mkubwa siyo kigezo katika kuajiri, lakini kwa kuona hivyo Serikali imeona changamoto

kwamba wale watu wenye umri mkubwa wameshindwa kushindana na watu ambao wametoka shuleni hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali kwa kuona hivyo, imetoa kipaumbele kuhakikisha kwamba wale watu ambao wana umri mkubwa watapewa kipaumbele pale ambapo wamelingana alama. Kwa hiyo, kama alama zimelingana atakayepewa kipaumbele ni yule ambaye ana umri mkubwa ili aweze kuingia kazini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul Yussuf.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali haioni haja ya kuondoa kigezo cha muda mrefu kwa vijana ambao wanaomba ajira Serikalini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, umemuelewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaelewa swali lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni haja ya kuondoa kigezo cha uzoefu wa muda mrefu kwa vijana wanaoomba ajira Serikalini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kama unajibu sawa, kama hauna...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru, kama nilivyokwisha kusema kwamba kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la Pili la mwaka 2008, kwa sasa ajira ni za ushindani na kigezo cha uzoefu hakipo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Kwa kuwa Serikali imekiri katika majibu ya swali la msingi kwamba vijana wanaojitolea wamekuwa wanajengewa uwezo. Je, Serikali haioni haja ya kuwa-*retain* (kuwashikilia) vijana wanaopitia katika Wakala wa *TaESA* kwa kundi la wanaojitolea na wale wa mafunzo kazini ili kupunguza gharama za ku-*recruit* upya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Serikali imeendelea kutoa miongozo mbalimbali inayohusiana na ajira kwa watumishi wa umma. Hata hivyo, Serikali imetoa mwongozo wa namna ambavyo tunakwenda kuwapata vijana ambao wanajitolea kwenye taasisi mbalimbali. Kabla ya mwongozo huo, vijana wengi wamekuwa wakiomba na wengine wakiomba kwenye taasisi wanapewa upendeleo kwa sababu ya kufahamiana na kujuana. Kwa kuona hilo Serikali imeamua kutoa mwongozo ambao unaelekeza kwamba ili upate nafasi ya kujitolea ni lazima upitie mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na swali la Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba Serikali inaona kuna haja ya kuendelea kuwaajiri wale watu wenye uzoefu ambao tayari wamekwishajitolea, lakini kwa kuzingatia sera ambayo sisi tumejiwekea kwamba ni lazima ushiriki katika mchakato wa ushindani ili kujenga usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine wamepata nafasi ya kujitolea kwa sababu ya kufahamiana. Sasa yule kijana ambaye hajapata nafasi moja kwa moja hatapata nafasi hiyo ya ajira. Kwa hiyo, ili kuleta usawa ni lazima tushiriki kwenye suala la ushindani ili ajira zetu ziwe kwa usawa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa Serikali imetumia busara kuwa wale vijana ambao wana umri mkubwa wapewe kipaumbele. Haioni kutumia busara hiyo hiyo kwa wale vijana ambao wanajitolea na ambao hawakupewa nafasi hizo kwa upendeleo na ni kazi ya Serikali kuwadhibiti wasipewe kwa upendeleo, waweze kupewa kipaumbele cha ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itaondoa usumbufu wa wale ambao wanaajiriwa kwenye maeneo ambayo hawayapendi baadaye wanaomba barua za uhamisho, lakini hawa wanaojitolea kwenye maeneo yao watabaki hapo. Serikali haioni ipo haja sasa ya kutumia busara hiyo hiyo vijana hawa waweze kupata kipaumbele? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuzingatia swali la Mheshimiwa Mbunge Saashisha kwamba wale vijana ambao wanajitolea bila upendeleo ni vigumu sana kutambua huyu kijana amepata ajira ya muda (ya kujitolea) kwa upendeleo au kwa kutotumia upendeleo, na ndiyo maana tumetoa mwongozo kwamba vijana wanaojitolea tunaendelea kuwaelekeza kwamba pamoja na kwamba wanajitolea, waendelee kuomba ajira zinazotangazwa na Serikali bila kuchoka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule fulani ambayo ina upungufu wa mwalimu, wamemwomba kijana amejitolea pale, Serikali imetangaza kazi, kijana huyo ambaye alikuwa anafundisha tayari kwenye shule hiyo ameenda kuomba halafu

anakosa kazi kwamba hana uzoefu. Nini kauli ya Serikali katika mazingira kama hayo kwa vjana hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Waitara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale vijana ambao wanajitolea katika vituo vyetu vya kazi kama walimu, kwanza kujitolea ni kumjengea uzoefu. Mwalimu huyo anapoendelea kufanya kazi ya kujitolea maana yake unamjengea uzoefu, pale ambapo anaenda kwenye usaili, anakuwa ana uwezo mkubwa wa kufanya vizuri kuliko yule ambaye hajajitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kutoa wito kwamba vijana wanapopata nafasi ya kujitolea, wajitolee, wafanye kazi ili kujijengea uzoefu zaidi na kuweza kushiriki kwenye ushindani wa ajira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ninakushukuru. *(Makofi)*

Tutaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Waheshimiwa Wabunge, wale ambao wanaandika vi-*memo* kwa kuuliza maswali ya nyongeza, ninaomba muandike na majina yenu kwa sababu mkiandika tu namba ya swali unalotaka kuuliza bila jina nitakuwa sijui ni nani anataka kuuliza. Kwa hiyo, ninaomba mnapoandika muandike na majina yenu chini.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Rashid Habib Ali, Mbunge wa Mtambwe, aulize swali lake.

Na. 114

**Manufaa ya Fedha za Wafadhili wa Mazingira**

**MHE. RASHID HABIB ALI** aliuliza: -

Je, Zanzibar inanufaikaje na fedha za mazingira zinazotolewa na wafadhili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Habib Ali, Mbunge wa Mtambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipokea fedha kutoka kwenye Mifuko ya Kimataifa ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi na wafadhili mbalimbali ikiwemo Mfuko wa Mazingira wa Dunia, Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Fedha hizo zimekuwa zikitumika kutekeleza miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025 jumla ya miradi kumi yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 97.6 imetekelezwa na kukamilika. Aidha, Serikali imeendelea kuandaa miradi kwa ajili ya kutafuta fedha kupitia vyanzo mbalimbali ambapo hadi sasa jumla ya miradi mitatu yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 62.6 ipo kwenye hatua za awali za maandalizi kwa utekelezaji kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi hii umeleta manufaa kwa jamii kwa kuongeza kipato kupitia utekelezaji wa shughuli mbadala na kuongeza uwezo wa jamii katika uhifadhi wa mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Aidha,

utekelezaji wa miradi hii umechangia katika ukuaji wa uchumi wa maendeleo endelevu na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*
**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Habib Ali.

**MHE. RASHID HABIB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, je, ni upi mgawanyo wa kiasilimia kwa pande hizi mbili za Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, ni upi mkakati wa Serikali katika matumizi ya fedha hizi katika kuyapa kipaumbele maeneo ambayo yameathirika kutokana na ukuaji wa bahari na mabadiliko ya tabianchi likiwemo eneo la Mtambwe Mkuu ambalo ni eneo la makazi ya watu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rashid Habib Ali, Mbunge wa Mtambwe kwa kuwa mdau mzuri sana wa mazingira. Ninakuhakikishia tu kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele cha hali ya juu kwenye sekta ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye Dira ya Maendeleo 2025/2050, kati ya nguzo tatu, nguzo moja inachukua suala la uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, ninaomba kwanza kukuhakikishia kwamba Serikali hii na kupitia Mheshimiwa Rais, amekuwa kinara na mdau namba moja wa mazingira kupitia 27 ya kijani, ameendelea kuhamasisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua nafasi hii kuhamasisha Waheshimiwa Wabunge wote, lakini pia viongozi wote wa mikoa na wilaya kuhakikisha kwamba ajenda ya uhifadhi wa mazingira inakuwa ajenda ya kudumu katika vikao vyao na shughuli zao za siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, nchi yetu ya Tanzania hivi sasa ni Makamu wa Rais wa Umoja wa Mataifa wa suala la mazingira *(UNEP 08)* ambayo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni amechaguliwa mwezi uliopita katika mkutano jijini Nairobi, ni Makamu wa Rais wa Dunia katika suala la mazingira. Kwa hiyo, kupitia nafasi hiyo, tunayo fursa nzuri ya kuendelea kupata miradi ya mazingira na kuboresha mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kwanza fedha za wafadhili, fedha za ndani na wadau mbalimbali zinazoletwa kwa shughuli za maendeleo ya mazingira zinagawanywa kwa pande zote mbili kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia uhitaji na vipaumbele vya pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tutaendelea kulifanya hivyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumeshafanya kazi kwenye maeneo yenye changamoto. Kwa mfano, Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika Wilaya ya Kaskazini A, maeneo ya kuhifadhi fukwe zilizoathiriwa na ongezeko la kina cha maji Sipwese Zanzibar, Pemba pamoja na maeneo mengine mengi tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mkakati wa kuendelea kuboresha maeneo ambayo yana changamoto hizo ikiwepo eneo la Mtambwe Mkuu, tutakwenda kufanya tathmini kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mara fedha za wafadhili zikipatikana, tutahakikisha tunafanya utekelezaji wa maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Hussein Saleh.

**MHE. ASHA HUSSEIN SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali haioni haja ya kushughulikia maeneo yanayojaa maji kwa wananchi wake hususan Jangamizini katika Jimbo la Fuoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama kuna majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwawakilisha vyema akinamama na Watanzania kwa ujumla katika sekta hii ya mazingira. Nami ninakuhakikishia tu kwamba katika shughuli zote za uhifadhi wa mazingira, moja ya kipaumbele ni kuhakikisha kwamba tunafanya ujenzi na matengenezo ya maeneo yote korofi ambayo yanapelekea wananchi kupata adha ya mafuriko ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kukuhakishia eneo hilo pia ni moja ya maeneo ya vipaumbele, tutaendelea pia kufanya tathmini na kutafuta fedha ili kuhakikisha wananchi wanaishi kwa utulivu na amani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwinyi Ramadhan.

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba atusaidie jibu letu, katika miradi 10 aliyoitaja ambayo imekamilika, miongoni mwao Jimbo langu la Bumbwini upo mradi wa mazingira, je, kwa sasa una hatua gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama una jibu la swali hilo la Bumbwini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake

mzuri kwa manufaa ya wananchi wa jimbo lake. Ninamhakikishia tu kwamba hii miradi 10 ambayo imetekelezwa kwa awamu ya kwanza ambayo ina thamani ya takribani shilingi bilioni 97.6 kama ambavyo amesema vizuri kwamba jimbo lake pia limenufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kazi hizi ni endelevu na sisi tutakwenda kufanya ufuatiliaji kuona hatua ilipofikia na tutakupa mrejesho Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassor Said Nassor.

**MHE. NASSOR SAID NASSOR MAROO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani kuongeza fedha kukabiliana na athari ya tabianchi hasa kwa nchi ya Zanzibar ukizingatia Zanzibar inaathirika zaidi kwa athari hizi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hajasikia vizuri, Waheshimiwa tutulie ili swali lisikike vizuri.

**MHE. NASSOR SAID NASSOR MAROO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani kuongeza fedha kukabiliana na athari za tabianchi hasa kwa Zanzibar, ukiangalia Zanzibar inaathirika zaidi na athari hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umeelewa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninampongeza sana Mheshimiwa Nassor kwa namna ambavyo ameendelea kuwa mdau mzuri wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli dunia ikiwemo Tanzania inakabiliwa na mabadiliko makubwa ya tabianchi ikiwemo kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari na hivyo kuathiri sana

makazi, lakini na rasilimali za uchumi na kijamii katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mpango wa Serikali ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunaendelea, kwa kushirikiana na wafadhili (Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Mazingira Duniani na wadau wengine) kuendelea kuongeza upatikanaji wa fedha na kuendelea kutambua maeneo yote yenye changamoto au dalili na *risk* za kupata changamoto hizo na kuendelea kufanya matengenezo, lakini pia kuwa na afua za utekelezaji kuhakikisha kwamba madhara haya hayawi makubwa au tunayadhibiti na hayawafikii wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hija Hassan.

**MHE. HIJA HASSAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kumuuliza maswali ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Swali moja tu Mheshimiwa.

**MHE. HIJA HASSAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lipo jimbo ambalo limeathirika kimazingira kwa Zanzibar, basi ni Jimbo la Kiwani. Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba amejenga tuta eneo la Sipwese ambalo ni sehemu ya Jimbo la Kiwani.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kufanya ziara na mimi kwenda kufanya tathmini ya kina Kiwani ili kujua ukubwa wa tatizo na kusaidia fedha kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kiwani

kwa kupaza sauti kwa niaba ya wananchi. Tunatambua kwamba moja ya dhamira ya Serikali hii ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na tabasamu muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya afua ambazo zinatekelezwa na Serikali hii kupitia sekta ya mazingira ni kuhakikisha kwamba maeneo yote korofi ambayo yanaleta athari kwa wananchi; athari ya mafuriko ya maji ya bahari na kadhalika yanatengenezewa bajeti na yanatengenezewa miundombinu yakiwepo matuta, kuta na kadhalika kuzuia mafuriko ya maji kwenda kwenye makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kushirikiana na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais tutaambatana nawe kwenda jimboni kuona eneo hilo ili tuweze kushirikiana katika kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba eneo hilo la Kiwani linadhibitiwa na wananchi wanaishi kwa utulivu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Hamza Singano, Mbunge wa Bumbuli, aulize swali lake.

Na. 115

**Kuanzisha Kituo cha Michezo – Bumbuli**

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha kituo cha michezo *(sports academy)* Bumbuli kwa kuwa lipo eneo kubwa kwa ajili ya viwanja vya michezo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nami hii ni mara yangu ya kwanza kusimama kujibu maswali kwenye Bunge hili la Kumi na Tatu, na kwa minajili hiyo kwa ridhaa yako ninaomba kutumia fursa hii kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka ya uhai na afya njema iliyotuwezesha kukutana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kijana wake niendelee kumsaidia kazi kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika nafasi ya Naibu Waziri. Ninamwahidi Mheshimiwa Rais ya kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uaminifu mkubwa na kwa maarifa yangu yote ambayo Mwenyezi Mungu amenijaalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hiyo hiyo, ninawashukuru wananchi wenzangu wa Muheza ambao wameendelea kuniamini niendelee kuwa mwakilishi wao na ninawaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana kuiletea maendeleo Muheza yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kujielekeza kwenye swali la Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Hamza Singano, Mbunge wa Bumbuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kusogeza huduma za miundombinu ya michezo kwa wananchi katika ngazi za mikoa, wilaya, halmashauri na majimbo mnayowakilisha Waheshimiwa Wabunge, na ni moja ya vipaumbele katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 na Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tunaendelea na ujenzi wa akademia ya michezo yenye hadhi ya kimataifa Malya, Wilayani Kwimba, Mkoa wa Mwanza chini ya mkandarasi *CRJE*

*(East Africa) Limited* ambapo mpango wa Serikali ni kujenga vituo hivi kikanda na tumeanza na Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikiwa inaendelea na juhudi hizo, ninatoa rai kwa uongozi wa Halmashauri ya Bumbuli kushirikiana na wadau wa michezo kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufadhili ujenzi wa kituo hicho muhimu kwa vijana wanamichezo wa Bumbuli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Hamza Singano.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninapongeza kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninaipongeza na Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada, lakini mipango mizuri ya kuwafikia wananchi. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwa kuwa suala la michezo ni suala la kuwagusa vijana sana hasa kiajira. Mbali na ufadhili kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuwagusa vijana katika eneo hilo kwa Bumbuli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, laini swali namba mbili, kuna jitihada gani za madhubuti kwa vijana kuibua vipaji kuanzia ngazi za chini shule ya msingi na sekondari hasa kwa michezo ya ngumi ambayo pia tunaona ni ajira kwa Tanzania ya leo hasa kule Tanga tukimtazama Mwakinyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Singano, Mbunge wa Bumbuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba inasimamia mafunzo mbalimbali, lakini na ufadhili pale ambapo inawezekana kadri ya upatikanaji wa fedha. Kwa sasa Serikali inaviendesha vituo viwili ambavyo vipo chini ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania kimoja kikiwa Tanga kule Mnyanjani na kingine Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo ambayo tunaweza kuyafanya kwa sababu ninafahamu kuhusiana na mashindano mbalimbali yanayoendeshwa na Waheshimiwa Wabunge, ni kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kukiwa na mashindano pale Bumbuli anialike ili niweze kuwaita wataalamu na *scout* kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania ili waweze kwenda kuangalia vipaji Bumbuli. Vipaji vitakavyopatikana vitapelekwa katika vituo hivi, lakini pia na kutafutiwa nafasi mbalimbali za kuweza kutumika kutumikia nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la jitihada za kuvumbua vipaji, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na pia Wizara ya Elimu, imekuwa ikiendesha mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa miaka kadhaa. Mchezo wa ngumi ambao Mheshimiwa Mbunge anauulizia ulikuwa haufanyiki kwenye mashindano haya kwa sababu ya uhatari wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na majadiliano ya hapa na pale kuona umuhimu wa mchezo huu kuanza vijana wakiwa wadogo na tuone namna ambavyo tunaweza kuchukua tahadhari kuhakikisha vijana wanaucheza bila kuathirika kwenye miili yao wakati wanafanya mchezo huu. Kwa hiyo, sasa hivi tumefikia katika hatua nzuri na nimhakikishie michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA kama siyo mwaka huu, mwaka ujao itakuwa na mchezo wa ngumi hali kadhalika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Kapoma.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu Morogoro ni kati ya mikoa yenye vipaji vingi, sasa nilikuwa ninataka kuuliza swali, je, Wizara imejipangaje tukiwa tunasubiri mikakati ya kujenga vituo vya kanda kwa sababu tuna maeneo mengi. Serikali inaweza ikatusaidiaje kwa sasa vijana wapate maeneo ya kujifunzia na kufanya mazoezi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umemwelewa?

Mheshimiwa Josephine jaribu kufafanua kwa ufupi sana.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro ni katika mikoa ambayo ina vipaji vingi sana, lakini hatuna maeneo ya vijana kujifunzia, tukiwa tunasubiri Wizara ikiwa inaanda sehemu za kikanda, je, kuna mpango gani wa haraka ambao tunaweza kuufanya ili vijana wapate sehemu za kujifunzia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama unajibu kuhusu Morogoro.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu langu ni la ujumla kwamba Wizara iko katika hatua za mwisho za kuanzisha taasisi ya usimamizi wa miundombinu ya michezo, itakuwa inaitwa Sima. Moja ya kazi kubwa za taasisi hii itakuwa ni kutambua, kufanyia marekebisho na kuhifadhi maeneo mbalimbali ambayo yatakuja kutumika, kwa ajili ya shughuli za michezo. Kwa hiyo, Morogoro na yenyewe ikiwa sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko katika mpango huo kwa sababu hatutaruka hata mkoa mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Josephine ya kwamba nafahamu jinsi Morogoro ilivyotoa vipaji vingi vya michezo na ni miongoni mwa maeneo ambayo

tunayatazama sana ili kupata vipaji kwa ajili ya kulitumikia Taifa hili, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jasmine Ng'umbi.

**MHE. JASMINE C. NG'UMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Swali ni kuwa, je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri walimu walio wabobevu katika masuala ya michezo katika shule, ili kusaidia wanafunzi wadogo kuibua vipaji vyao wakiwa na umri mdogo kuliko kusubiri mtu aje kuibua kipaji chake akiwa ameshaongeza umri zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo la kitaifa.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Jasmine kwa swali zuri. Serikali inaendelea kutoa mafunzo kwa ajili ya walimu wa michezo ambao wanakwenda kufundisha kwenye shule za msingi na kufundisha vijana wakiwa wadogo pale katika Chuo chetu cha Michezo cha Malya. Ni programu endelevu na kila wakati tunaendelea kudahili wanafunzi wengi zaidi ambao wengi ni walimu kwa ajili ya kufanya shughuli hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakar Mussa.

**MHE. ABUBAKAR MOHAMMED MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Serikali kupitia Wizara ya Michezo ina mpango thabiti wa kuinua vipaji vya vijana; je, Serikali haioni haja sasa ya kuanzisha ligi ya muungano kwa vijana wa *juvenile, junior* na *central*, kwa ajili ya kukuza vipaji hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Abubakar kwa swali zuri na la kujenga hasa. Hatujawahi kujadili suala hili, lakini naomba nilichukue kama wazo zuri niendelee kulipitia na wenzangu tuone namna ambavyo tunaweza kulitekeleza jambo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa majibu hayo ya Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Edibily Kazara Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini, aulize swali lake.

Na. 116

**Ujenzi wa Kiwanda cha Saruji, Kasulu**

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Kiwanda cha Saruji *(TACECO Ltd.)* cha Kasulu utaanza kwa kuwa mwekezaji alishapewa eneo miaka mitatu iliyopita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali namba 116 kutoka kwa Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa eneo lililopo katika Kata ya Kagera Nkanda katika Wilaya ya Kasulu lilitolewa kwa mwekezaji wa Kampuni ya *TACECO Ltd.* kutoka nchini Burundi kujenga kiwanda cha saruji. Mwekezaji huyo yupo katika hatua ya

kufanya tathmini ya kina *(feasibility study)* ya upatikanaji wa malighafi kama vile *clinker, gypsum* na *pozolana*. Hata hivyo, kasi yake imekuwa ndogo katika kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea kumhimiza kuhakikisha kwamba mradi huu unaanza utekelezaji haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edibily Kazala.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Swali ni kuwa, nataka Mheshimiwa Waziri awaeleze wananchi wangu wa Jimbo la Kasulu Vijijini kwamba ni *feasibility study* gani ambayo inafanyika kwa miaka mitatu huku unasomba mawe usiku na mchana kwa miaka mitatu kupeleka Burundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, eneo alilopewa mwekezaji kujenga kiwanda, lile eneo analima maharage na mahindi; je, Serikali haioni haja ya kulirudisha eneo lile kwa wananchi ili waendelee na shughuli zao za kawaida wakati yeye anaendelea na tathmini ya kina? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umeelewa swali la kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelielewa.

**MWENYEKITI:** Haya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, naomba kukiri kwamba kasi ya kufanya tathmini ya kina kwa mwekezaji huyu imekuwa ni ndogo katika utekelezaji wa mradi huu ambao ni tegemeo kubwa sana la wananchi wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hatuna taarifa kwamba mwekezaji huyu anafanya shughuli nyingine ya kilimo katika ardhi ambayo tumempatia kwa ajili ya uwekezaji, naomba kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara tumuite mwekezaji huyu, tufanye naye majadiliano, tupange mkakati, kuona kwamba anaenda kutekeleza mradi kwa kadri tulivyokubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nauliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Bunda Mjini zaidi ya miaka 12 limetenga ekari 3,173 kwa ajili ya ukanda wa uwekezaji *(economic zone),* lipo pembezoni mwa ziwa, kuna barabara ya lami. Ni lini mtatuletea wawekezaji wajenge viwanda ili kuinua uchumi wa Jimbo la Bunda Mjini na Halmashauri ya Mji na kutengeneza ajira kwa vijana na akinamama wa Jimbo la Bunda Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama una majibu kutoka Bunda huko.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inazungumzia suala zima la kuhamasisha uwekezaji hasa wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Dira ya 2050 inasisitiza sana kuongeza uzalishaji kwa maana ya idadi ya viwanda na pia kutumia malighafi za ndani katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Mipango na Uwekezaji tumekuwa katika jitihada za kuhamasisha uwekezaji kutoka ndani na nje, lakini sasa hivi tumefanya *mapping* ya maeneo yote ya uwekezaji likiwemo

eneo la Bunda. Kwa hiyo, kazi ambayo tunayo sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunaendelea na hamasa ya kutafuta wawekezaji wa ndani, mashirika, taasisi na wawekezaji binafsi na yeye Mheshimiwa Mbunge naamini kabisa kwamba ana *network,* atusaidie kwenye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia vikao vya Baraza la Madiwani, *DCC* na *RCC* waweke mipango kulingana na malighafi ambazo zinapatikana hapo ili kushirikiana na Serikali tufanye ama tuendeleze hamasa ya kutangaza vivutio katika maeneo ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Othman Maulid.

**MHE. OTHMAN MAULID SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, swali nililotaka kuuliza amelitolea ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ghati Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya swali na pia kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa isiyokuwa na viwanda vinavyofanya kazi na ni mkoa wenye maeneo mazuri ya uwekezaji wa viwanda.

Je, ni lini sasa Serikali imejipanga kuja kuwekeza viwanda katika Mkoa wa Mara maeneo kama ya Tarime Mjini, Bunda Mjini, Musoma Mjini na maeneo yote yanayozunguka Mkoa wa Mara? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama una majibu kuhusiana na Mkoa wa Mara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Ghati kwa swali

lake la nyongeza kuhusiana na hatma ya uwekezaji wa viwanda katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuna swali la msingi kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko ambalo litakuja kuhusiana na Tarime kuwa na viwanda, lakini nakiri kwamba mkakati wa Serikali upo na ndio maana tumeshalipa fidia ya ekari zaidi ya 3,000 katika Wilaya ya Bunda kwa ajili ya uwekezaji. Lengo la Serikali sasa hivi ni kufufua viwanda na ujenzi wa viwanda vipya kama Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na Dira ya 2050 inavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaegele.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejiandaa kuuliza swali la nyongeza katika swali namba 116.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ndio hili swali la 116. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Patali Shida Patali, Mbunge wa Mbeya Vijijini aulize swali.

Na. 117

**Ujenzi wa Barabara Jimbo la Mbeya Vijijini**

**MHE. PATALI S. PATALI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mbalizi - Shigamba na Isyonje – Kikondo ili kuunganisha Wilaya ya Makete?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mbalizi – Shighamba imekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa sehemu ya Mbalizi – Santilya (kilometa 10).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa Barabara ya Isyonje – Kikondo (kilometa 22), ambayo ni sehemu ya Barabara ya Isyonje – Kikondo (Mbeya/*Njombe Border*) – Makete (kilometa 96.2), ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea kwa sehemu ya Makete – Iniho (kilometa 36.3) iliyopo mkoani Njombe na umefikia 28%. Sehemu zilizobaki za barabara hizo zitaendelea kujengwa kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Patali Shida Patali.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali juu ya ujenzi wa barabara hizi mbili, Mbalizi - Shighamba pamoja na Isyonje – Kikondo. Barabara ambazo ni muhimu sana kwa uchumi wa Jimbo la Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza; kwa kuwa kumekuwa kunatokea ajali nyingi Mlima Iwambi kuelekea Mbalizi na kufanya Wana-Mbeya Vijijini kuwa waathirika wakubwa wa ajali hizo, mara ya mwisho mwezi Juni, 2025 tumepoteza watu 28 pale.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya mchepuo kwa kiwango cha lami kutoka Iwambi hadi Mbalizi ili kupunguza msongamano wa magari Mlima Iwambi ambayo itasaidia kupunguza ajali hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametafuta mwekezaji wa takribani shilingi bilioni moja kuwekeza kwenye Mgodi wa Nubian uliopo Songwe, Mbeya Vijijini unaotarajiwa kuanza hivi karibuni, kwa msisitizo wa dhana ya Wizara kusomana na kutengeneza fursa zaidi kupitia miradi mikubwa ya Serikali.

Je, kupitia Wizara ya Ujenzi, haioni kuna haja ya kupanua eneo la maegesho ya magari pale Songwe Viwandani ili kutegeneza mazingira mazuri yatakayokuwa yanahudumu kwenye mgodi huu pamoja na yale yanayoegesha kwenye barabara hiyo hivi sasa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Patali Shida Patali, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *bypass* kwa maana ya Iwambi - Mbalizi ipo kwenye mpango wa kuijenga. Tunavyoongea sasa hivi imeboreshwa na kuna magari yanapita, lakini mpango ni kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, hivi tunavyoongea tayari hata wataalamu wako kwa ajili ya kupitia tena usanifu uliokuwepo ili barabara hii iweze kujengwa na itajengwa sambamba na *bypass* kubwa ya kuanzia Uyole kwenda Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kwamba kuna magari mengi ambayo yanapita barabara hii ya TANZAM, Mbeya kwenda Tunduma likiwepo hilo eneo la Songwe ambapo tumejenga daraja, tumeacha barabara iliyokuwepo ya zamani kwenda kwenye eneo jipya. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo lile linaweza likatumika kwa muda tu ile ambayo ilikuwa barabara ya zamani, kwa ajili ya ku-*park* malori, lakini namkumbusha kwamba hiyo barabara ndiyo tunakwenda kuijenga njia nne. Kwa hiyo, inaweza ikatumika kwa muda kwa ajili ya ku-*park* hayo malori, lakini haitakuwa moja kwa moja kwa sababu tutakwenda kujenga njia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge na halmashauri kwamba waweze kutafuta eneo sahihi, eneo hilo la Songwe Viwandani ili waweze kuwa wana-*park* magari kwa sababu tutakapoanza kujenga njia nne hilo eneo litatumika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza na pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nataka nimuulize; barabara ile ya Mwigumbi – Maswa, Serikali ina mpango gani wa kuijenga kwa kiwango cha lami na kwa ubora ambao upo, ipo ambayo imejengwa, lakini ubora wake haulingani na hali halisi ambayo ipo sasa hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama una majibu ya Maswa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Barabara ya Mwigumbi – Maswa imejengwa kwa kiwango cha lami. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ilikuwa kwa kiwango cha chini ambacho tayari Serikali imeshamchukulia hatua huyo mkandarasi aliyeijenga na bado tunaendelea naye ili aweze kurekebisha maeneo yote ambayo yameonekana yana kasoro kwa mujibu wa mkataba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Masanja.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na naomba niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya kutoka Ngoma – Nansio, Wilaya ya Ukerewe kwa kiwango cha lami yenye kilometa 12, mkandarasi ameenda *site* na amebomoa baadhi ya nyumba, wakitarajia kwamba watalipwa, lakini mpaka sasa hayupo *site*. Je, ni lini Serikali itawalipa hawa wananchi na pia itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pana maswali mawili hapa, ujenzi na suala la fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ujenzi ni kweli, mkandarasi alishaanza ujenzi. Namhakikishia Mheshimiwa Mary Masanja kwamba tuko tunakamilisha malipo yake ambayo ametuletea Wizarani ili aweze kuendelea kukamilisha hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia, namuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba kama watu hao wanastahili ambao hawajalipwa na wamebomolewa nyumba, tuweze kupata taarifa zao sahihi kwa sababu si utaratibu wa Serikali kubomoa nyumba ya mtu wakati anastahili na hajalipwa bado, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yohana Msita.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo langu la Itigi lina barabara yenye urefu wa kilometa 219 kutoka Mkiwa – Itigi – Mitundu – Mwamagembe - Rungwa kwenda Makongorosi. Barabara hii imekuwa na ahadi karibu awamu tatu, Awamu ya Nne, Awamu ya Tano na sasa Awamu ya Sita. Sasa kipande kidogo tu kimejengwa kwa kiwango cha lami na wakandarasi wako, lakini wanasuasua. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha barabara hii ambayo ni kiungo muhimu sana kwa Mikoa ya Mbeya, Tabora na Singida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa kwenda Makongorosi imeanza kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini kwa awamu. Tumeanza kujenga kuanzia Itigi hadi Noranga na mkandarasi amebakiza kilometa chache sana, tena amelipwa ili aweze kukamilisha hilo eneo. Kuanzia Itigi kwenda Mkiwa, kwa maana ya kuunganisha hii Barabara Kuu ya Manyoni kwenda Singida, muda wowote mkandarasi anakwenda *site* kwa ajili ya kuunga Mkiwa –

Manyoni hadi Noranga wakati Serikali inatafuta fedha ya kutoka Noranga kwenda Rungwa hadi Makongorosi Chunya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile Wizara hii ina maswali mengi, basi ninawasisitiza angalau muulize maswali kwa ufupi sana ili wengi mpate nafasi.

Mheshimiwa Hawa Chakoma.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Ni lini Barabara ya Makofia – Mlandizi – Mzenga – Vikumburu kule *Stiegler's* itajengwa kwa kiwango cha lami ikizingatiwa barabara hii inaunganisha majimbo matano ya Bagamoyo, Kibaha Vijijini, Kibaha Mjini, Kisarawe na Rufiji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hii barabara aliyoisema ni kweli barabara ni ndefu, tumeshaanza kuijenga kwa awamu. Makofia – Mlandizi tunatafuta fedha tuweze kujenga, lakini kuanzia Mlandizi tayari tunajenga, ilikuwa ni sehemu ya kukamilisha zile barabara zinazokwenda kwenye *SGR*. Pia katika Wilaya ya Kisarawe tumeshatangaza kazi ya kilometa kama 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunakwenda kwa maeneo kulingana na uhitaji na hasa maeneo ambayo tunadhani yanahitaji kujengwa kwa kuanzia kwa sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haran Sanga.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kuniona, maana dah, nimesimama sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza niipongeze Serikali imekuwa ikitekeleza ujenzi wa madaraja kwenye Barabara

ya Mji Mwema – Somangila – Kimbiji – Pemba Mnazi. Ninaomba niulize swali la msingi, je, ni lini barabara hii ... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni swali la nyongeza Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza swali la nyongeza; je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ndiyo barabara mama ambayo itaenda kuchochea uchumi katika Kata yetu ya Pemba Mnazi, kwa sababu ndiyo kata ambayo ina viwanja vya uzalishaji, *it is industrial area? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunaelekea Pemba Mnazi. Majibu kama unayo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunatambua kwamba eneo analolitaja hilo la Pemba Mnazi ni eneo la viwanda, kwa kulitambua hilo tumeshaanza kujenga. Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba tumeshaanza kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kibada – Tundwi Songani – Kimbiji na sasa hivi tutaanza kutoka Kimbiji kwenda Pemba Mnazi ili kukamilisha lile eneo lote la Jimbo la Kigamboni ambalo sasa hivi limekuwa ni eneo muhimu sana, hasa kwa upande wa viwanda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faraji Buriani.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Swali langu ni kama lsifuatavyo: -

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Masasi Mji kupitia Kata ya Chikunja – Kata ya Lukuledi – Wialaya ya Nachingwea? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hii barabara ilikuwa ni kati ya barabara zile ndefu ambayo ilikuwa

kilometa 175, Masasi – Nachingwea – Liwale, na kwa sasa tutaanzia Liwale tukiwa tunakuja Nachingwea kilometa 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo alilolitaja tuna daraja ambalo tutalijenga, lakini kwa sasa tumeshakamilisha usanifu, kwa hiyo, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuikamilisha hiyo barabara yote, kwa maana ya Masasi – Nachingwea – Liwale.

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea na Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, Mbunge wa Mkinga aulize swali lake.

Na. 118

**Ujenzi wa Barabara ya Mabokweni – Korogwe**

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA** aliuza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mabokweni – Gombero – Mapatano – Maramba – Bombomtoni hadi Korogwe kilometa 127.69?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mabokweni – Korogwe inajulikana kwa jina la *Old Korogwe* – Kwamndolwa – Magoma – Mashewa – Bombomtoni – Mabokweni yenye urefu wa kilometa 127.69. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kwa kuanza na sehemu za *Old Korogwe* – Kwamndolwa kilometa 10 na Maramba JKT – Mtapwa kilometa 10 ambapo taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata makandarasi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kuwapata makandarasi ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja.

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu haya ya kuonesha juhudi ambazo zinatarajiwa kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambayo nimeiulizia inaunganisha zaidi ya majimbo saba ambapo uchumi wa wananchi hao wanategemea barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii pia ikikamilika itaipunguzia foleni barabara inayotoka Segera kuelekea Tanga, hasa kwa kuwa sasa Bandari ya Tanga imefunguka. Tumepata taarifa kutoka mkoani kwamba mkandarasi alipatikana, lakini ikaonekana kwamba ameweka bei kubwa. Tunaona kama kuna ucheleweshaji sana wa taratibu wa kukamilisha barabara hii.

Je, ni lini sasa wakandarasi hawa watapatikana na barabara hii ianze katika mwaka huu wa fedha, kama ambavyo imetengwa katika bajeti ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ni muhimu, lakini nimhakikishie tu Mbunge kwamba tunavyoongea sasa hivi hiki kipande cha Maramba JKT – Mtakwa kimeshakamilika na kimeshatangazwa tayari ili wakandarasi waweze kuiomba na ninadhani baada ya siku 10 tutafungua hiyo *tender*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paschal Chinyele.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wakazi wa Jimbo la Dodoma Mjini tunaishukuru sana Serikali kwa kujenga reli ya *SGR*, hata hivyo, wakazi wa maeneo ambayo yanapitiwa na reli ya

*SGR* wanapata shida kubwa sana ya kuvuka kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine.

Je, ni lini Serikali itachukua juhudi za haraka za kujenga barabara zinazovuka reli ya *SGR* ili kuwapunguzia adha wakazi wa Kata za Kikuyu Kusini, Mkonze pamoja na Zuzu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba nikubaliane kabisa na Mbunge Chinyele, hiyo changamoto si kwa wananchi wa kwako tu Dodoma, ninadhani ni maeneo karibu yote ambayo *SGR* imepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SGR* baada ya kujengwa kuna watu wametenganishwa tu na *SGR*, nyumba iko upande huu upande huu anatakiwa aende kilometa tatu. Serikali ilishaliona, kwa hiyo Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na wenzetu wa TAMISEMI *(TANROADS)* walishakaa, wanapitia upya ili kutafuta namna ya kuhakikisha kwamba hawa wananchi kunakuwa na mawasiliano kwa kujenga *overpass* itakapobidi ama *underpass* ili kuweza kurahisisha mawasiliano kati ya upande mwingine wa *SGR* na upande wa pili wa *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Mbunge ninakushukuru, Serikali ilishaliona na linafanyiwa kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka mitatu sasa kipande cha Mbulu – Garbabi wananchi ambao wamepisha mradi huu hawajalipwa fidia yao.

Je, ni nani anayepaswa kuwalipa wale wananchi fidia katika eneo la mradi huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wote ambao wanapisha mradi ama mradi unawafuata kwa mujibu wa sheria wanalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria, lakini wale wananchi ambao wanakuwa walikuwa ndani ya hifadhi, kwa mujibu wa sheria zetu wanakuwa waliivamia barabara. Kwa hiyo, huwa hawana stahili ya kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna wale ambao barabara imewafuata, ama wamepisha ujenzi na hawakuwa ndani ya wigo wa barabara, ninaomba tuonane ili tuweze kuwatambua, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Baraka Mwamengo, ajiandae Mheshimiwa Thomas Mgonto.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona.

Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Ibanda – *Itungi Port* ambayo tayari Serikali imelipa fidia kwa wananchi wa Kajunjumele?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii barabara ilishatangazwa na ilipata mkandarasi, alianza kazi, lakini baada ya kuona mwenendo wake haufai Serikali ilimwondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ilitangazwa tena upya na tayari mkandarasi ameshapatikana, sasa hivi tupo kuandaa malipo yake ya awali ili mkandarasi mpya aweze kuanza kazi na kuijenga hiyo Barabara ya Ibanda – Kajunjumele. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Thomas Mgonto, ajiandae Mheshimiwa Joshua Nassari.

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Handeni – Kiberashi – Chemba – Kwa Mtoro – Misughaa mpaka Singida kama ilivyo ahadi ya Rais alipokuwa Tanga wakati amefanya ziara?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachia mbali kipande ambacho kinajengwa cha Handeni mpaka Mafuleta, barabara yote hii kama alivyosema tunategemea kuijenga kwa njia ya *PPP* ambapo wenzetu wa *TANROADS* na *TPA* kwa maana ya bandari, wako kwenye majadiliano ya kuona namna ya kuijenga hiyo barabara kwa ubia. Hii ni barabara ambayo inapewa umuhimu mkubwa sana hasa kutokana na ufanisi mkubwa ambao Bandari ya Tanga sasa inafanya ili kurahisisha kusafirisha hiyo mizigo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joshua Nassari, ajiandae Mheshimiwa Twaha Mwakioja.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, nina swali moja kwa Serikali.

Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha sasa mchakato wa ujenzi wa Barabara ya Mererani – *Mbuguni Bypass*, kwa kuzingatia kwamba kuna michezo ya *AFCON* kesho kutwa inayokuja na ndiyo barabara inayo-*serve* kutoka *KIA Airport*?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, b Barabara ya Tengeru – Mbuguni – Mererani tumeshakamilisha usanifu kilometa 28 na tunavyoongea sasa hivi wataalam wapo uwandani kufanya tathmini ya fidia kwa watu ambao watapisha barabara. Tunategemea kwamba siyo tu *AFCON*, lakini katika mpango wa ujenzi wa barabara kwa mwaka ambao tunaandaa

bajeti, tunaamini kwamba hiyo barabara itaingia kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha.

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru tena kwa fursa hii. Ninapenda kuuliza swali la pili la nyongeza kwa barabara inayotokea Handeni – Kang'ata – Mziha – Turiani – Dumila.

Je, ni lini Serikali itaikamilisha barabara hii ili kuipunguzia foleni barabara inayopita Mkata? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tulishaanza kuijenga, kuanzia hii barabara kuu ya Dodoma – Morogoro tumeshajenga kilometa 50 na sasa tutaanza kuijenga ambapo tayari ilishapata kibali cha kuanza kuijenga kuanzia Handeni kuja Turiani kilometa 30. Kwa hiyo, muda wowote hiyo barabra itaanza kujengwa kwanza na kipande cha kilometa 30, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi.

Ninakiri kwamba wiki iliyopita niliuliza kuhusu Barabara ya Utegi – Shirati na Naibu Waziri ulinipa jibu ambalo kiukweli bado wananchi wamenituma tena niulize kwamba ni lini barabra hii ya Utegi – Shirati itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni kati ya barabara ambazo zipo kwenye utaratibu wa kuijenga kwa kiwango cha lami kwa mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zinaendelea, kwa hiyo na mwaka unaokuja wa fedha pia itakuwepo ikiwa ni pamoja na kwamba tupo kwenye utaratibu ule ule wa kuitangaza muda wowote katika mwaka huu wa fedha na ule unaokuja tutaendelea nayo hiyo Barabara ya Utegi – Shirati. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mbunge wa Tanga Mjini.

Na. 119

**Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Saadani hadi Makurunge**

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Saadani hadi Makurunge kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Saadani hadi Makurunge yenye urefu wa kilometa 256 kwa kiwango cha lami kwa awamu nne. Awamu ya kwanza ni ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani kilometa 50 ambapo umefikia 77%. Awamu ya pili ni ujenzi wa Daraja la Mto Pangani pamoja na barabara unganishi yenye urefu wa kilometa 14 ambapo ujenzi umefikia 80.16%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya tatu ni ujenzi wa Barabara ya Tungamaa – Mkwaja – Kwamsisi hadi Mkange kilometa 92.5 ujenzi wake umefikia 57.38%. Aidha, sehemu ya nne iliyobaki ya Mkange – Makurunge kilometa 75, usanifu umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuanza ujenzi wa barabara hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Barabara ya Tanga – Pangani mpaka kufikia Makurunge, makutano ya Barabara ya Bagamoyo – Msata – Dar es Salaam ni barabara ya kimkakati sana kwa sababu ni barabara inayounganisha nchi mbili. Inaunganisha Kenya kupitia Mombasa na inaunganisha Tanzania kupitia Tanga, lakini inakwenda vilevile mpaka Lindi na Mtwara Kusini kutokea Msumbiji. *(Makofi)*

Swali langu la msingi limejikita lini sasa ujenzi wa barabara hii utakamilika? Hiyo michakato yote ya uendeshaji sisi tunaijua ipo na inaendelea. Tunataka kujua ni lini? Hii ni *project* lazima iwe na *timeframe*. Imeanza, lini itakamilika? Mwakani, mwaka kesho, mwaka huu? Tunataka majibu lini hii barabara itakamilika? Hilo ni swali la kwanza, nipate majibu ya *timeframe* lini. *(Makofi)*

Swali la pili, barabara hii watu walivunjiwa nyumba zao, watu wakatokwa na machozi sana, leo wamebakiwa wanamwagiwa vumbi. Kuna walioshinda kesi mahakamani, je, Waziri yuko tayari niwalete watu hao walipwe fidia walioshinda kesi zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu nimkumbushe Mbunge kwamba hii barabara tumesema inajengwa kwa awamu, kwa maana awamu ziko nne. Katika hizi awamu zimeanza kwa muda tofauti, kwa hiyo zitakamilika kwa muda tofauti ili kuikamilisha barabara yote hii yenye urefu wa kilometa 256.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kipande cha kilometa 75 ambacho bado hatujampata mkandarasi na Serikali inaendelea kutafuta fedha. Kwa hiyo, hatuwezi kusema barabara yote itakamilika lini. Ingekuwa ni *lot* moja tunaweza tukaisemea, lakini kwa barabara yote hatuwezi tukasema lini itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mbunge kwamba hata Serikali kufanya jitihada zote hizi za kukamilisha tunatambua umuhimu huo wa barabara ambayo inatoka Kenya hadi Lindi, ni barabara ambayo inapita Pwani yote ya Afrika Mashariki kuanzia Kenya hadi kule Kusini Mtwara. Kwa hiyo, Serikali imeipa uzito mkubwa sana na ndiyo maana unaona tunaijenga barabara yote kwa ukubwa wake na wakandarasi watatu wako *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hao wananchi ambao wameshinda kesi, ninaomba nimhakikishie hilo ni suala la kisheria. Ninamwomba Mbunge kabla hajawaleta wananchi ni vema tukaonana naye tuone kama kuna ulazima wao kuja ama wanatakiwa tu walipwe wakiwa hata huko huko Tanga.

Kwa hiyo, ninamwomba Mbunge baada ya hapa tuweze kuonana naye mimi pia na wataalam wanaohusika, tutashauriana halafu tuone tuwafuate hao wananchi badala ya wao kutufuata hapa Dodoma, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alan Mvano na baadaye Mheshimiwa Fagason, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kakonko ina jumla ya kata 13, kata nane zinapakana na nchi jirani ya Burundi. Watu wa Mgunzu, Katanga, Gwanumpu, Rugenge, Gwarama, Muhange, Nyabibuye wote hao wanapakana na nchi jirani ya Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yale ni ya milimani na wanafanya biashara za mpakani. Tunayo barabara ambayo imepandishwa hadhi tayari iko chini ya *TANROADS* kilometa 41.43 ambayo inatoka Kakonko kuelekea mpaka wa Muhange ikipitia Gwarama.

Je, ni lini Serikali au mpango wa Serikali ni upi ili kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami iweze kuwanufaisha wananchi wa Kakonko? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayotajwa ilikuwa chini ya Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA)* na imeshapanda hadhi ya kuja *TANROADS*. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mbunge kitu cha kwanza tutakachofanya, ni kuijenga hii barabara kwa viwango vya *TANROADS* na baada ya kufanya hivyo itakuwa sasa ni kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili Serikali ikishajua gharama basi iweze kuijenga kwa kiwango cha lami kwa sababu ni barabara ambayo inaunganisha nchi na nchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fagason.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami pia niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbogwe linalo changamoto kubwa ya barabara; barabara inayotoka Masumbwe kuelekea Kasosobe ambako ndiyo makao makuu ya Jimbo la Mbogwe. Je, ni lini sasa Serikali itakuja kujenga barabara hii inayotoka Masumbwe – Kasosobe – Lulembela yenye kilometa 83? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mbunge kwamba sasa hivi tumeelekezwa kuunganisha barabara zote zinazotoka makao makuu ya wilaya ama halmashauri na barabara kuu ama makao makuu ya mkoa kwa kiwango cha lami. Hivyo, jambo la kwanza tutakalofanya ni kuifanyia usanifu hiyo barabara halafu tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami kadri fedha itakavyopatikana. Mbunge atakubaliana nami kuwa, tumejenga daraja kubwa sana

katika yale madaraja ya dharura katika barabara hiyo ambayo ilikuwa na adha kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, jambo la kwanza tutakalofanya ni kuifanyia usanifu hiyo barabara halafu tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami kadri fedha itakavyopatikana. Mbunge atakubaliana nami kuwa, tumejenga daraja kubwa sana katika yale madaraja ya dharura katika barabara hiyo ambayo ilikuwa na adha kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dickson na Mheshimiwa Florent, nimewaona. Mheshimiwa Dickson Villa.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Kinyanambo A, Madibila mpaka Lujewa, Halmashauri ya Mji wa Mafinga tulipewa kilometa 1.2 kujengwa kwa lami, na tayari mkandarasi alishakuwa ameanza kazi ya ujenzi wa hiyo kilometa 1.2, lakini baadaye akatoweka. Naomba kauli ya Serikali, mkandarasi atamaliza lini barabara hii, kwa sababu wakati wakifanya maandalizi ya kuweka lami, walifumua sana eneo lile na linaleta kero kwa wananchi kwa ajili ya vumbi pamoja na matope? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hiyo kilometa moja na nusu, ninaomba kwanza niongee na Mheshimiwa Mbunge, na pia nitoe maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Iringa aweze kutupatia taarifa kuhusiana na changamoto ambayo imetokea kwenye hiyo kilometa moja na nusu, mkandarasi huyo kutoweka na huku ameshaifumua barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitalifuatilia ili kuhakikisha kwamba mkandarasi anarudi *site* na anakamilisha kipande hicho, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Serikali iliahidi kujenga barabara ya lami Mtukula kwenda Mizilo. Ninaishukuru Wizara ya Ujenzi wameshaanza ujenzi wa awali wa barabara ya changarawe kilometa sita, bado kilometa takribani nane. Mheshimiwa Naibu Waziri alifika pale Mtukula na akaona. Sasa hivi ni miaka mitatu hakuna kinachoendelea. Je, ni lini sasa barabara hiyo ambayo ni ahadi ya kiongozi wa Kitaifa itakamilishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara hii kulikuwa na maeneo ya kuifungua upya kabisa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, cha kwanza ni kuanza kuifungua na kuifanya barabara yote ipitike kuwa kiwango cha changarawe wakati tukiandaa fedha ya kufanya usanifu kwa ajili ya kuiandaa kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Phillipo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi alifika Songwe tarehe 20 mwezi wa Sita mwaka jana, 2025 akiwa na Mkuu wa *TANROADS* na mkandarasi ili kuja kumkabidhi barabara ya kutoka Mkwajuni mpaka Saza, ambacho ni kipande cha kutoka Mbarizi mpaka Makongolosi. Hata hivyo, hadi leo mkandarasi yule amepotea, hajaripoti na hali ya barabara ni mbaya sana. Je, Serikali ina kauli gani kwa mkandarasi wa aina hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alichosema Mheshimiwa Mulugo Mbunge wa Jimbo ama Wilaya ya Songwe. Nimhakikishie tu kwamba, mkandarasi ameshaleta maombi ya kulipwa fedha ya awali, na Serikali tupo, tunaandaa kumlipa fedha ya awali ili aweze kuanza kukusanya vifaa *(mobilization)* na kuanza kufanya hiyo kazi.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, ninaamini mmeona kuwa Mheshimiwa Waziri anajua maeneo mbalimbali ya barabara zetu nchini. Kwa hiyo, hata mkipunguza maswali kwa Wizara ya Ujenzi bado kazi inaendelea vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba sasa aulize swali lake.

Na. 120

**Kugawa Matrekta kwa Wakulima**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza: -

Je, upi mpango wa Serikali wa kugawa matrekta kwa mkulima mmoja mmoja ili kuondokana na jembe la mkono?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali siyo kugawa matrekta kwa mkulima mmoja mmoja, bali ni kuhakikisha kuwa huduma za zana za kilimo zinapatikana karibu yake na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imeanza utekelezaji wa mpango wa kununua na kusambaza matrekta 10,000 ambayo yatasambazwa katika vituo vya huduma za zana za kilimo 1000 ifikapo mwaka 2030. Mpango huu ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Desemba mwaka 2025 vituo jumuishi vya kutoa huduma za zana za kilimo 79 vimeanzishwa katika halmashauri mbalimbali nchini ambapo matrekta makubwa 592, matrekta madogo ya mkono 800 na mashine 11 za

kuvunia mazao ikiwemo mpunga, mahindi, alizeti na ngano zimesambazwa katika vituo hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Jimbo la Momba ambalo lina wakazi 259,000 *plus,* na likiwa ni watu ambao ni nguvu kazi, nikimaanisha wapigakura 135,000 *plus*. Zaidi ya 80% sisi watu wote ni wakulima, lakini kwa miaka mitano iliyopita huko nyuma, mwaka 2025, tumepata matrekta matano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa dhana ya Serikali ni kuuza matrekta kwa bei nafuu na kwa karibu, Mkoa wa Songwe ni kati ya mikoa ile ya *big five* ambayo inazalisha chakula hapa nchini. Je, kwa Jimbo la Momba na kwa Mkoa wa Songwe ni mahali gani wameweka kituo cha kuuza hayo matrekta kwa bei nafuu na kwa ukaribu ili kuwasaidia wanachi wa Jimbo la Momba ambao ni wazalishaji wakubwa katika Mkoa wa Songwe, na Taifa kwa ujumla ikiwa katika hiyo mikoa mitano niliyoitaja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mheshimiwa Rais wetu alipolihutubia Bunge la Kumi na Tatu alitoa kauli nzito akisema kuwa kipindi hiki tutakwenda na dhana ya kumfanya mkulima kuwa mwekezaji na kilimo kuwa biashara. Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wote wamepewa dhamana kubwa na Mheshimiwa Rais kumsaidia kwenye jukumu hili zito. Je, wamejipangaje kumsaidia mkulima wa Tanzania na hususan wale wa Momba ambao mpaka sasa wanalima kwa kutumia jembe la mkono?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, anasema, tunataka kumfanya mkulima awe mwekezaji. Atakuwaje mwekezaji bado analima kwa kutumia jembe?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimjibu Mheshimiwa Condester Michael

Sichalwe, Mbunge wa Jimbo la Momba na dada yangu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, nimthibitishie tu kwamba Serikali ya Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan itawawezesha wakulima katika mikoa yote nchini, ikiwemo Mkoa wa Songwe na Jimbo la Momba. Moja ya mkakati tuliyonayo, kwanza, kwenye *issue* ya biashara ya vifaa kama matrekta, Serikali haifanyi moja kwa moja, isipokuwa tunatumia sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mpango tulionao, tumeshazungumza na baadhi ya wale wauzaji wakubwa wa matrekta kuja kufungua kituo pale Momba. Vilevile, kuhusu haya matrekta ambayo sisi tunaweka katika vituo, halmashauri zote nchini, tutaweka vituo kwa ajili ya wakulima kwenda kukodi yale matrekta katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vituo hivi vitakuwepo. Tunduma kitakuwepo kituo cha *mechanization center*; Momba kitakuwepo kituo cha *mechanization center,* na halmashauri zote nchini tutafanya hivyo. Kwa hiyo, hilo ni moja ya jambo ambalo tunalifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ambao tumejipanganao ili kuwawezesha wakulima wa Momba na kuhakikisha kwamba tunawaondoa katika kilimo cha jembe la mkono ni pamoja na kuweka hiyo *mechanization center* na kumfanya mkulima kuwa mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mpango mkubwa tulionao ni kuongeza miradi ya umwagiliaji pale. Unajua tunakwenda kufungua mabonde ya Kamsamba, Kasinde, na Chitete pale, yote yale. Miradi hii mikubwa itagharimu mabilioni ya shilingi, takribani shilingi bilioni 400 kwa ujumla wake. Kwa hiyo, huo ndiyo mpango wa Serikali katika Jimbo la Momba. Nimhakikishie tu, hadi mwaka 2030 utakuwa katika utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timida Mpoki, kama una swali la nyongeza kuhusiana na matrekta.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali. Binafsi nina swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeonesha nia ya dhati ya kuwekeza kwenye kilimo. Je, Serikali ina mpango gani kwa vijana ambao wamehamasika kuwekeza katika sekta ya kilimo, lakini wana changamoto kubwa ya masuala ya pembejeo, ili kuweza kuwafanya waweze kukua kiuchumi na pia kuweza kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo la Kitaifa kwa vijana, kama unayo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tuna mpango mzuri sana kwa vijana, hususan wale wote wanaotaka kuingia katika sekta ya kilimo. Sehemu ya Mpango tulionayo ni pamoja na: moja, tumesema vijana wote wanaotaka kuingia katika kilimo kuna mpango madhubuti wa *BBT* (Jenga Kesho Iliyobora). *BBT* ambayo tunakwenda kuifanya sasa hivi ni kuhakikisha kuwa katika halmashauri zote 184 tutapeleka mpango wa BBT katika hizo halmashauri ambapo vijana na akina mama watakuwa ni sehemu ya mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kutumia benki zetu: Benki ya Kilimo, Benki ya Ushirika, pamoja na Mfuko wa Pembejeo *(AGITF)* kuendelea kutoa mikopo kwa bei nafuu. Vilevile tutaendelea kuwapa elimu kuhusu kilimo bora na cha kisasa ambacho vijana ndio watakaokuwa wanufaika wakubwa. Pia, Mpango wa Serikali wa kutoa ruzuku kwenye pembejeo utaendelea ili kuhakikisha kuwa tunampunguzia mkulima gharama katika kilimo chake.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Kilimo. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa aulize swali lake.

Na. 121

**Hitaji la Majisafi Kata ya Manda**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha taratibu za manunuzi ili wananchi wa Lutala Kata ya Manda wapate huduma ya majisafi na salama?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi minane katika Wilaya ya Ludewa kwa gharama ya shilingi bilioni sita ambapo inalenga kuwanufaisha zaidi ya wananchi 33,000 waishio katika vijiji 17 vya wilaya hiyo. Baadhi ya miradi inayotekelezwa ni pamoja na Luvuyo, Mawengi, Mavanga, Igalu - Lupingu na Kipingu - Ngelenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha kuwa miradi yote inayoendelea inakamilika na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi kabla ya kuanzisha miradi mipya. Hata hivyo, Serikali imekamilisha usanifu wa upanuzi wa mradi wa kutoka Skimu ya Ilewa kwenda kwa wananchi wapatao 1,256 waishio katika vitongoji vya Lutara Kata ya Manda na Idusi Kata Mkomang'ombe vilivyopo Wilaya ya Ludewa Mkoani Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha taratibu za manunuzi ya kuajiri mkandarasi atakayetekeleza mradi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwani tulizungumza juu ya mradi wa Maji wa Ludewa, na leo nimepata taarifa kuwa mabomba yanaanza kwenda kushuka pale. Kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja, Mji wa Mlangali ni mji ambao unakua kwa kasi, una idadi kubwa ya watu, na taasisi nyingi na pana, lakini kuna changamoto kubwa sana ya maji. Je, Serikali ina maelekezo yapi kwa wataalamu ili waende kuhuisha *feasibility study* ya Mto Salali ili kuweza kuhudumia eneo kubwa zaidi la Kata la Mlangali ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ; Serikali imetumia zaidi ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya kujenga Mradi wa Madope, lakini chanzo kile inaonekana kipo bondeni sana, maji yanashindwa kupanda mlima, licha ya tenki kuwa zuri sana. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuchimba kisima kirefu, kwa sababu Serikali imenunua mitambo ili iweze kujaza maji kwenye tenki na kuhudumia wananchi ?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mbunge machachari na Mbunge anayewatumikia wananchi kwa kuhakikisha kwamba sekta ya maji ndani ya jimbo lake inaendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, itaendelea kusikiliza na kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili kuhakikisha kwamba Ludewa inapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na Mradi wa Kata ya Mlangali. Mlangali ni kata ambayo ina wakazi wengi, takribani 15,000, na tunafahamu kabisa kwamba kuna chanzo chake pale cha Salali. Kikubwa ni kwamba mradi unapofanyiwa usanifu *(feasibility study)* kwa muda mrefu ikishapita miaka mitano ni lazima tufanye mapitio ya *feasibility study*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwagiza *RM* Mkoa wa Njombe, kuhakikisha kwamba hili suala anaenda kulifanyia kazi haraka sana, na ndani ya mwezi huu liweze kupata mrejesho ili tuone hatua ya kuchukua kulingana na mapitio ya *feasibility study* itakayokuwa imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ; ni kweli kabisa, ninaomba uniruhusu nisahihishe kidogo katika takwimu za Mheshimiwa Mbunge. Ule Mradi wa Madobe unagharimu shilingi milioni 580 na siyo shilingi milioni 600. Kwa hiyo, mradi huu ambapo tenki hili lililojengwa lenye ujazo wa lita 150,000, ni kweli kabisa kwamba kile chanzo kilishindwa kupandisha maji kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachokielekeza ni kwamba, *RM* Mkoa wa Njombe atoe majibu ya namna gani usanifu ulifanyika na matokeo yake, maji yasipande kwenye tenki. Wakati tunafanya tathmini hiyo, watafute mbinu mbadala ya wananchi wa eneo hili kuendelea kupata huduma ya majisafi na salama, na baada ya hapo, tutamhusisha Mheshimiwa Mbunge ili kuona kwamba wananchi wake wanasaidiwa namna gani.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali unaelekea kwisha, tunaendelea na Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, aulize swali lake.

Na. 122

**Mradi wa Maji Kikombo - Ving'hawe Mang'hangu - Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Mradi wa Maji wa Kikombo, Ving'hawe hadi Mang'hangu utaanza kutekelezwa katika Jimbo la Mpwapwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi maji kwa kutumia visima virefu viwili vya Kikombo vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita 1,580,000 kwa siku. Mradi huo unalenga kunufaisha zaidi ya wananchi 51,000 wa Mpwapwa Mjini hususan maeneo ya Kikombo, Ving'hawe na Mang'hangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa kazi zitakazofanyika kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa vyumba ya mitambo *(pump house),* ujenzi wa tenki moja lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita 200,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 55.8 sanjari na ujenzi wa vituo saba vya kuchotea maji vya malipo ya kabla *(prepaid water points*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huo unaotarajia kugharimu zaidi shilingi bilioni 6.3.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jibu hili la Serikali, nina swali moja la nyongeza. Mradi huu ulianza kwa kuchimba visima viwili katika eneo la Kikombo mwaka 2021, baada ya kuchimba visima hivi viwili hakuna kilichoendelea mpaka leo. Bunge lililopita niliuliza maswali mara mbili kuhusu mradi huu, na sasa nimeuliza mara ya tatu kuhusu mradi huu. Je,

Serikali ina tamko gani? Maana wananchi wa Mpwapwa wamechoka kusikiliza majibu ya aina hii. Ninaomba Serikali sasa iseme, ni lini hasa mradi huu utaanza kutekelezwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Malima. Kwa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya jimbo la Mheshimiwa Malima ametekeleza miradi 13 yenye gharama ya shilingi bilioni 2.9, na bado kuna miradi miwili inaendelea kutekelezwa yenye gharama ya shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ni hatua kwa hatua. Tunamaliza mradi mmoja, tunakuja mradi mwingine. Hii miradi miwili inayoendelea itakapokamilika, na huu mradi wa shilingi bilioni 6.3 Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, itaitekeleza na wananchi wa Mpwapwa watapata huduma ya majisafi na salama.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, muda wa maswali unaendelea kwisha. Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mbunge wa Kyerwa.

Na. 123

**Uhitaji wa Majisafi Jimbo la Kyerwa**

**MHE. KHALID M. NSEKELA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji kwenye Vijiji vyote 99 na Vitongoji 670 vya Jimbo la Kyerwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Musa Nsekela, Mbunge wa Jimbo la Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama wilayani Kyerwa Mkoani Kagera imeendelea kuimarika mara baada ya kukamilika kwa jumla ya miradi 19 mwaka 2025 na kuweza kufikisha huduma ya majisafi kwenye vijiji 55 kati ya vijiji 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa minne ya Kaisho - Isingiro, Runyinya - Chanya, Kimuli – Rwanyango - Chakalisa na Kikukuru na ipo hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo ikikamilika itanufaisha vijiji 30 vya Wilaya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kuendelea kuboresha zaidi huduma ya maji wilayani Kyerwa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa kwa kutumia maji ya Mto Kagera kwa lengo la kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji 26 ikiwemo vijiji 14 ambavyo vitakuwa havijafikiwa na huduma hiyo kupitia miradi iliyopo na inayoendelea. Mradi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 58.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalid Nsekela.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, ninashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunasubiria miradi hii mikubwa iweze kukamilika wananchi wa Kyerwa bado wanaendelea kuwa na shida kubwa ya maji. Sasa tunatambua Serikali hii sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilinunua mitambo mikubwa ya kuchimba visima kila mkoa. Je, Mheshimiwa Waziri anaridhia na yuko tayari niambatane na wataalamu wake tukachague maeneo machache ili wachimbe visima ili wananchi hawa wapate angalau matumaini ya kupata maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, ni lini Serikali itakuwa na mkakati madhubuti na makusudi kupeleka majisafi, salama na

toshelevu katika hizi taasisi za kutoa huduma kama shule za bweni na Kituo cha Afya cha Kamuli? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sera yetu ya Taifa ya Maji inaelekeza kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma ya majisafi na salama na maji yenye utoshelevu. Ninatambua kabisa kwamba mahitaji makubwa ya Jimbo la Kyerwa ni katika kuhakikisha kwamba maeneo mbalimbali yanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumwelekeza *RM* Mkoa wa Kagera aungane na Mheshimiwa Mbunge kwenda kuangalia na kufanya tathmini na kujiridhisha ukubwa wa tatizo na baadaye watushauri tuchukue hatua gani kulingana na tatizo ambalo litakuwa limebainika kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya usanifu wa mradi wa kutumia maji kutoka Mto Kagera. Mradi huo utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 58 na utakapokamilika tutazingatia kuhakikisha kwamba tunafikisha maji kwenye shule za bweni, vituo vya afya na maeneo mengine taasisi za umma ambao watahitaji majisafi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, Mbunge wa Mbozi, aulize swali lake.

Na. 124

**Wananchi Kupewa Kipande cha Ardhi Hifadhi ya Isalalo**

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa kipande cha ardhi wananchi wanaozunguka Hifadhi ndogo ya Isalalo iliyo chini ya *TFS*?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Onesmo Merdson, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Msitu Isalalo ilianzishwa mahususi kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kuhifadhi mimea na wanyama, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kuhifadhi udongo. Hii inatokana na ukweli kwamba msitu huu unazungukwa na vijiji vitano ambavyo ni Itentula na Hamwelo (Kata ya Itaka), Nambizo, Ipapa, na Utambalila (Kata ya Nambizo) ambavyo ni muhimu kulinda mazingira yake ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kiikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa haina mpango wa kumega hifadhi hiyo kwa matumizi ya kibinadamu. Hivyo, Serikali inashauri wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo kuzingatia Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ili kukidhi mahitaji yao ya sasa na baadaye kwa manufaa ya vizazi vyote. Aidha, Serikali inawaruhusu wananchi kuendesha shughuli ambazo hazikinzani na uhifadhi ndani ya hifadhi kama vile ufugaji nyuki ambao baadhi ya wananchi tayari wameanza kufanya shughuli hizo katika hifadhi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Onesmo Mnkondya.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili. Jambo la kwanza, kwa kuwa wananchi wa maeneo haya wa Itentula na Hamwelo (Kata ya Itaka), Pangala, Kata ya Halungu na wananchi wa Ipapa, Nambizo na Utambalila wa Kata ya Nambizo wana uhaba mkubwa wa ardhi ya kuendeshea shughuli zao za kilimo na ndicho kilimo chao; mpaka sasa hii ardhi

imeshakosa sifa ya kuitwa hifadhi, kwani haina wanyama hata wa kufugwa, hata sungura hayupo pale lakini pia haina vyanzo vya maji lakini pia mimea ya asili miaka 20 iliyopita imeshapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni haja sasa ya kuwapa wananchi wa maeneo haya kipande hiki cha ardhi ili waweze kuendesha shughuli zao za kilimo kuendana na sera ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo inataka mkulima au mwekezaji na pia kilimo kiwe biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa mimi ni mwakilishi wa walio wengi, na ndio walionituma nije hapa niwaletee swali na maombi haya, na wanasubiri nikirudi niweze kuwapelekea mrejesho wa swali hili. Je, yuko tayari baada ya Bunge hili kuambatana na mimi kwenda kwenye hifadhi hii; jambo la kwanza, kwenda kuwasikiliza; na pia kuona hali halisi ilivyo na kujiridhisha hifadhi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kabla ya kujibu maswali ya ndugu yangu Mheshimiwa Onesmo nimpongeze sana, maana yake kila uchao yupo ofisini anafanya mawasiliano kuhakikisha kilio cha wananchi wetu kinaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Mbunge kwa sasa awe na subira kwanza, ili tuone taratibu baada ya kwenda huko na mimi nikaona pamoja na wataalamu wetu tuone utaratibu ukoje, kwa sababu ni vigumu sana kwa sasa kumega sehemu ile ya hifadhi kuipeleka kwenye shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie kwamba mimi niko tayari kwenda kuona hali halisi ya eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mbunge wa Moshi Mjini.

Na. 125

**Mafunzo kwa Wapagazi *(Porters)***

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufadhili mafunzo kwa Wapagazi *(Porters)* kwenye Vyuo vya *VETA* ili kuwaongezea ujuzi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali imeanza kuchukua hatua za kurasimisha mafunzo kwa Wapagazi kupitia Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka kilichopo Moshi Mkoani Kilimanjaro na kuandaa mpango wa kujenga kituo atamizi pamoja na mtaala wa mafunzo ya Wapagazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika kuhimiza vyuo mbalimbali nchini, ikiwemo *VETA* kuwa na programu za mafunzo kwa wadau walio katika mnyororo wa huduma za utalii ikihusisha wapagazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa maandalizi ya programu hizo, Serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* itashirikiana na wadau mbalimbali katika kuwezesha utekelezaji wa programu za kuwaongezea ujuzi wapagazi kama ambavyo imekuwa ikifanyika kwa waongoza watalii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ibrahim Shayo.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, ni lini Serikali itaona kuna umuhimu sasa wa hawa wapagazi na waongoza watalii kuhakikisha kwamba

wanaweza kupata bima ya afya kwa kuweza wao wenyewe kuchangia kutokana na vyama vyao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni lini Serikali itaweka mfumo wa hawa watalii, wageni au wenye makampuni ya utalii kuweza kuwalipa hawa vijana malipo yao stahiki kwa wakati sahihi na kwa kiwango sahihi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Shayo kwa maswali mafupi ya Kibunge. Maswali kama haya ndiyo yanatakiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimpongeze sana ndugu yangu Mheshimiwa Shayo kwa namna anavyofuatilia vijana wetu hawa wapagazi na waongoza watalii. Kwa hakika ni Mbunge ambaye yuko sambamba na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa bima ya afya kwa wapagazi hasa kulingana na mazingira ya kazi yao. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko pamoja nao, na tayari imeshatoa wito na inaendelea kutoa wito kwa mashirika yao kupitia vyama vyao, wajiunge na Mfuko wa Bima ya Afya ili kusudi kila mmoja na mwenyewe awe na bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maslahi sawa kwa wapagazi, Serikali inalitambua hili, lakini malipo wanayopata wapagazi ni kulingana na mikataba ambayo waliingia na waajiri wao. Hata hivyo, Serikali inatoa wito kwa waajiri kuangalia kutoa malipo yaliyowiana, yaani kusiwe na tofauti kubwa sana na Serikali inafuatilia hili siku hadi siku kwa kupitia hata mikataba yao ambayo wanayowaajiri kati ya waajiri na waajiriwa. A *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tunamalizia na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa *Eng.* Kija Limbu Ntemi, Mbunge wa Katoro, aulize swali lake.

Na. 126

**Gari la Zimamoto – Katoro**

**MHE. ENG. KIJA L. NTEMI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka gari la Zimamoto Katoro ili kutoa huduma kwa wakati inapotokea dharura?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba unipe ruhusa nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yake ni kubwa sana, lakini ninatambua dhamana hii ni kubwa, inahitaji Mwenyezi Mungu aweze kuniongoza, na hivyo ninashukuru sana pia viongozi: Mheshimiwa Makamu wa Rais, pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, na viongozi wa mhimili huu; Mheshimiwa Spika na viongozi wote. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge nikiwa na matumaini kwamba tutafanya kazi kwa pamoja na kwa kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana kwa kuchaguliwa na wananchi, na nina imani kubwa kwamba tutafanya kazi hii kwa pamoja kwa uaminifu na kwa utii usiogawanyika kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ya Mambo ya Ndani tunawaahidi tutafanya mabadiliko na tutafanya kazi kwa kuhakikisha kwamba tunaleta matokeo chanya na kuhakikisha tabasamu la wananchi ambalo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliloliahidi kwa Watanzania tunalifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Kija Limbu Ntemi, Mbunge wa Jimbo la Katoro kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendea kazi. Aidha, Jimbo la Katoro tayari limepatiwa gari moja jipya la zimamoto na uokoaji aina ya *IVECO* ambalo liko Mkoani Dar es Salaam na linatarajiwa kufika Mkoani Geita tarehe 9 Februari, 2026. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Eng.* Kija Ntemi.

**MHE. ENG. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Pia, ninamshukuru Waziri Katambi kwa majibu mazuri. Kwanza, nimpongeze kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na tunaamini yeye ni mtu wa vitendo na nimeona kitendo chake kwamba tarehe 9 Februari, gari litakuwa Katoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina maswali mawili, moja ameshalijibu, maana nilikuwa ninatamani kuuliza kwamba lini gari litafika Katoro? Amejibu, ni tarehe 9 Februari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Gari linakuja Katoro kweli tarehe tisa, lakini ni namna gani watendaji wake, wale Askari watakaokuja kusimamia sehemu ya kujisitiri? Ni changamoto. Mimi nimekuwa nikizungumza na Polisi kwa muda mrefu, wana changamoto atakapoleta gari. Je, wataishi wapi kwa ajili ya matumizi yao kwa ajili ya kuhudumia wananchi? Ninaomba anisaidie kwamba, atakapoleta ile gari, watakaa wapi ili waweze kuratibu mambo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba ardhi ili tuweze kupata sehemu ya kujenga kituo cha zimamoto, lakini tukajibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba zoezi hilo ni Wizara ya Ardhi, lakini leo ninyi mmepata ardhi, mnajenga Geita kituo kipya cha zimamoto…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeshaliuliza swali, na Mheshimiwa Waziri amelielewa.

**MHE. ENG. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Basi ninaomba Mheshimiwa Waziri, anijibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tayari tuna hatua za utwaaji wa ardhi katika eneo la jimbo lake pale Katoro kupitia Halmashauri ya Geita, na kutakuwa na kikao kwa wiki ijayo ambapo kitajumuisha Mkurugenzi wa halmashauri pamoja na Idara ya ardhi ikiwa ni pamoja na Mamlaka yetu ya Zimamoto na Uokoaji (Jeshi la Zimamoto na Uokoaji) ili waweze kupata eneo ambao wataliainisha na ujenzi uweze kukamilika kwenye hilo eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira njema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuwepo na hata sasa tuna miradi zaidi ya 10 katika mikoa ya ujenzi wa *fire brigades* kwa maana ya ngazi ya mikoa, lakini pia tuna miradi tisa katika wilaya na tuna chuo kimoja ambacho kiko katika hatua ya ujenzi na mradi mwingine wa makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hivi vitu vinaenda siyo pamoja na vifaa tu kuboresha yale mazingira ya kazi, ni pamoja na magari 49 ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshayaleta na tumeshayagawa kwenye mamlaka mbalimbali za mikoa zaidi ya 35 ambayo ni *fire tenders* pamoja na *rescue tenders* ambazo tunaendelea kuzitoa kwenye kila mkoa kulingana na uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha. Niendelee kuwasisitiza wote kujifunza kuuliza maswali

mafupi ya Kibunge. Ninajua kuna baadhi ya maswali yanakuwa na hoja; hoja ziwe fupi sana ili Mheshimiwa Waziri aweze kuelewa swali linakusudia nini?

Waheshimiwa Wabunge, vinginevyo, tutakosa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza, na siyo vizuri Mwenyekiti kumwambia Mbunge uliza swali. Huko jimboni itaonekana bado hujaelewa. Kwa hiyo, ninaomba sana mjifunze ili pale ambapo mnauliza, basi msikatizwe na Kiti.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nina matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Kuna wageni saba wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, Mbunge na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambao ni wawekezaji kutoka Kampuni ya *Southern Highland Hidden Wonders*. Karibuni sana, Wawekezaji wetu. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, kutoka Timu ya Mabadiliko Chanya ya Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Vilevile, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, Mbunge ambao ni marafiki zake na wafanyabiashara kutoka Mpanda Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Chamazi, Mkoani Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni pia ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni Ndugu Joshua Kadama kutoka Jijini Dar es Salaam, na Ndugu Amina Ahmed kutoka Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 39 kutoka Chuo cha Maendeleo na Ujasiriamali cha Jijini Dodoma. Karibuni sana, wanafunzi. *(Makofi)*

Tunao wageni 65 kutoka Jumuiya ya Wanafunzi Wanaosoma Udaktari, Chuo Kikuu cha Dodoma (TAMSA). Karibu sana, wanafunzi kutoka Chuo cha Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna kikundi cha sala kutoka Kanisa la *Catholic,* Parokia ya Kiwanja cha Ndege, Jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu. Karibu wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, tunalo tangazo kwa Wabunge Wanawake. Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania *(TWPG),* unawatangazia Wabunge Wanawake wote kwamba leo tarehe 4 Februari, 2026 mara baada ya kusitishwa kwa Shughuli za Bunge sasa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Wabunge wote wanawake katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Ajenda ni uchaguzi wa viongozi wa *TWPG.*

Kwa tangazo hili, Wabunge wote wanawake mnaombwa kuhudhuria na kushiriki bila kukosa.

Katibu.

**NDG. ZAINABU ISSA - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Mipango.

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/2027 - 2028/2029**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatia Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga ajiandae.

**MHE. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba tuna mijadala mitatu hapa, mpango wa mwaka mmoja, miaka mitano na miaka 25. Waziri wa Mipango alieleza kwa ufasaha mkubwa sana. Ujumbe mkubwa kutoka kwake ni kwamba ifikapo mwaka 2050, pato la Taifa *GDP* tunataka iwe ya dola trilioni moja. Mwaka huo huo tunataka pato la mtu mmoja mmoja *GDP per capita* iwe dola 7,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na yeye katoa hotuba ya ufasaha mzuri, ujumbe mkubwa kwetu sisi Watanzania anasema kwamba mwaka ujao wa fedha 2026/2027 uchumi utakuwa kwa asilimia sita nukta tatu na bajeti atakayotuletea hapa baadaye mwaka huu 2026 itakuwa karibu ni ya shilingi trilioni 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenda na *vision* ya 2050 ya dola trilioni moja na *GDP per capita* ya dola 7,000 inawezekana, hawajafanya makosa. Kwa niaba ya Wananchi wa Musoma Vijijini haya tunayoyajadili yote ni mazuri kwa sababu miradi yetu mikubwa, barabara, umwagiliaji imo kwenye mipango na Serikali inatafuta fedha. Kwa hiyo, Serikali inafanya vizuri na Mheshimiwa Rais anafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kuwasaidia kutoa mchango kwamba, makisio hayo yanahitaji uchumi ukue kwa kadri ya 10%, ukipungua sana asilimia nane, na sisi tupo asilimia

sita nukta tatu. Kwa hiyo, kazi yetu ya kwanza ya kufanya tufanikiwe hapa ni kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Mipango amesema, kwa takribani miaka 20 uchumi wetu umekuwa kwa asilimia sita, na ni kweli kwamba ukiangalia rekodi yetu ni mara moja tu tumenusa asilimia saba. Hata hivyo, wataalamu wa uchumi walivyoandika toka miaka ya 1980 wanasema, kama nchi maskini inataka kupunguza umaskini kwa kasi, ni lazima uchumi ukue kwa asilimia nane na sana sana 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili linawezekana. Kwa hiyo, Watanzania hatujafanya kosa, na mipango yetu siyo makosa, lakini twende kwenye uhalisia. Mfano wa mafanikio ni huu, China mwaka 1978 pato lake la Taifa lilikuwa karibu shilingi bilioni 150. Baadaye kama miaka 25 tuliyoiweka sisi, pato lake la Taifa likawa dola trilioni 1.7; lakini hayo mafanikio ya China ni kwamba uchumi ulikuwa kati ya asilimia tisa nukta moja na 10.1%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu mipango yote tunayoiongea, Mawaziri na Viongozi wote wakisimama kama uchumi haujavuka asilimia nane hatuwezi kufanikiwa. Hilo ndiyo la kwanza kabisa. Yote tutaongea, lakini chini ya asilimia nane hakuna mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la kwanza, ili uchumi ukuwe kwa kasi ya karibu 10% kwa mwaka, na pato la Taifa liongezeke, twende kwenye dola trilioni moja. Kuna sekta za uzalishaji ambazo zinapaswa kuchangia pato la Taifa, na mapendekezo yangu ni haya:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kilimo na bidhaa za kilimo ichangie 35% ya *GDP*; uchumi wa gesi *(natural gas)* labda baadaye tutapata na mafuta, uchangie 25%; madini bado sana, inapaswa ichangie 20%; utalii 15%; uvuvi na ufugaji asilimia tatu; michezo, muziki na utamaduni asilimia mbili. Tusipokwenda na hizo asilimia, haiwezekani tupate uchumi wa shilingi trilioni moja ndani ya miaka 25 ijayo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tena, Tanzania ni sehemu ya dunia. Humu mijadala yote tumejijadili sisi wenyewe. Majadiliano huwa hayaendi hivyo. Huwezi ukaweka mipango ya maendeleo unajijadili wewe mwenyewe. Ni lazima ulinganishe ndiyo utaona kwamba unafanya vizuri au unakwenda vizuri. Kwa hiyo, makisio ya uchumi wa dunia mwaka huu ni dola trilioni 124, ndiyo *GDP* ya dunia mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi tano bora, hizi nimezichukua, na baadaye mtaona umuhimu wake. Nchi ya kwanza ni Marekani ambayo ina uchumi wa shilingi trilioni 31.8. Nchi ya pili ni China 20.7, namba tatu Ujerumani yenye shilingi trilioni 5.3, ya nne India yenye shilingi trilioni 4.5; nchi ya tano ni Japan yenye shilingi trilioni 4.46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu hapa kuangalia, sisi watu wa Afrika tujifunze kutoka kwa China na India. Kwa mara ya kwanza toka mwaka 2025 India imekuwa namba nne duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimechukua hizi nchi mbili nikalinganisha na nchi za Kiafrika ikiwemo Tanzania. Kwanza tunaenda kwenye ubora, uchumi unavyokua. Nimeangalia karne ya 20 na karne ya 21. Karne ya 20 nimechukua mwaka 1960 *exchange rate* yaani dola moja ya Marekani mwaka 1960, dola moja ulikuwa unapata Yuan 2.6 za China, India zilikuwa Rupee 4.7, Kenya ilikuwa shilingi 7.14 na Tanzania haikuwepo, ila ilikuwa Tanganyika mwaka 1960, ilikuwa shilingi 7.3 kwa dola moja. *GDP per capita* mwaka huo wa 1960, China ilikuwa dola karibu 90, India 85, Kenya 103, Tanganyika ilikuwa dola 276. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunavyojadili hivi, Watanzania tuweke maanani kwamba tulishawahi kuwa juu kiuchumi kati ya China, India na Kenya mwaka 1960. Mwaka 1980 dola moja ya Marekani ilikuwa Yuan 1.5, *Rupee* 7.86, Kenya shilingi 7.03, Tanzania sasa, (1980 ilishakuwa Tanzania) dola moja ilikuwa shilingi 8.02. *GDP per capita* ya mwaka 1980, China ilikuwa dola 195, India 271, Kenya 435, Tanzania bado tulikuwa tunazidi hizo nchi kwa sababu *GDP per capita* yetu ilikuwa karibu dola 479. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuingia karne ya 21 nina takwimu nyingi nimechukua, mwaka 2025, exchange rate, Mchina na India wamebaki pale pale; China ilikuwa *Yuan* saba, India *Rupee* 90, *Kenyan shillings to a dollar* ilikuwa 130, *Tanzania exchange rate* yetu ilikuwa zaidi ya dola, shilingi 2,460. *GDP per capita*, China imetuacha. Iliyotushinda sasa ni dola 13,806, imekuwa huko tunapokwenda *upper middle*, India ni dola 2,900, Kenya dola 2,550, Tanzania dola 1,302. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa tunachojadili hapa, tunataka tutoke *GDP per Capita* ya dola 1,302 ndani ya miaka 25 twende dola 7,000. Haiwezekani kufika huko kama uchumi wetu hautakuwa kati ya asilimia nane na kumi, na hasa zaidi 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitoa ahadi ya kuwapa vyanzo vipya vya fedha. Naomba uniongezee dakika.

Mheshimiwa Kangi, umesema unanipa dakika zako eeh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kangi ananipa dakika zake hapa, kusudi niwapatie vyanzo vipya vya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka huo uchumi ukue, vya kwanza nimeshawapatia zile sekta sita zituchangie hizo fedha, kilimo, cha pili na ninashukuru Profesa alikitamka, ni lazima tuanzishe kitu kinaitwa *wealth funds* za *natural resources*. Yaani hapa *topic* ni (sijui Kiswahili chake unajua wengine sisi tunatoka Bara, Kiswahili kibaya lakini tuongee lugha inayojulikana duniani) *Natural Resources Wealth Funds. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, bila kupata hii, uchumi wetu hautafanikiwa. Ninashukuru Mheshimiwa Waziri wa Mipango ametaja, sasa *wealth fund* ya kwanza ni *Natural Gas Sovereign Wealth Fund* kama ya Norway. Norway walianzisha mwaka 1990, sasa hivi wana dola trilioni 2.2 na wakimgawia kila M-Norwegian anapaswa kupata dola 340,000, na *Sovereign Fund* ya Norway imenunua hisa kwenye *Stock Exchange* dunia nzima,

imechukua *1.5%* ya *equity* kwenye *Stock Exchange* za dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wewe ukienda Amazon kununua, unachangia Norway, ukiwa *Microsoft* unachangia Norway, wamenunua dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi mafuta yetu kwa kuwa tunaingia kwenye shughuli ya uchumi wa gesi hasa wa *LNG* ni lazima tuwe na *Sovereign Fund.* Ninashukuru Mheshimiwa Waziri aliitaja, na mfano ni kwamba sasa hivi tuna gesi kiwango cha 57.5 *TCF (Trillion Cubic Feet)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani miaka michache ijayo tukifanya *exploration* kule kwenye Ruvuma *Basin* huenda tutafika hata *trillion 100, a hundred trillion cubic feet.* Ni gesi nyingi na hiyo ndiyo itatufikisha huko kwenye uchumi wa trilioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, ni lazima tuanzishe *Mineral Wealth Fund*, hatuwezi kuwa tunafurahia tu dhahabu imechangia, lakini kama mlivyosema, dhahabu inaisha, vizazi vingine havitapata. Kwa hiyo, tutakuwa na *funds* mbili, za mafuta na gesi iwe na *fund* halafu tuwe na *fund* nyingine ya madini tu. Mfano ni kwamba, dhahabu Januari, 2020 bei yake, yule mchimbaji mdogo ilikuwa *ounce* moja ilikuwa dola 1,500, lakini Januari, 2026, *ounce* moja ni zaidi ya dola 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona sasa, kuna tofauti hapo, lakini sisi tunachukua mambo kama ya kawaida. Tulitakiwa hiyo faida tuweke *fund*, tuzifungie mahali fulani hizo fedha. Kwa hiyo, tutakuwa hii ya madini tutatumia dhahabu, na *Tanzanite*. Cha ajabu ni kwamba mwaka 2024, India ambayo haina *Tanzanite, export* yake duniani ilikuwa dola milioni 80 na Tanzania sisi wenye *Tanzanite export* yetu ilikuwa dola milioni 19.2. Kwa hiyo, tunampa Mhindi, anachonga, anasafirisha, sisi wenye *Tanzanite* tupo chini kabisa. Tutatumia *Tanzanite. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tatu, tutatumia *technology minerals*, yaani tuna *uranium*, tuna *graphite*, madini yote yanayotakiwa sasa hivi, tukichimba na kuyauza, tuweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, kwa upande wa madini ni hili. Gesi ya *Helium* ambayo kule Rukwa tumeshagundua tuna karibu *a 170 billion cubic feet of helium gas;* na *helium* ya kwetu ni nzuri kwa sababu ni *natural helium,* wakati nyingine zinatokana na mabaki ya *processing* ya mafuta na *gas*, kwa hiyo, haya madini na yenyewe yawe yana *fund. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya mwisho ya tatu ni *gold reserve*. Sasa sitaki kuiongea hii, mmeongea mengi, lakini ninashukuru tulipendekeza *gold reserve* ikaanzishwa. Tukitaka uchumi wa dola trilioni moja ni lazima tuwe na *reserve* ya dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya nne ya kuleta ni ndugu zetu wa *diaspora*. Tusile tu siasa, tu-*export;* na hapa ndiyo watu wanaodharau elimu, waliosema mkidharauliwa inabidi muwe wapole, lakini huwezi ukaikwepa elimu hata iweje. Kwa hiyo, mliosoma mkitukanwa, kuweni wapole tu. Hakuna mtu anayeweza kukwepa elimu kwa sababu hawa labour *export diaspora* wanaoleta fedha ni wale wasomi, wataalam wanaopata mshahara zaidi ya dola 10,000 kwa mwezi. Kwa hiyo, hapa nikiangalia *remittance,* kwa nini ninasema la wasomi, tuwekeze watoto wasomi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *remittance* watakaoleta fedha nchini mwaka 2025: India mwaka 2025 imevuna dola bilioni 135, China imevuna dola bilioni 50, Kenya imevuna dola bilioni tano, Tanzania tumepata milioni 800. Kwa hiyo, hiki nacho ni chanzo cha pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho ni ambayo msemaji mmoja Mbunge ninadhani ametaja vizuri. Ndugu zangu hakuna kusema kwamba Serikali isifanye biashara. Hayo ni mambo ya kizamani. Sasa hivi Uingereza imeanza kutaifisha hata reli zake. Kwa hiyo, China wanaendesha dunia, ni kwa sababu Serikali ya China inafanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu lazima tuwe na *state capitalism*. Ninakuja kumalizia ya mwisho lazima tuwe na *state capitalism*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja ya mwisho, ninamalizia moja tu hili. Moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwe na kampuni za Kitaifa ambazo zitaweza kuwekeza. Kwa mfano, migodi. Tuwe kabisa na kampuni zetu, huko kwenye *railways* na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na hili ni la muhimu sana, matumizi yetu ya umeme ya sasa hivi, Waheshimiwa wa Mipango, sijui tunasema tuna *Megawatts* ngapi? Mipango yetu kufika mwaka 2025 zilikuwa ziwe *Megawatt* 10,000. Haiwezekani twende na uchumi wa dola trilioni moja na umeme mdogo kiasi hiki. Mfano mzuri ni hapa, China na India na uzalishaji wetu wa umeme ni lazima tuzalishe kutoka kwenye jua, upepo na joto ardhi *(geothermal)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, sasa ninamalizia, hii ndiyo ya mwisho sasa, sitaki kusumbua. Ni kwamba *solar* ndugu zangu nimewapatia hii mwipate *solar power*. Tumesema China ndiyo ya pili duniani kwa Uchumi. Angalia umeme unaozalishwa kutoka kwenye jua, umeme jua *(solar),* wana *Gigawatt* 1,200. Maana yake ni *Megawatt* 1,200,000 za *solar*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, India ambayo ni ya nne duniani kiuchumi, umeme jua *(solar energy)* wana *Gigawatt* 136. Inamaanisha *136,000 megawatts*. Tukichukua umeme, China ni ya pili duniani kiuchumi. Umeme wa upepo una *gigawatt* 640. inamaanisha *megawatt* 640,000. india ina *gigawatt* 55, inamaanisha *megawatt* 55,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie kwa kusema mipango tuliyoiweka inawezekana, uchumi ukue kwa takribani 10% na tuwe na umeme mwingi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Sana Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo ametumia nafasi ya Mbunge mwenzake, ambaye alimpa muda wake. Kwa hiyo, msione ameongea sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, na Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuweza kunipatia fursa ya kuweza kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka 25, Miaka Mitano, Mwaka Mmoja na ule Mpango wa Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, kwanza kabisa kwa masikitiko nipende kutoa pole kufuatia kifo cha diwani wetu wa Kata ya Ketare Ndugu Philipo Marwa Gikaro ambaye alikuwa anatoka kwenye Baraza la Madiwani akielekea kwenye Kata yake ya Ketare, lakini akapata ajali kwenye ile barabara ambayo ninaizungumzia ya *keep left* Mogabiri ambayo kwa kweli inapoteza nguvu kazi ya Taifa, na inalemaza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iipe kipaumbele kama jambo la dharura, itupelekee fedha, shilingi bilioni nane tu kuweza kuokoa maisha ya wananchi wa Tarime. Pia, ile barabara ndiyo Uchumi. Watu wanatoka Nairobi (watalii) kwenda Mugumu, wanapita pale, wanaenda Nyamongo wanapita pale, sisi wenyewe Tarime Mji, pale ndiyo Makao Makuu ya Wilaya, ndiyo barabara, ni finyu na imeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde, ninaomba muweze kutoa kipaumbele kwenye ile barabara ya *keep left* Mogabiri kuweza kuokoa maisha ya Wanatarime na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee sasa kuweza kuchangia Mpango. Nitajielekeza kwenye nishati, ukuaji wa uchumi na pato la mtu mmoja, na pia nitaenda kuchangia *point* mbili kama muda utanitosha. Nimejaribu kumwuliza hapa Mheshimiwa Sanga naye anipe muda, amesema ameshachangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye nishati Mpango wa muda mrefu umeonesha na ninapongeza ripoti ambayo imekuwa *tabled* na Wizara na ripoti ya Kamati yetu ya Bajeti ambayo imefanya uchambuzi wa kina kabisa kwa maslahi ya Taifa letu. Kwenye Mpango wa muda mrefu imeainisha kwamba Serikali *ina-target* kuhakikisha kwamba inazalisha *Megawatt* 70,000 ifikapo 2050/2051 kutoka *Megawatt* ambazo tunazalisha sasa hivi za 4,032.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, imeainisha kwamba matumizi ya mtu mmoja yatatoka *Kilowatt* 108 mpaka *Kilowatt* 3,000 kwa mwaka kwa jinsi ilivyo sasa hivi. Vyanzo vya uzalishaji wa umeme huu wameainisha kwamba ni jua, maji, joto ardhi, makaa ya mawe, upepo, pamoja na gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia hivi vyanzo ni vizuri na lengo ni zuri, lakini ukifuatilia utaona kwamba hii miradi ambayo tumeainisha hapa inatumia muda mrefu sana kuweza kutekelezwa na Serikali. Kwa mfano, chanzo cha maji ambacho kimeainishwa, cha Luhiji na Lubakali, walishafanya upembuzi yakinifu hapo mwaka 2022. Baadaye wakawaacha tena, wakaja, sasa hivi wanafanya uhuishaji wa upembuzi yakinifu ambao unatumia zaidi ya shilingi 3,000,200,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchuchuma na Liganga tumeongea kwa muda mrefu sana ambapo ingewekwa kwenye utekelezaji, ingeweza kuchangia kwenye *energy mix,* na upepo wa Singida. Pia, tuna joto ardhi kule Mbeya bado hivyo vyote havijaweza kuwekwa. Sasa ili Serikali *on average,* kwa jinsi ilivyojiwekea ni kama vile inakuwa inazalisha ongezeko la *Megawatt* 2,639 kwa mwaka kuweza kufikia *target* ya *Megawatt* 70,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kufanya haya yote, mimi nilikuwa nashauri tuweze kuhakikisha tunashirikisha sekta binafsi, kwa uhalisia kwa kuona kwamba, sasa hivi chini ya Serikali mambo haya-*move* kihivyo. Tushirikishe sekta binafsi, nayo iweze kuingia kwenye uzalishaji wa umeme tukizingatia kwamba nishati ni kichocheo cha sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tukiwa na nishati ambayo ni toshelevu, tunaenda kuongeza mnyororo wa thamani kwa sekta nyingine kama viwanda, biashara, madini, utalii, *whatever you name it.* Yaani tukiwa na umeme ambao ni toshelevu, tunaenda kuinua uchumi kwa asilimia kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukichukua mfano wa nchi ya China, amesema hapa ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Muhongo, wenzetu wale waliweka malengo ya kuhakikisha kwamba wanatumia *energy mix* kwa asilimia nyingi na wakaziambatanisha na sera yao ambayo kwao nishati ni uti wa mgongo wa viwanda. Pia, sera ya nishati waliiunganisha na sera ya ajira, viwanda na mauzo ya nje na wakahakikisha wakajiwekea *target* ya kuzalisha *Megawatt* kadhaa katika kila mwongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza hapa, wanazalisha *Megawatt* 2,800,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, ni moja kati ya nchi ambayo ina umeme toshelevu. Ni Dhahiri, sisi tunategemea bidhaa nyingi sana kutoka China kuja kwenye soko letu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba tukiboresha sekta hii ya umeme, tunaenda kuhakikisha kwamba tunakuza uchumi na kufikia malengo ambayo tumeyaweka ya kuhakikisha kwamba uchumi wetu wa Taifa unakua kati ya 10% mpaka 12%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nishauri kidogo katika hayo ambayo nimeyasema, ili tuweze kusonga vizuri, tukaribishe hiyo sekta binafsi, lakini tuhakikishe pia tunatenganisha katika uzalishaji, usambazaji na uunganishaji, ili kuhakikisha kwamba kama ni sekta

binafsi, tunai-*chop*, inaenda kwenye sekta fulani ili kuweza kuboresha ufanisi na kuleta ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tukizingatia Tanzania, tunaenda kujiunga na *hub* ya umeme kwa nchi za *SADC* tuweze kuweka bei ya ushindani. Kama tutafikia huko tukazalisha umeme ambao ni *extra, tuweke* bei shindani ili tuweze kuziuzia na nchi ambazo zitakuwa zinauhitaji wa umeme na kwa kufanya hivyo tunaweza tukakuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye pato la mtu mmoja la ukuaji wa uchumi. Kwenye Mpango wameainisha kwamba *target* sasa ni kuhakikisha kwamba kufikia 2050/2051 kwa maana ya miaka 25, Tanzania inakuwa na pato la mtu mmoja dola 7,000 kutoka ya sasa hivi ambayo ni dola 1,275. Ni malengo mazuri na yana matamanio mazuri na *indicator* nzuri ya kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakua na wananchi wanaweza kuwa na pato ambalo ni la uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbukuka mwaka 2019 tuliweza kukuza pato letu mpaka 1,080 tukawa kwenye uchumi wa chini wa kati. Hebu turejee huu Mpango ambao tunamalizia wa miaka 25, tuliweka *target* ya kukua kwa pato la mtu mmoja *on average* kama dola 3,000, kwa maana waliweka *range* kutoka 1,416 mpaka 4,515.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2000 kipato cha mtu mmoja ilikuwa dola 756, lakini kwa miaka yote 25 tumeweza kufika tu dola 1,275 kwa maana ongezeko la 516 tu kwa miaka yote 25. Sasa lazima tukae tuangalie hii ya dola 7,000 ili iweze kuwa *realistic,* tunatakiwa tuje na mipango ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *gap* kutoka 1,275 kwa dola 7,000 ni *gap* kubwa sana. Mbaya zaidi katika mpango wakati ninasoma, katika utekelezaji wa miaka mitano (2026/2027 - 2030/2031) tunaonesha tutaenda kuongeza pato la mtu mmoja kwa dola 363 tu, kwa maana kutokea sasa 1,275 hadi 1,638.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunaweka *projection* ya kuongeza ndani ya miaka mitano 363 tu, maana yake ukifanya *on average* jumla ya *assumption,* tunatarajia kuongeza miaka 20 iliyobaki dola 1,452 kwa ujumla wake, inakuja kama dola elfu mbili na kitu hivi au 3,090. Kwa hiyo, kwa miaka yote ukifanya *on assumption* ni 3,000 mpaka 4,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kufanikisha hili, kitu kingine *projection* ya ukuaji wa uchumi tu, ni kati ya 10% mpaka 12% lakini sasa hivi *as I speak* ni kati ya hiyo asilimia tano nukta tano mpaka sita. Kwa mwaka huu 2026 inaweza kwenda kuwa asilimia tano nukta tisa. Kwa mwakani imewekwa *projection* ya six *point three on average*. Ili tuweze kufikia hii *target,* lazima kila mwaka tuhakikishe tunakua kwa uchumi wa 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafikiaje hapa? Moja, (ni vema mmeainisha) Mpango uende kugharamiwa *(sponsored)* kwa asilimia kubwa na *private sector* 70% na 30% Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kusema tuki-*involve private sector,* kwa mfano, kutoka *Singapore,* ukiiga tu mfano hapo, wao uchumi wao kwa asilimia kubwa unachangiwa na *private sector* kati ya 80% mpaka 90% ambao wamewekeza kwenye viwanda. Wamewekeza kwenye biashara, wamewekeza kwenye teknolojia, na pia nao waliweza kufungamanisha hivyo hivyo sera zao kuhakikisha uchumi wao unakua kwa kuwawezesha hawa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ukiangalia kwenye nchi za ukanda wetu wa Afrika Mashariki na *SADC (South Africa* na Rwanda); Rwanda wao wana-*range* kati ya 60% na 70% *of which* na sisi tumeweka vizuri. Tukiwezesha *private sector* zika-*take off* kwa hiyo 70% kuweza kugharamia Mpango, tutajikuta walau tunafikia malengo ambayo tumeyaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili hili liweze kufanikiwa lazima pia tubadilishe utaratibu wa utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo. Pia na maamuzi ambayo tunayafanya kwenye uchumi wetu, lazima tubadilishe mitazamo ya kimaamuzi ambayo

tunayafanya kwenye uchumi wetu, kwa maana kwenye vitu ambavyo vinaenda *ku-drive* uchumi wetu, bila kufanya hivyo hatuwezi kufikia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie, ninaona kengele imelia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima pia kuwepo na *the regional potential assessment,* yaani kila mkoa tu-*assess* kwamba mkoa A kwa mfano, Mkoa wa Mara, una fursa gani ambazo tukiziwekeza zitaenda kuchagiza zaidi kwenye uchumi? Kule Mara tuna madini, kilimo tuna ardhi ambayo ina rutuba nzuri, kilimo kita *take-off* vizuri, tutafuga, tutavua, na pia utalii, *partly*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Arusha *the more* ipo kwenye utalii, ukienda Dar es Salaam biashara labda na usafirisha *and the like of.* Tuki-*categorize* hizi zote tukajua *potentials* za kila mkoa na tukaenda kuwekeza kulingana na u-*potentiality,* hakika tutaweza kusaidia kuhakikisha kwamba tunafika mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kingine ambacho ninapenda kumalizia ni kuhusu sekta ya utalii. Hii ni sekta ambayo tungewekeza kwa kiwango kikubwa zaidi. Kwanza kabisa tuki-*take on board* kwamba Mwenyezi Mungu ametubariki, tuna vyanzo vya asili vingi vya kitalii, lakini ukweli wa Mungu hatujavi-*exhaust.* Ukiacha juhudi ambazo Mheshimiwa Rais anafanya na matangazo *and the like,* zile ambazo ni *natural* tu *attraction* hatujazi-*exhaust.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukitembelea Mataifa mbalimbali utakuta hata wale ambao hawana *natural attractions,* lakini wametengeneza *artificial attractions* nyingi ambazo zina-*generate income* kwa Taifa husika. Yaani tuna vivutio vya kiasili, leo nitakuja mimi nitatembelea, nitaona fisi, nitaona simba, nitaona nini kule Serengeti, nitaenda kwa Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo kwa Baba wa Taifa nako paboreshwe. Tukienda *South Africa,* kwa Mandela kule wanachukua fedha nyingi sana. Kwa Baba wa Taifa ni baba ambaye anafahamika duniani, pale pia ni kivutio cha utalii cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukifanya hivyo, zile za *natural,* kuweka hivi vingine vya michezo, weka utalii wa matibabu, weka na *artificial.* Tu-*create* kwa mfano, hapa Dodoma ni Makao Makuu, si mnaweza mkaweka vi-*artificial attraction* hapa ili watu wakifika wanakuja wanatembelea na wanaingiza fedha; hiyo itaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa sana ku-*create* ajira na kuongeza mapato, na fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko. Nilimtaja Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka ajiandae.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa wasaa na mimi niweze kuchangia katika Mpango wa miaka 25, miaka mitano, na mwaka mmoja kama ulivyowasilishwa vyema kabisa na Waziri wetu wa Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Prof. *Comrade* Kitila Mkumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ni-*declare* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, na pia michango yangu itajikita katika vitu vitatu. Kwanza, nitachangia kwenye upande wa *informal sector,* halafu pili nitachangia uwekezaji wa viwanda na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukianza kuangalia tathmini ya utekelezaji wa Dira yetu ya muda mrefu, kuna changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zinaainishwa zinazosababisha watu kutokuwa na imani na utekelezaji wa Mpango wa miaka 25, miaka mitano kwenda mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasoma kidogo hapa; moja, kwa sababu ya uzalishaji mdogo wa kilimo. Kilimo chetu kimekuwa siyo kilimo biashara na ukiangalia kuna mchangiaji mmoja alichangia juzi hapa akawa ametoa mfano wa ile *project* ya *BBT* namna ambavyo iliweza kutumia rasilimali nyingi za Serikali, lakini pia haikuweza kuwa na tija katika Taifa letu. Sasa vitu kama vile haviashirii haya malengo ambayo tunayazungumza kama ambavyo tumekuwa tukiyapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ukuaji wa sekta ya uzalishaji wa viwanda, ninaomba nizungumze kidogo hapo. Viwanda ndiyo mkongo wa uchumi katika Taifa lolote duniani. Mimi ni Mbunge wa Kigamboni. Kigamboni sasa hivi tunavyozungumza, kama nilivyozungumza kwamba ina takribani viwanda 342: viwanda vikubwa vikiwa 42 na viwanda vidogo vikiwa 298. Hata hivyo, ukianza kuangalia vichochezi vya vile viwanda ni ile barabara moja tu iliyojengewa kutoka Kibada – Mwasonga - *Tundwi Songani Junction* kwenda Kimbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu amefanya kazi ambayo imeenda kutengeneza ile *line* inayoitwa sasa hivi *industrial corridor*. Hivi sasa tunavyozungumza kuna Wachina wanakuja kuwekeza viwanda 50, ambavyo vitasaidia pato la Taifa, lakini pia itasaidia kuongeza ajira, pia itasaidia hata halmashauri zetu kuweza kupata mapato ya *Service Levy*. Kwa hiyo, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme kwamba, Serikali tunavyokuwa kwenye hii mipango ambayo inatakiwa kuleta uchumi chochezi katika Taifa letu, lazima tuangalie *infrastructure* zinazosogeza au zinazoendesha uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi hapa leo ukiniambia Kigamboni kama sehemu yangu ya jimbo, ninahitaji kupata barabara ya kutoka Mji Mwema - Somangila - Kimbiji mpaka Pemba Mnazi. Hii barabara ni muhimu sana katika uchumi wa Kigamboni na uchumi wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Pemba Mnazi sasa hivi tunavyoongea eneo kubwa limewekezwa maeneo ya viwanda tu, siyo makazi ya watu. Kwa sasa ni msitu kwa sababu, hakuna miundombinu wezeshi ya kuwapeleka wawekezaji waweze kujenga kule na kuhakikisha uchumi unakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka kuchangia ni eneo la teknolojia na mifumo. Nilikuwa ninapitia Ripoti ya *CAG*, *Performance Audit on the Systems* ambazo zipo kwenye Serikali. Serikali yetu imekuwa na mifumo mingi sana ambayo haina tija, kila siku Mheshimiwa Rais toka mimi ninamfahamu anaongea kwamba, lazima wataalam wahakikishe mifumo inasomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifumo haisomani kwa sababu ya maslahi binafsi ya watu ambao wanaweka katika *projects* hizi, kitu ambacho kinasababisha upotevu wa mapato, na pia, kutokuwa na *efficiency* katika utekelezaji wa hii mifumo. Serikali hivi tunavyozungumza kila taasisi ina mfumo, lakini ukiuliza hii mifumo inasomana? Inaweza ku-*fetch information* kwenye *system* nyingine? Huwezi kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano, leo tunavyozungumza hospitali zetu za rufaa zina mfumo wake binafsi, lakini pia, hospitali za wilaya zina mifumo yake. Sasa unaanza kuuliza kwa nini hospitali za wilaya zina mifumo inayojitegemea na hospitali za mikoa zina mifumo inayojitegemea? Kwa nini, wataalamu hawa wasikae pamoja wakatengeneza kitu ambacho kinachoweza kuwa na njia moja ikamsaidia hata mwananchi anayeumwa kule Pemba Mnazi, Kimbiji au kule Makete aweze kufika katika Hospitali ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ripoti inasikitisha, kwa maana wameainisha mifumo ambayo haifanyi kazi. Ukiangalia masuuli yaliyotumika kununua ule mfumo ni hela nyingi sana katika Serikali. Ninaomba Waziri anayehusika na mambo ya teknolojia aitishe kikao cha wakuu wote wa taasisi wanaosimamia mifumo *(ICT's)* wakae, waje watupatie Mkongo wa Serikali wa Mfumo,

uwe ni mmoja na sisi tuweze kuweka mifumo tegemezi, ambayo inakuwa *integrated* kwenye ule mfumo, kama ambavyo benki zinavyofanya. Benki zina mfumo mmoja unaitwa *Co-Banking System (CBS)*, mfumo ule ndiyo unaoendesha *operation* zote za benki, lakini bado unaweza ukakuta kuna *application systems* ambazo zinaongea na ule mfumo mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itatusaidia nini? Kwanza itatusaidia katika hatua ya kuwa na *data* kamili kama Serikali. Pili, mfumo ule utatusaidia katika kutengeneza mipango, kama tunavyosema sasa hivi, tutakuwa na uwezo wa kupanga vizuri na kuhakikisha Watanzania wote wanajulikana kwa kutumia hii mifumo ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukianza kuangalia *data* ambazo zinatumika sasa hivi, unaweza kukuta ni za *NBS,* lakini unaweza kukuta labda kuna *data* nyingine ambazo, yaani Wizara ya Fedha ina *data* nyingine na *NBS* wana *data* nyingine. Sasa unaweza kuangalia tofauti hii inatokana na nini? Ni kwa sababu ya kutokuwa na mifumo ambayo inaweza kuongea kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitoe tu rai. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Prof. Muhongo hapa alipotoa mapendekezo yake kwamba, wakati umefika wa Serikali kuhakikisha inawekeza kikamilifu katika sekta ambazo zinazalisha na zinaongeza tija katika pato letu la Serikali. Ametoa mfano hapa kwamba, hiki kilimo tunachokizungumzia, basi Waziri mwenye dhamana ya kilimo aende ajielekeze kutafuta wakulima wanaofanya kazi wawezeshwe kulima kilimo biashara, tuwafuate kwenye mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ninaomba nizungumzie habari ya utalii. Disemba nilienda Dubai nikakuta kule kuna *ocean made* ambayo Watanzania na watu kutoka duniani wanaenda kutalii kwenye lile ziwa ambalo limetengenezwa. Ule utalii ambao umekuwepo pale watu wanatengeneza *boat dinner;* unaenda kwenye *boat,* unaingia mle ndani, unalipia dola 350. Sasa ukianza kuangalia *rate* ya watu walioko pale ni karibu *millions of people,* wanalipa hiyo dola 350. Ukifanya *collection* unaweza ukakuta ni shilingi ngapi ambayo ile Serikali inachukua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Dodoma, kama mwenzangu alivyokuwa anazungumza hapa, inahitaji twende shule kutengeneza Ziwa Dodoma tuwe tukitoka huku Bungeni jioni twende tukapate kidogo hewa ya maji ya Bahari. Inahitaji kuingia darasani?

Mheshimiwa Mwenyekkiti, haihitaji kuingia darasani. *The artificial man-made tourist* ndiyo tunatakiwa sasa tuweze ku-*focus,* ili kuhakikisha tunaleta mvuto katika Jiji letu la Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na mimi pia, nitumie nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu kwa mipango iliyowasilishwa hapa Bungeni. Nawapongeza sana Mawaziri wetu wawili ambao wamewasilisha mipango yetu mitatu, Waziri Kitila na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuutazama mpango ambao umewasilishwa hapa, ni dhahiri kabisa ni mpango uliojielekeza kuibadilisha Tanzania, iwe Tanzania ya uchumi. Katika maeneo yote mahsusi, ambayo yameainishwa kwenye mipango yetu mitatu yote, kama itatekelezwa na kusimamiwa ipasavyo, basi tutakwenda kuwa na Tanzania iliyochanua, yenye uchumi unaojitegemea na watu walioimarika kimapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nianze kuutazama mpango wetu kwenye eneo la kilimo. Kama kuna jambo kubwa katika mipango iliyopita lilifanywa kwa uthabiti na kwa nguvu kubwa ni kuhakikisha sekta ya kilimo inakuwa ya uzalishaji na kujenga uchumi wa wakulima, hasa mkulima mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita, tulijielekeza katika kuhakikisha kwamba, wakulima wote nchini wanapata ruzuku za pembejeo, ili kukuza uzalishaji wa kutosha na kupata masoko ya uhakika. Nimefurahi kuona kwenye mpango kwamba, tumekusudia kufikia 45% ya wakulima wote nchini wawe wanapata ruzuku. Kwa nini tunatoa ruzuku kwa wakulima wetu? Lengo ni kupata uzalishaji mkubwa na kuongeza mapato ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri jambo. Wakati tunapoelekea kutekeleza mpango wa kukuza maeneo ya uzalishaji, ni lazima tukubali kuoanisha na kuziunganisha sekta zetu zifanye kazi kwa pamoja. Kwa mfano, leo hii huwezi kuzungumzia Sekta ya Kilimo ukaacha kuiunganisha na Sekta ya Barabara kwa sababu, ili mkulima aweze kuzalisha, ni lazima apeleke mazao yake sokoni; na ili apeleke mazao yake sokoni ni lazima awe na barabara za uhakika zinazopitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatokea Jimbo la Nachingwea. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2024/2025 wakulima wa korosho walizalisha tani 31,000 na kuweka mfukoni fedha zaidi ya shilingi bilioni 72. Jambo hili limewezekana kwa sababu, Serikali ilitoa ruzuku na pembejeo bure kwa wakati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2025/2026 wakulima wa korosho wa Nachingwea wamezalisha tani 41,000 na wameingiza fedha zaidi ya shilingi bilioni 100. Ukitazama hii fedha ambayo imezalishwa katika kipindi cha misimu miwili, ni matokeo ya utekelezaji wa mipango ya Serikali na juhudi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha kwamba, wakulima wanapata tija. Kwa bahati nzuri tu, sekta hii ya kilimo imekuwa inaweka msukumo mkubwa sana, ili kila mkulima aweze kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata changamoto kubwa sana tunapotekeleza mpango wa maendeleo katika eneo la miundombinu ya usafirishaji, hususan barabara za wilaya moja

kwenda nyingine na kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nachingwea ina barabara inayobeba korosho nilizozitaja hapa kwa tani kutoka Nachingwea – Masasi. Barabara hii ina kilometa 45, na ndiyo barabara inayotumika kuunganisha mfumo wa maghala na usafirishaji wa kwenda Bandari ya Mtwara na Dar es Salaam. Barabara hii haipitiki na inawezekana kama isingekuwa msimu wa safari hii umechelewa kupata mvua, basi barabara hii tungeweza kupata shoti kubwa ya korosho kubaki kwa sababu ya kukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nilikuwa ninasikiliza majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faraji wa Ndanda, anasema, Barabara ya Nachingwea – Liwale kutokea Masasi ni barabara ambayo ipo kwenye Mpango na tayari wameshaweka utaratibu wa kuanza ujenzi wake kutoka Liwale – Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimetaja hii hoja ya Mheshimiwa Waziri? Ni kwa sababu tunapotekeleza mpango wowote wa maendeleo lazima tuwe na kipaumbele cha kuona tija ya wananchi ni nini katika mradi unaotekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la barabara, Wilaya ya Nachingwea tija ya barabara iko kutoka Nachingwea – Masasi, siyo kwamba hakuna umuhimu wa kutoka Nachingwea – Liwale, hapana. Liwale tija yao pia ni kutoka Liwale kwenda Nangurukuru kutokea Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mkandarasi anapoanza kutoka Liwale kuja Nachingwea ni sawa, na ni moja ya kipaumbele, lakini tija ya uzalishaji na kujenga uchumi kupitia usafirishaji inakuwa inachelewa kwa sababu, uchumi wa Barabara ya Nachingwea unajengwa kuanzia Nachingwea penyewe kwenda Masasi, na uchumi wa Liwale unajengwa kwa kuanzia Liwale kwenda Nangurukuru kutokea Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maoni yangu? Kama kulikuwa na mpango unaotekelezwa, na katika kutekeleza mipango hii ya ujenzi wa Barabara ya Nachingwea – Masasi – Liwale – Nangurukuru na tukaamua kuchagua kuanzia Liwale – Nachingwea, ninaomba sana kwa unyenyekevu mkubwa, kama kipo kipengele kinachoweza kubatilisha (kughairisha) utaratibu Barabara ya Nachingwea – Liwale ina kilometa 122, ukizigawanya hapa mimi ninaweza kumwachia Liwale hata kilometa 70 zote ziwe zake. Nipeni kilometa 45 za Nachingwea – Masasi ili mazao ya korosho, ufuta na mengine yaweze kusafiri, uchumi wa Taifa letu uweze kukua na tuchangie pato la Taifa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliweka wazi, Wananachingwea, kwa kadiri tunavyojua kwamba, Serikali ina maeneo mengi ya kutekeleza miradi ya barabara, ili kukuza uchumi, sisi tunapokea hata kwa awamu. Alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifanya kazi nzuri pale Nachingwea, nikamwambia hata wakitupatia kilometa 20 kuanzia Nachingwea – Masasi bado itakuwa imetumesaidia usafirishaji wa mazao na kuwawezesha wananchi wetu kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nijielekeze kwenye eneo hili la kilimo ambalo litatusaidia kama tutaunganisha sekta zetu ziweze kufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nizungumzie sekta ya usafirishaji katika eneo la bodaboda. Nchi yetu inalitambua kundi la waendesha pikipiki, maarufu kama bodaboda, lakini mpaka sasa tunaendelea kutengeneza jitihada ya kulitambua, kama rasilimali na chanzo cha mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninamzungumzia bodaboda, ambaye ukimwita ukakaa naye, ukimwuliza una nini? Atakwambia nina nyumba ya vyumba vitatu. Ninamlea mama na baba yangu, nina wadogo zangu wanasoma. Leo ninazungumzia bodaboda ambaye ukimwuliza una nini mkononi? Atakwambia nina *Degree* ya Ualimu, nina *Degree* ya Uchumi. Tayari amemiliki pikipiki mbili au zaidi ya biashara nyingine. Tumekuwa na juhudi kubwa za kuwafanya wawe rasmi, lakini bado tumekuwa na

uoga wa kuwasogeza kama sekta inayotambulika, kama makundi mengine ya wajasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina makundi ya wachimbaji, wafugaji na wakulima. Hizi sekta zote katika mpango zimetambuliwa kwamba ni sekta ambazo zinaweza kuchangia uchumi wa Taifa. Ninataka nikwambie mbele ya Bunge lako Tukufu, bodaboda ni chanzo kimojawapo cha kuongeza mapato ya nchi hii.

Mheshimiwa mwenyekiti, bodaboda wanakadiriwa kuwa zaidi ya 3,000,000 na ninamshukuru sana Waziri wa Vijana, Mheshimiwa Nanauka, amefanya kazi kubwa ya kukutana na vijana, Mama Lishe hasa wale wanaoendesha pikipiki na akamwalika Waziri Mkuu katika mkutano ule. Moja ya jambo lililojadiliwa pale, ni uwepo wa masharti magumu sana ya kuendesha shughuli hii. Tunaichukua kama shughuli ya dharura ya usafiri, lakini siyo sehemu ya kutengeneza uchumi wa Taifa letu. Sasa basi, mimi nina mapendekezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, sambamba na kutambua bodaboda sasa hivi siyo wa kuwawekea hofu kabisa, tayari wameanza utaratibu mzuri wa kujisajili. Wakijisajili kwa namba na idadi yao, tukiwapunguzia baadhi ya masharti, tutaweza kupata fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuanze kwenye eneo la leseni. Kwa sasa Serikali inataka dereva mmoja wa bodaboda apate leseni kwa shilingi 70,000/=, lakini tuna bodaboda 3,000,000. Mpaka leo ninapozungumza 20% tu au chini ya hapo ndio walioweza kwenda na kuchukua leseni zao kwa fedha ya shilingi 70,000/=. Kwa nini tusipunguze tukakusanya kidogo kwa watu wengi na tukawawezesha bodaboda wengi kuwa rasmi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweke kiwango cha shilingi 30,000/= kwa kila bodaboda, ili aweze kupata leseni ambayo itasaidia kila kijiji, kata, wilaya na maeneo yote mikoani kuwa na bodaboda wenye leseni wanaoweza kutambulika kwa usajili

waliojiwekea. Pale Ilala wameanzisha utaratibu mzuri sana wa *dashboard* maalum ambayo kila bodaboda anajisajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiachilia mbali masuala ya kiusalama, ambayo tunayaweka katika uendeshaji wa shughuli zao na usalama wa barabarani, lazima tuwawekee mazingira ya kuwatambua kwa shughuli wanazozifanya kwa kuwawekea utaratibu zaidi, ukiacha masuala ya ufuatiliaji wa Sheria za Barabarani ambazo wanazivunja kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunaweza kuamua katika miezi mitatu kwa mwaka tukaweka siku moja au tano za ukaguzi wa masuala ya uendeshaji wa bodaboda barabarani. Tutumie siku hizo kukagua yale yote yanayohusu wao, kama ni leseni au ni utaratibu wa usajili wao, ili kuwawezesha bodaboda hawa kufanya kazi kwa utulivu kuliko kila siku kuendelea kuwakagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nichangie maeneo hayo mawili. Ninakushukuru sana, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fadhili Liwaka. Nilimtaja Mheshimiwa Asia Halamga na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja, Mitano na 25 katika maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwepo humu ndani. Pia, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama katika nchi yetu, pamoja na vikao vyote vya maamuzi vilivyonipitisha kuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi na leo nipo humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Wana-CCM wote wa Wilaya ya Hanang'. Kubwa zaidi, kwa wananchi wa kata zote 33 na vijiji vyote 96 kwa kutoa kura za kishindo kuanzia kwa Rais, mimi Mbunge, pamoja na Madiwani wote wa Chama Cha Mapinduzi kwa kura za kishindo na za kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu imani kubwa ya Wanahanang' kwa kutoa kura kwa Chama Cha Mapinduzi ni kwa sababu, kipindi cha miaka minne Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa ya maendeleo, ndiyo maana Wanahanang' hawakuwa na hofu wala shaka ya kuhakikisha wanamchagua kwa kura zote za kishindo na kuwachagua viongozi wote wanaotokana na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani zangu hizo, ninaomba sasa nijielekeze kwenye Mpango. Wakati ninajielekeza kwenye Mpango, ninatumia nafasi hii kuwapongeza sana Mawaziri kwa kazi kubwa ambazo wanafanya wakiongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite katika uingizaji wa bidhaa kwenye nchi yetu, hususan bidhaa tano muhimu, mojawapo ikiwa ni ngano inayoingizwa katika nchi yetu. Tunatumia fedha nyingi za kigeni kuingiza ngano ndani ya nchi yetu. Uhitaji wa ngano ni zaidi ya tani 100,000 tunazoziagiza nje, lakini ndani tuna uwezo wa kuzalisha tani 120,000. Hivyo, 85% mpaka 95% ya ngano ya nchi yetu ya Tanzania tunaagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia fedha za kigeni zaidi ya milioni 350 mpaka milioni 450, hii ni sawa na shilingi trilioni moja ambapo ni fedha tunazitumia kwa ajili ya uingizaji wa ngano hapa nchini. Ninaomba kutumia nafasi hii kuipongeza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kujikita katika kubadili historia na kuhakikisha tunapunguza kwa kiasi kikubwa kuagiza ngano katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee mashamba makubwa ya kihistoria katika nchi yetu. Mashamba ya ngano ya Basutu yaliyopo Wilaya ya Hanang' ambayo yalianza toka mwaka 1970, kwa sasa yana mwekezaji ambaye anaitwa *Ngano Limited*. Mwekezaji ana shamba takribani ekari 43,000 na muda ambao amepewa sasa ni miaka 20. Huku Taifa likitumia gharama kubwa kuagiza ngano nje ya nchi. Shamba ambalo lilikusudiwa kulimwa ngano kwa miaka 20, shamba hilo limekuwa ni pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaiomba sana Serikali kutoka na kwenda kuliangalia Shamba la Basutu *Plantation* ili kuweza kupitia mkataba wa mwekezaji na makubaliano tuliyompa shamba lile kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo cha ngano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 1970, walikuwepo Wakanada, Hanang' ilikuwa ni sehemu ya historia katika nchi, uwanja wa ndege upo na ndege zilikuwa zinashuka kwa sababu ya ngano, ambacho ni kilimo kikubwa kilichopo pale. Leo Taifa linapoingia hasara ya kwenda kuchukua ngano nje ya nchi wakati tayari tulikuwa tunao mwendelezo mzuri wa shamba na lilikuwa linazalisha, siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuiomba Serikali yangu sikivu irudi kupitia upya shamba la mwekezaji la Ngano *Limited* kwa sababu halimi, hazalishi, na mwisho anatutengenezea changamoto kati ya viongozi, wananchi na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamezaliana, wanaliona shamba liko pale, shamba limekuwa pori na linakodishwa kwa mtu yeyote ambaye mwekezaji anajisikia na wananchi wanabakia wakiangalia. Hii haikubaliki. Ninaiomba tena Serikali yangu sikivu ipitie upya mkataba wa Shamba la Basutu. Tukiweza kuchukua shamba la Basutu tutaweza kuiokoa

nchi yetu kwa 26% ya kutokuagiza ngano nje ya nchi ambayo tunatumia fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kupongeza sana Wizara hii kwa mipango endelevu hususan viwanda. Tunaona namna Serikali ambavyo imejipanga kuuendeleza Mji wa Dodoma, pia kuendeleza Mkoa wa Arusha kwa kupelekwa fursa nyingi pamoja na Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa maendeleo endelevu ili kuondoa foleni mbalimbali na kuubana mji huu tena wa Dodoma, ushauri wangu ni kwamba, Mkoa wa Manyara ni mkubwa. Ni Mkoa ambao bado una ardhi kubwa. Ninaomba sana suala la viwanda tuweke Mkoa wa Manyara kama eneo la kimkakati na hususani Wilaya ya Hanang' ili kwa miaka kadhaa huko mbele tuondoe foleni na *jam* kubwa ya kuwekwa viwanda hapa na kutanua fursa za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongelea viwanda kuwepo Mkoa wa Manyara, maana yake ni kuwa, tunayo fursa ya kupeleka bidhaa nchi jirani kama Nairobi - Kenya, kutoa bidhaa kupeleka nchi jirani kama Rwanda, Burundi pamoja na Congo na kuingiza hapa katikati ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la viwanda, Wilaya ya Hanang' tunayo fursa kubwa, kwani tunayo chumvi ya kutosha, tunayo malighafi ya simenti yenye zaidi ya miaka 100, tunayo dhahabu ya kutosha. Tunaomba Serikali iangalie Wilaya ya Hanang' kwa jicho la kipekee na wananchi wako tayari kwa ajili ya kupokea viwanda kwa ajili ya uwekezaji ili kukuza pato la Taifa na kutoa ajira kwa wananchi wa Wilaya ya Hanang' Mkoa wa Manyara na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali yangu, Serikali iliyofanya kazi kubwa katika nchi yetu, imeweza kuboresha Bandari ya Tanga na sasa inafanya kazi kubwa na nzuri sana. Unapoongelea suala la bandari, namna ambavyo imeboreshwa, fedha zinazopatikana pale lazima uone sasa magari yanayotoka bandarini, njia zinazopita lazima ziwe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea kwa Kanda ya Kaskazini kwa maana ya Bandari ya Tanga ukitoka Tanga mpaka unapofika mpakani Gehandu ambako ni Wilaya ya Hanang' Mkoa wa Manyara kwenda Singida kipande korofi cha barabara ni kipande cha kutoka Dareda mpaka Gehandu Jimbo la Babati Vijijini pamoja na Jimbo la Hanang'. Kazi hii kubwa imeshafanyika. Ninaomba tufanye ukarabati mkubwa wa kukwangua ile lami kwa sababu imewekwa viraka mara kwa mara lakini bado imekuwa ni sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imekuwa ni sugu kwa sababu Wilaya ya Hanang' ni Wilaya zalishi ya mazao ya kibiashara pamoja na mazao ya chakula. Ninaomba sana, moja ya viwanda vinavyotakiwa kuwepo Wilaya ya Hanang' ni viwanda vya nafaka. Tutapandisha sana thamani ya mazao ya watu wetu kwa sababu ni wakulima wakubwa na ndiyo maana barabara inaharibika mara kwa mara kwa sababu magari mengi yanaingia pale kuchukua mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya ya kuendeleza vijana hususan kujenga vyuo vya *VETA* nchini. Serikali inatoa fedha kwa ajili ya mikopo kwa vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa, ili kuwa na mpango endelevu, vijana hawa wanapotoka *VETA* kuwe na utaratibu wa kuwakopesha vifaa ili baada ya hapo wanatoka wakiwa na elimu, lakini pia wanapata vifaa, na baada ya hapo wanapewa muda wa kurejesha fedha ambazo zimetolewa na Serikali. Hii itasaidia kuleta tija zaidi ya vile ambavyo tumeweza kuvianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asia Halamga. Nilimtaja Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, ajiandae

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninafurahi jinsi unavyolitamka jina langu vizuri sana, hivyo ndivyo linavyotamkwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyekiti wa chama chetu Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na vikao vyake kwa kuniteua niweze kugombea Ubunge katika Jimbo la Kinondoni; na hapa niwashukuru sana wananchi adhimu kabisa wa Jimbo la Kinondoni kwa kuweza kunichagua na kunirudisha tena Bungeni. Nataka niwaambie *aluta continua*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajadili hotuba zote mbili kwa pamoja. Kwa hali hiyo basi, niseme kwanza kilichonifurahisha ni kuona kwamba Mawaziri wote wawili wanatueleza kwamba mipango pamoja na bajeti ambazo zinatarajiwa, ambazo wamezieleza vizuri katika maandiko yao ni kwamba ni mambo ambayo yanakwenda kugusa wananchi mmoja mmoja na hivyo kuboresha ustawi wa wananchi wetu na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lazima tulipigie mstari. Hakuna maendeleo yanaweza kusimama kama hayamgusi mtu. Maendeleo lazima yaguse mtu na naamini kabisa Mheshimiwa Profesa Kitila kwenye mipango hii hakika tutaweza kwenda ku-*win* vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa na wananchi wa Kinondoni, nizungumzie mambo manne kwa haraka. Kwanza ni kuhusu urasimishaji wa maeneo ambayo hayajapimwa katika Jiji la Dar es Salaam, hakika hili ni jambo ambalo linatuumiza sana na nitalieleza vizuri huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni upatikanaji wa maji. Miaka zaidi ya 60 ya Uhuru bado Dar es Salaam tuna-*struggle*, na kuna kipindi hali inakuwa ngumu. Najua kwamba, kuna mpango huu wa Bwawa la Kidunda ambalo mpaka sasa hivi wanasema takribani 40% imeshatekelezwa na kwamba ifikapo Disemba mwaka huu, 2026 Mungu akijalia bwawa lile litakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba kwa Serikali ni kuhakikisha kunakuwa na *cashflow* (mtiririko wa fedha) usikatike ili ifikapo Disemba hakika bwawa hili ambalo linakwenda kunufaisha wakazi zaidi ya milioni sita wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na wale wa Mkoa wa Pwani, hili ni jambo muhimu sana. Maji ni uhai, maji ni uchumi, maji ni viwanda, maji ni kila kitu, hivyo suala la maji tusilichukulie kama ni suala poa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninampongeza Waziri Mkuu, kwenye 10% ya mikopo amezungumza vizuri hapa wiki iliyopita. Ombi langu kwa Serikali, wakati mwingine inatoa matamko, na maelekezo inawaelekeza watu wa chini, lakini kama haikushusha barua, tunakutana na watendaji kule chini wanakwambia Serikali inaendeshwa kwa makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umemsikia Waziri Mkuu Bungeni, anasema nimemsikia, lakini karatasi iko wapi? Barua ya Serikali iko wapi? *Where is the commitment?* Iko wapi *commitment* ya Serikali? Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, popote alipo, naona hapa hayupo, lakini Serikali ipo humu ndani, ishushe barua zinazokwenda kwa watendaji kule chini kuwaelekeza jinsi ya kurekebisha na kulegeza masharti magumu ili wananchi waweze kupata hii mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, naomba nilete fikra mpya. Yawezekana hizi fikra zilikuwepo, na hii inahusiana na Jiji la Dar es Salaam. Dar es Salaam ni Mkoa kama mikoa mingine, lakini kiukweli ile *governance structure* jinsi mkoa unavyotawaliwa kwa kutumia sheria zile za Serikali ya Mitaa, hakika hatuisaidii Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam yawezekana sasa hivi na inasemekana kwamba ni moja kati ya majiji yanayokua kwa haraka sana katika Afrika na hata katika majiji ya kidunia, Dar es Salaam inatajwa kwamba inakua haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukua kwake, sheria ambazo zinasimamia Dar es Salaam zinadumaza maendeleo, hazifungui fursa kikamilifu ili Dar es Salaam itumike kama

*economic hub*, kama eneo ambalo linaweza likasaidia uchumi wa nchi hii na kuweza kusaidia mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yamefanyika katika majiji mengi duniani. Nimefanya *study* kidogo kule Shanghai China, Shanghai imesaidia sana kukua kwa miji mingine mingi sana kutokana na jinsi Serikali ilivyopeleka umuhimu katika jiji lile na kubadilisha taratibu za kiuendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia takwimu, *African Development Bank* waliandika taarifa yao ambayo imeandikwa katika kitu kinachoitwa *Smart Cities Dive*. Wanasema Dar es Salaam kati ya mwaka 2005 - 2025 imekua kwa 85.2%. Ni ukuaji mkubwa, tusiuchukulie poa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na ukuaji huu, Dar es Salaam ina watu milioni sita na ushee, lakini wanaoingia mle na kutoka sio chini ya watu 5,000 kwa siku. Hili ni jiji ambalo watu wanafuata mahitaji ya kibiashara, mahitaji ya kimaisha na vitu vingine. Kwa hali hiyo basi, utaona kwamba Dar es Salaam ina mchango mkubwa sana kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua 17% pekee inatoka Dar es Salaam, lakini hata ukiangalia mapato ya Serikali *(Government Revenue)* zaidi ya 80% zinakusanywa kupitia Dar es Salaam kwenye bandari, kwenye masuala ya viwanda na uzalishaji, vilevile kwenye mambo mengine mengi ambayo yanaifanya Dar es Salaam kuwa hakika ni kitovu cha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo nilisema kuhusu makazi yasiyo rasmi. Sikiliza, 70% ya watu wa Dar es Salaam tunaishi katika maeneo ambayo hayajapimwa. *Can you believe this*? Unaweza ukaamini Dar es Salaam, Jiji linalokua kwa haraka, tuko Kinondoni pale tumezungukwa na *squatters!* Siyo jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba mpango huu unaokuja ambao leo uko katika mapendekezo, utuambie, utoe *details* useme neno moja, Serikali inakwenda kufanya nini katika suala zima la urasimishaji wa ardhi katika Mkoa wa Dar es Salaam?

Kama fedha haitoshi, tuanze na Kinondoni iweze kuwa mfano. Kinondoni ipimwe ipendeze, halafu mtaona ni jinsi gani tunahitaji kufanya urasimishaji wa maeneo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niseme sasa, Dar es Salaam kwa kutumia Sheria za Serikali ya Mtaa itabidi tuwe na mtazamo mwingine mpya. Hapa sasa najikita kuiomba Serikali ijitolee kufanya utafiti, itembee katika majiji ambayo yamekua kwa haraka zaidi, ambayo yanahitaji *transformation* ili ule utafiti utuambie Dar es Salaam itawaliwe kwa sheria zipi? Siyo hizi ambazo sitaki, nitaje mikoa ambayo mtasema Tarimba labda nina *downplay* mikoa mingine, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba sheria zinazotumika Dar es Salaam ndizo hizo zinazotumika Sumbawanga, sheria zinazotumika Dar es Salaam ndiyo hizo zinazotumika kwetu Tanga. Mahitaji ya maeneo haya yako tofauti. Hivyo, ninaomba ufanyike utafiti ambao kama ukifanyika mapema na ukiwahi ndani ya kipindi hiki cha miaka mitatu, wakati Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan bado ni Rais, kwa sababu ninaamini matokeo ya utafiti ule, Rais wetu kipenzi atapenda kuona Dar es Salaam inakuwa *transformed*, Dar es Salaam inakwenda kusaidia uchumi wa Tanzania ili uchumi wa Tanzania ukamsaidie mwananchi mmoja mmoja kwa kupitia mambo makubwa ambayo yapo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba. Nilimtaja Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo na Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nami niweze kuchangia hotuba ya Mpango wa Miaka 25 (2025 - 2050).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza sana Rais kwa maono mazuri. Ninawapongeza sana Mawaziri wote

wawili kwa jinsi walivyoaminiwa kutengeneza mpango wao mzuri ambao unatia matumaini kwa Watanzania. Niendelee kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Itilima kwa kuendelea kuniamini kuwepo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango hii mizuri ambayo imeletwa, wameongea wachangiaji wenzetu, lakini Mheshimiwa Prof. Muhongo amejaribu kuongea kwa mapana sana. Niende tu kusema kwamba Serikali iangalie sehemu za kimapato ambazo zinaingiza kwenye nchi yetu. Hapa ni mashahidi, Rais alikuja na mpango wa kupanua bandari, *DP World,* leo pale Dar es Salaam ukifika mizigo iliyopo ni zaidi ya mara tano yake, barabara zimefungwa kwa sababu mizigo imejaa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali katika mpango huu tuwe na mpango wa dharura, wa haraka utakaoweza kurekebisha barabara, tusitumie barabara moja ya kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro. Tuangalie namna gani hata kupita Kisarawe itokee Morogoro kwenda Iringa kwenda Tunduma. Nasi kama Watanzania katika mipango yetu tunayoiweka hapa Mezani, tukumbuke tuna nchi saba zinatuzunguka hapa, huo tayari ni uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapozungumzia pato la Mtanzania, tunapozungumzia kufika shilingi trilioni 477 kwa miaka mitano inawezekana tukiwa na uthubutu wa maamuzi. Viongozi wetu mlioko hapa Mezani chukueni mawazo haya, tubadilishe mfumo katika uchumi wa mali ambayo inapatikana kwa haraka ili tuweze kufika matarajio ambayo tunayoyatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hatuwezi kukwepa kilimo. Karibu 70% ni ya wakulima na wafugaji, lakini wote hawa ni wafanyabiashara kwa sababu wanazalisha mali. Nini kifanyike? Ninaomba kati ya fursa zilizopo katika mikoa yote ya nchi ya Tanzania iangaliwe ni mkoa upi unahitaji uwekezaji wa aina gani ili tusaidie uwekezaji katika maeneo husika ili tuongeze pato la Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo tunayoizungumza katika Bunge letu hili Tukufu, hao waliokaa hapo wote ni wachumi. Vilevile kuna Profesa mmoja, amekuwa Chuo Kikuu miaka mingi sana na amefundisha wanafunzi. Bila kuwa na maamuzi, bila kuwajengea uwezo watumishi wetu, haya tunayoyazungumza bado tutakuwa tunapiga *mark time*. Ninazungumza hivyo kwa sababu gani? *Experience* inatuonesha, Bunge na Taifa, viongozi wengi wanakosa uthubutu wa kufanya maamuzi. Akiamua, akifanya hivi, pataingia na dosari hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninaliona binafsi na Taifa kwa ujumla, tunapozungumza uwekezaji mkubwa, je, tuna benki za maendeleo? Benki zetu zilizoko hapa ni za *commercial,* maana yake mipango yote tunayoifanya hatuwezi tukafika kwa sababu benki zetu ni za *commercial,* zinatubana kisera, zinatubana kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima Benki ya Maendeleo iimarishwe katika Mpango wa miaka 25, watafute watu wenye weledi, wenye kuweza kusimamia hizo benki ili kusudi haya tunayoyazungumza yawezekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa yote, nchi zinazotuzunguka ukiziona ni ndogo sana, sisi tuna takribani watu milioni 70, tayari ukizungumza uchumi ni pamoja na watu, lakini tunakosa nini? Tunakosa maamuzi ya kusimamia na kuelekeza nini kifanyike? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuomba, Taifa kama Taifa tuwe na lugha moja, kuanzia chini hadi juu tukizungumza iwe lugha moja ya kufanya utekelezaji. Bila hivyo, mipango yetu ambayo tutakuwa tunaijadili hapa tutakuwa tunafeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukizungumzia sekta ya usafiri, ukiondoka hapa kwenda tu Tunduma, ukifika pale malori yanakaa zaidi ya siku 14, tumezuia Uchumi, lakini pale tungetengeneza *parking* kubwa tukapanua, leo *RTO* wa pale kila siku anaongelea tu habari ya kuvusha gari, kuvusha gari, nasi tupo

na viongozi mpo, lakini majibu hayapo, na huku tunazungumzia fedha, tutazitoa wapi? Ninaomba hilo jambo tuliangalie kwa mapana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, sekta zetu za kilimo; kahawa, tumbaku, pamba; kwenye mazao haya tumekuwa na mchanagnyiko. Mchanganyiko huu ninaomba katika Mpango huu iwekwe vizuri. Tunapozungumza kutoza *VAT* kwa mtu anayezalisha kiwanda cha ndani, anayefanya *export,* halipi *VAT,* maana yake ni kwamba, unatengezea mazingira mwekezaji wa ndani aende akamtoze mkulima, atoe risiti ili ile risiti ya 18% akatwe halafu huyu aje achukue kodi. Hicho kitu hakitawezekana, biashara itakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wetu huu wajaribu kuangalia ni namna gani ya kutengeneza kodi ya kupata mapato ili tufikie malengo ambayo tunayatarajia. Tukifanya hivyo, itakuwa ni sehemu nzuri sana katika kuchochea uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wameelezea, wakasema, miaka mitano hii inatakiwa tufanye uwekezaji wa zaidi ya shilingi trilioni 477, ni jambo jema. Hata hivyo, nilichokuwa ninataka kusema, pamoja na mipango hii, basi tutengenze historia, kwamba, kila mwaka tunapokutana kwenye Bunge lako Tukufu tuangalie tumefanya nini ndani ya miaka mitano, na ni kipi ambacho kimeonekana na kwenye mkoa upi ili tufanye kazi ya kuwa na majawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Kule Simiyu tulikuwa tumeandaa mpango wa kujenga kiwanda cha vifaatiba ambacho kingefanya kazi kwenye nchi nzima kwenye hospitali zetu. Ule mpango umefanya baada ya miaka mitano kwisha, kila kitu kimepokea, na fedha za Watanzania zaidi ya shilingi bilioni moja zimetumika kufanya *due diligence* kwenye maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, ninaomba, jambo hilo ni muhimu sana ambalo wataalamu wanaweza wakatusaidia ili kuyafikia malengo tunayoyatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Prof. Kitila ameandika katika mambo matano yanayohusika. *Technology*, afya na kadhalika. Ninaona kuwa tukitaka kufanikiwa sehemu kubwa sana, cha kwanza tuondokane na suala la kulipa *cash*. Ukienda kwenye nchi za wenzetu, kila fedha wameshaweka utaratibu wake. Ukiingiza tu, kwamba umepanda hata *taxi,* ukilipa *automatically* fedha yake inakwenda Serikalini na mwenye chake anabakinacho, hakuna kuonana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi mazingira tuliyoyafanya ni ya kuonana ili kusudi watu wafanye mazungumzo ili kusudi kupoteza muda. Hata suala la *VAT* ukiliangalia halina maana kwamba mtu umeagiza mali, ukaitoza Serikali, ukalipa, ukaweka kwenye *account* Serikali hiyo hiyo tena inakuja kukurudishia fedha. Sasa unajiuliza, ni nini? Ni lazima tuangalie utaratibu mpya utakaokuja kutusaidia kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nchi zote tunatumia hizi *iPad, computer, iPhone, Samsung* na kadhalika. Wenzetu wanakaa na kuangalia, huyu mwenye kampuni X tumwezeshe nini ili tupate kodi ya kiasi gani ndani ya miaka yetu; mwaka mmoja au miaka mitano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa tunawazungumzia matajiri wanne, au watano tu, wakihama tunaanza kuulizana kwamba tunatokea wapi? Tunaondokea wapi? Serikali ifike mahali ibadilike, ianze kujenga uchumi wa mtu na kumsimamia yule mtu ili afanye kazi ya kulipa kodi ndani ya nchi yake. Hakuna jambo lisilowezekana. Inawezekana, lakini kinachohitajika ni utashi na uthubutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa tuliyoyazungumzia hapa yameendelea kwa sababu kwanza yamewekeza kwa watu, watu walio na akili, wenye uwezo wa kufikiri, wenye kujiamini. Siyo kwamba mtu unapewa nafasi, umesimama pale, hujiamini, hutoi maamuzi, maana yake unatuchelewesha. Hivyo, hufai kuwepo katika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kuomba, katika Taifa letu hili, tunayo mambo mengi makubwa. Tuna madini, mifugo, uvuvi, na ng'ombe. Tuna kila kitu, lakini bado tunakwama kwa sababu ya kutoweka uthubutu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu suala la usafiri. Nchi yetu takribani ni watu milioni 70, wafanyabiashara zaidi ya milioni tatu, milioni nne wanahitaji kusafiri kwenda kujifunza, kwenda kubadilisha maeneo, lakini leo hata hapa *SGR* unakaa zaidi ya masaa Matano, unasubiri usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yule mtu anayekwenda kufanya kazi, hawezi kufanya kazi ya haraka na kurudi kuongeza kuchochea uchumi katika eneo letu. Ninaomba, suala la usafiri ni muhimu sana. Ni muhimu kwa sababu hao watachochea uchumi kwenye maeneo husika. Ukienda Ethiopia wao wana ng'ombe tu, lakini sisi tuna vitu zaidi ya 10, utalii na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege tulizonazo ni nne, tano na kila siku zina-*delay*. Kwa hiyo, viongozi wetu waliopo hapa waangalie utaratibu mzuri ili wawatumie wataalam tulionao. Tuna wataalamu wazuri sana, hata kwenye maandiko. Changamoto kubwa ni uthubutu. Akifanya uthubutu ataambiwa, ulimwona fulani? Kwa hiyo, jambo hili kama Taifa ni lazima tulikemee, tulipige marufuku ili watu wafanye maamuzi ya kuleta maendeleo ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru sana. Baada ya kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi ya kuchangia katika mpango. Kwa nafasi ya pekee nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa

kuweza kunirudisha katika jengo hili na kuendelea kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Missenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, na Rais wetu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na uongozi wa chama pia kwa kuniteua na kunipa nafasi ya kuweza kutetea kiti hicho na kurudi katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee niwashukuru wananchi wa Jimbo la Missenyi ambao wamenipa ridhaa ya kurudi kuendelea kuwatetea katika hoja na mahitaji yote ndani ya Jimbo letu la Missenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee ninaomba nitoe pongezi kwa ufupi. Nimpongeze Mheshimiwa Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wote na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuingia katika jengo hili ili kuendelea kuishauri Serikali katika mambo ya msingi kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara ya Mipango na Uwekezaji chini ya Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila Mkumbo; Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Chaya; Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Balozi Khamis na Naibu Waziri wake kwa jinsi ambavyo wameandaa Mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitia mipango ya muda mrefu ya miaka 25, miaka mitano na mwaka mmoja. Pongezi kubwa ni kuandaa dira na mipango elekezi kwa wakati mmoja, jambo ambalo lilikuwa halijawahi kutokea na lilikuwa ni kikwazo cha nyuma, lakini *this time* wamefanya hivyo. Ndiyo maana tuna uhakika kuwa mipango hii ikisimamiwa, lakini pamoja na maboresho tunayotoa tunaamini tutafika mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika maeneo ya Mpango yaliyoelekezwa, kuna maeneo ambayo yamewekewa mkazo. Nitajikita katika maeneo machache, kama matatu hivi

kama muda utaruhusu. Suala la kwanza ni katika upangaji, upimaji, na utoaji hati katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaongelea suala la ardhi. Pia nitaongelea kuhusu kutumia fursa zinazotokana na jiografia, ambapo tuna madini katika nchi yetu. Tatu, nitaongelea kuhusiana na mazingira rafiki ya uwekezaji na biashara, na hapo nitaongelea kuhusu biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuwa Tanzania tuna utajiri wa ardhi. Tuna kilomita za mraba zaidi ya 947,000; na sehemu hiyo tukitoa sehemu ya maji ambayo ni 6.2% eneo lililobaki lote ni sehemu ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona, kwa matakwa mema ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia kauli yake aliyoisema kwamba anahitaji kuona kuwa kila kipande cha ardhi katika nchi yake anayoisimamia kinapimwa. Tumeona sasa ongezeko la hati za viwanja na mashamba, kutoka mwaka 2021/2020 ambapo ilikuwa takribani hati milioni mbili, lakini leo tunaongelea milioni tatu. Pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu. Hii inaonyesha kuwa kiongozi akiwa amedhamiria inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo tunakusanya fedha kutokana na ardhi, tunakusanya kodi ya ardhi, tunakusanya kodi ya upimaji, tunakusanya kodi ya *survey*, tunakusanya kodi ya uthamini. Hata hivyo, ukiangalia makusanyo na hitaji la uwekezaji katika eneo hili, kwa sasa hivi haliendi sawa. Zipo sababu ambazo tunatakiwa kushauri kwenye mpango ili ziweze kuwa *accommodated* tuweze kupata *return on investment* tutakayowekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Kamati ya Bajeti imetuambia, kwamba tunahitaji takribani shilingi bilioni 591 kuwekeza Wizara ya Ardhi ili tuweze kupima, tuweze kupanga na kuweza kutoa hati, lakini ukiangalia katika eneo hilo mwaka 2025, Wizara ya Ardhi ilijiwekea malengo ya kukusanya shilingi bilioni 250 kutokana na

kodi ya ardhi lakini iliweza kukusanya shilingi bilioni 146 peke yake. Sababu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwalaumu, tunataka tuwawezeshe sasa ili waweze kukusanya vizuri. Ukiangalia Kodi ya Ardhi imebaki ni hiyari ya mtu mwenye hati ndiye anayeweza kulipa Kodi ya Ardhi. Wameweka *penalty* kwamba unaweza kuweka *penalty* lakini haimlazimishi mwananchi au anayemiliki hati kwenda kulipa Kodi ya Ardhi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili linafahamu kuwa nchi yetu tunaendesha mfumo wa bajeti yetu kwa *cash system,* kwamba tunachokusanya ndicho tunachokipeleka kwenye bajeti tuliyojipangia ili tuweze kutekeleza majukumu yote yaliyopo katika bajeti hiyo. Sasa tusipokusanya leo, tunasema leo tumeweka *target* ya kukusanya shilingi bilioni 500 ukakusanya shilingi bilioni 100, maana yake hiyo bajeti itaendeshwa na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu hili mwaka 2025 lilinituma nikaongoza *delegate* ya Waheshimiwa Wabunge kwenda nchini Ethiopia kwa suala lingine, kuangalia ni jinsi gani *diaspora* wanavyochangia katika pato la Taifa nchini Ethiopia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jukumu hilo, sisi tulijiongeza tukaenda kwenye mambo mengine ili kuweza kuona ni jinsi gani sasa Ethiopia inakusanya *land rent*. Kitu ambacho tunakosa katika nchi yetu, Ethiopia imekitatua, kwa kuwa na sheria ambayo inawekeza kufanya *enforcement* ya kukusanya *land rent.* Sheria hizo nikizinukuu, kuna *Urban Land Lease Holding Proclamation No. 721, 2011*, na kuna *The Federal Rural Land Administration and Use Proclamation No.* 456, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi zinampa Waziri wa Ardhi kuweza kufanya *enforcement* kwa ajili ya kukusanya fedha kwa wakati ndani ya mwaka. Kama una hati milioni tatu kama tulizoona, tunategemea tuone *reflection* ya fedha zilizokusanywa kutokana na hati zilizopo katika nchi yetu, lakini kwa sasa suala hilo haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijifunza kutoka katika Wizara nyingine, kwa mfano Wizara ya maji, leo ukiwa na bili ya maji wataalamu baada ya muda watakuja na kukupigia simu. Pia wanakufuata ili kuhakikisha kwamba umelipa bili ya maji ili sasa tuendelee kupata *service.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ardhi, kwa mfano, kama mimi ninadaiwa Kodi ya Ardhi, nitaendelea kudaiwa hadi siku nikijitoa mwenyewe niende kule. Hata kama *penalty* ipo, haisaidii kwa wakati huo, hizo fedha hazijakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe sana, kupitia Bunge lako Tukufu kama kuna kikwazo tujifunze kwa wenzetu wa Ethiopia. Tuwe na sheria ambayo itampa mamlaka Waziri wa Ardhi waweze kukusanya hizo fedha ili tuendelee kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kwenye suala hili la ardhi, tunayo nguvu kazi ambayo imelala kule halmashauri. kwa bahati nzuri nimekuwa mtumishi wa umma, nimekuwa Mkurugenzi wa Wilaya. Tulikuwa na wataalamu wa ardhi ambao wanawajibika katika baraza, wanasimamiwa na Mkuu wa Wilaya, lakini leo wataalamu wetu wa ardhi wapo kule *redundantly,* hawana mwenyewe. Ninaweza kusema ni watu ambao hawana baba wala mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi aweze kusema kwamba anawasimamia kufanya kazi, halmashauri wanawaambia kuwa wao sio mamlaka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshiriki kusaini *MOU* ya kuhamisha majukumu ya injinia wa ujenzi kwenda TARURA, nimeshiriki kusaini kwenda *RUWASA,* leo tunaona *RUWASA* na *TARURA* zinavyofanya kazi nzuri katika eneo la kila Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwenye upande wa ardhi tunashindwa nini? Kama hatuwezi kuwarudisha halmashauri, basi tutii kama Mheshimiwa Rais aliyoelekeza, tuunde *Land*

*Commission* au *Agency* ambayo itakuwa inasimamia suala la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule chini suala la upimaji, suala la upangaji, suala la hati limedorora, na kwa hiyo, makusanyo ya *Land Rent* hayawezi kuwepo bila wataalam hawa na nguvu hii kusimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, na wataalamu wenyewe wanamlilia nani? Wanamsemea nani? Hakuna mtu anayewasikiliza matatizo yao. Changamoto walizanazo ni za kwao, vitendea kazi hawana, wapo katikati ya halmashauri na Wizara. Wapo pale. Mimi ninaomba mpango huu uweze ku-*reflect* kwenye suala hilo ili kuhakikisha kwamba inalitibu. Ninaamini kuwa wataalamu wetu wakiwa katika hali nzuri masuala ya kukusanya kodi, upimaji, upangaji yatakuwa ni mazuri zaidi, na tutaongeza ajira na pia pato la Taifa hili litaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ambalo nataka kuchangia ni suala ambalo nimesema ni kuhusiana na mpango elekezi kwenye eneo la fursa zinazotokana na kijiografia, hasa upande wa uwepo wa madini. Katika eneo hili, tunaona kuwa pato la Taifa kutokana na madini ni 10.1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Prof. Muhongo hapa amesema kwamba tukitaka kufanya vizuri zaidi katika Taifa letu tuna uwezo wa kupambana mpaka tukapata 20% iwe ni pato la Taifa kutokana na madini. Hapo ndipo tutakuwa kidogo tunasogea katika kutokuwa tegemezi na Taifa letu litaendelea kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona sasa hivi mauzo ya dhahabu yameongezeka, lakini pia tunaona juhudi za dhati za Mheshimiwa Rais. Leo tunaona kuwa amewawezesha wachimbaji wadogo, tunaona viwanda vya kuchenjua dhahabu vimeongezeka, na pia tunaona uwezeshaji mkubwa uliopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kufanya vizuri zaidi katika eneo hilo. Kwa hiyo, tukifanya vizuri zaidi tukaongeza pato la Taifa

kwanza tunatengeneza ajira, na pato la Taifa linaongezeka. Kuna maswali madogo ambayo tunaweza kujiuliza kupitia Serikali yetu, kwamba, je, tulishawahi kujiuliza kwamba mwekezaji mdogo au mchimbaji mdogo akipewa leseni tunajua ni gharama gani anazoingia mpaka aweze kupata *gram* moja ya dhahabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao watu ambao wana vipimo, ni watu wa kawaida wa mtaani, wanakwenda kukupimia unaona kwamba kumbe mzigo upo hapa! Hivi Serikali inashindwa nini kupima ili leseni ikawa ina taarifa za kina, halafu hizo gharama za upimaji, huyu mchimbaji akaenda kukatwa kidogo kidogo, lakini tukiwa na wachimbaji wengi, tunatengeneza mabilionea na nchi yetu inapata pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia inaweza, na mipango yetu ikisisitiza katika maeneo hayo, tutaweza kufikia malengo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninakushukuru kwa nafasi, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent Kyombo. Nilimtaja Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka na rehema zake. Pili, ninakishukuru Chama changu cha Mapinduzi kupitia Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunipitisha katika mchakato mzima wa uchaguzi, na mpaka leo nimekuwa Mbunge wa Jimbo la Malinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Malinyi kwa kunipa kura nyingi za kishindo. Ninawaambia kuwa sitawaangusha, nipo pamoja nao bega kwa bega kuhakikisha maendeleo ya kweli yanapatikana katika Wilaya ya Malinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kura nyingi za kishindo alizozipata, lakini pia kwa kazi nzuri anayoifanya na anayoendelea kuifanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii pia kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuandaa mipango mizuri ya muda mrefu na muda mfupi. Pia ninaipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa namna walivyochangia Mpango na kutoa maoni na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, hasa maoni na mapendekezo ya Mpango ambayo yameeleza kwa kina taswira ya Taifa letu kwa kipindi cha muda mfupi na muda mrefu, na imetoa dira na malengo ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kujenga Taifa letu kwa kufanya kazi kwa bidii na weledi mkubwa, na pia kuyafanyia kazi yale yote yaliyopendekezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia kuhusiana na ahadi za viongozi ambazo zilikuwa katika mapendekezo ya Kamati. Ahadi za viongozi wakuu wa nchi hii ziwe sehemu ya mpango. Nimesoma mle lakini sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza ahadi kuu za viongozi wa nchi hii, wale viongozi wakubwa, ziwe sehemu ya Mpango na zipangiwe kabisa bajeti ili tuweze kuzitekeleza na wananchi waweze kufurahia ahadi ambazo viongozi wakuu wanapoenda kwenye maeneo wakitoa ahadi ili Serikali iweze kuzitekeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatolea mfano kwa Jimbo langu kule la Malinyi, kwa vipindi vitatu vya viongozi wakuu, tangu wakati wa Mheshimiwa Mkapa, amekuja Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, amekuja Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli,

wote waliahidi kuwa watafungua ile njia ya kutoka Malinyi kwenda Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wanapokaa wanategemea kuwa ahadi za Serikali huwa zinanukuliwa sehemu, zinaandikwa na zinakuja zinatekelezwa, lakini mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezeka. Hii inakuwa siyo picha nzuri kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba suala hili la ahadi za viongozi liingizwe kwenye Mpango na litengewe bajeti mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ninaomba nichangie kuhusu suala la vipaumbele. Ninaishauri Serikali, inapoweka vipaumbele vyake iwe na vipaumbele vya kimkakati ambavyo vitatoa matokeo chanya na kuleta tija kwenye jamii husika. Kwa mfano, miradi mingi ya Serikali imekuwa kwamba, wanaweza wakapeleka kwenye kata moja mradi wa shule, wamejenga, imeishia kwenye boma, lakini baada ya siku kadhaa, unakuta tena Serikali inaleta mradi mwingine wa shule ambao unaanza upya badala ya ule mwingine kuukamilisha. Kwa hiyo kuna vitu kama hivyo vinakuwa navyo siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nilikuwa naishauri Serikali iwe na vipaumbele katika maeneo husika. Tunapotoka huko, na ukizingatia, kama kule kwangu Malinyi utakuta kuna kata moja inapelekewa zahanati au kituo cha afya, lakini hapo hapo tena wanakuja wanajenga zahanati ilhali hii nyingine inakuwa bado haijakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninapenda kuchangia kwamba vipaumbele hivi viwe vya kimkakati ambavyo vitatoa matokeo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichangie sehemu ya utalii. Ninaipongeza sana Serikali kwa kuona kuwa utalii ni sekta muhimu sana ambayo inaliingizia Taifa mapato. Pamoja na jitihada zote hizo kubwa zinazofanyika, bado kuna vivutio vingine vingi ambavyo Serikali bado haijavirasimisha au haijavibainisha kuwa pia ni vivutio vya utalii katika maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mkoa wetu wa Morogoro tuna vivutio vingi vya utalii. Kuna maporomoko ya maji kule ambayo huwa yanatiririka yenyewe. Kwa hiyo, hapo ni kivutio mojawapo. Pia kuna mabonde yale ya Udzungwa ambayo nayo pia ni kivutio kikubwa sana cha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kwangu kule Malinyi kuna kivutio cha utalii cha bwawa. Kuna bwawa moja ambalo ni la kihistoria na ambalo ni zuri sana. Labda niwaeleze kidogo. Kule Malinyi tuna bwawa moja katika eneo la Kilosa Mpepo, kunajulikana sana kwa jina la Iyowanja kwa sababu watu wengi, hata viongozi hapa ndani, ninadhani hata Mheshimiwa Tarimba anakufahamu Iyowanja, kwani alikuwa anatoka *Chief* Kilembwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kuna bwawa la maajabu ambalo ni kubwa. Bwawa hili lina viboko weupe, weusi, pia lina mamba, samaki na pia lina ndege wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa hili lilikuja kuwa ni la kihistoria kwa sababu kulikuwa na mwanamama mmoja ambaye alikuwa anaonewa sana na mume wake, yaani ananyanyasika sana. Kwa hiyo, baada ya yule mama kuwa anatafuta suluhu yake ni nini, alikwenda kwa Chifu ili aweze kupata msamaha au msaada ili mume wake asimpige. Alipoenda kwa Chifu, alitegemea Chifu atampa jibu pale pale au atatoka naye kwenda kwa mume wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, baada ya hapo, Chifu akamwambia, nimepokea malalamiko yako. Kwa hiyo, wewe nenda, sisi tutakuja kesho. Yule mama akawa anaogopa kurudi kwa sababu yule mume wake kule nyumbani atampiga. Kwa hiyo akawa amekaa pale, akasema mimi siondoki, ninaogopa mume wangu atanipiga kule. Chifu akamlazimisha akisema nenda sisi tunalifanyia kazi, kesho tutakuja na hii timu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mama alivyokuwa amemuaga Chifu, amegeuka tu amempa kisogo, huku nyuma likatokea bwawa. Kulikuwa na kijiji pale, nyumba kama mia mbili

na zaidi zote zilizama kwenye maji. Pale pakageuka bwawa. Lile bwawa likawa lina viboko weupe, Weusi, samaki wengi sana, lina mamba wengi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu ni kwamba wale mamba hawali binadamu. Unaweza ukashangaa ni lini mamba akakosa kula binadamu? Wale hawali binadamu, wako pale. Ila akitoka, na mafuriko hivi yakatoka, yule mamba akaenda kwenye mito huko huko, akienda anakula, lakini akiwa kwenye lile bwawa hali. Kwa hiyo, ni kivutio kizuri mno, na ni bwawa kubwa kabisa kama Bwawa la Mindu, labda limepungua kidogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninapendekeza kwamba maeneo kama haya ya utalii nayo yaweze kurasimishwa, kubainishwa ili yaweze kuongezea Taifa mapato pamoja na ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsanteni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku. Waheshimiwa Wabunge watakaoanza kuchangia jioni ni Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, Mheshimiwa Regina Henry na Mheshimiwa Sara Msafiri na wengine wataendelea.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile tumemaliza shughuli zote za mchana, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge Wanawake kuhusu mkutano wetu. Ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Mipango.

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali Katika Muda wa Kati ya 2026/2027 - 2028/2029**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga atafuatiwa na Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuwa mahali hapa, muda na wakati huu. Pia nikishukuru Chama Cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kwa kupendekeza jina langu na kuendelea kuwa mwakilishi wa wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam. Vilevile, niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuendelea kuwa na imani na mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa kwa kumpongeza Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kaka yangu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Mpango huu. Pia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar kwa maandalizi mazuri ya huu Mpango. Mpango huu ni mzuri sana, lakini endapo utatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Mpango Elekezi ni Dira ya 2050 ambayo imejikita kabisa katika kuhakikisha pato la Taifa linaongezeka na uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa kuzingatia fursa za usawa kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia utekelezaji wa Mpango huu ili tuone tija na matokeo na kupima utekelezaji wake, mdau wa kwanza ni mwananchi na ndiyo maana kukawa na suala la kufikiria namna ya kuongeza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kuwainua wanawake kiuchumi, kuwainua jamii kiuchumi au pato la mwananchi, tukienda kuangalia Mpango huu na fursa ya mikopo ya 10% kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, nilikuwa ninapendekeza Maafisa Biashara wa Halmashauri wawe karibu sana na vikundi vinavyonufaika na mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Biashara hawa watasaidia sana katika suala la elimu, kuwaonyesha namna ya kuzifikia zile fursa, mafunzo ya ujasiriamali na mafunzo ya fedha. Vikundi vingi

vimefeli katika mikopo wanayopewa kwa sababu ya kukosa elimu. Lengo la mikopo hii ni zuri sana, lakini utekelezaji wake umefeli, sababu wanufaika wengi wanapata pesa kabla ya kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi viko vya aina tatu. Kuna kundi la kwanza ambalo wao wanaunda vikundi kwa kusubiri mikopo, na wengi wao wamepata, lakini wameshindwa kurejesha. Kuna kundi la pili ambalo tayari wameshaanza uwekezaji mdogo mdogo, wao kama wao. Mikopo hii imewasaidia lakini bado haijafikia lile lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la tatu, ni makundi ya wanawake wawekezaji wa huduma ndogo za kifedha almaarufu kama vikoba. Hawa tayari wana mitaji yao, wanawekeza hisa kwenye vikundi vyao, wanakopeshana mikopo midogo midogo, wenyewe wanahitaji fedha kubwa kwa ajili ya kufanya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninapendekeza fedha hizi ziangalie makundi yote matatu. Kuwe na makundi mbalimbali, yaani kundi hili lipate mkopo huu; kundi hili, mkopo huu; na kundi hili mkopo huu. Dira inasema, kuwe na viwanda vidogo vidogo. Sasa ili tuvione hivi viwanda, lazima vikundi ambavyo vinajiweza na vina mitaji viweze kukopeshwa mikopo kwa ajili ya kuanzisha viwanda. Vikundi hivi Mkoa wa Dar es Salaam vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam kuna vikundi vya akina mama vina mitaji mpaka shilingi milioni 700 mpaka shilingi bilioni moja. Sasa watu hawa hawatafuti mikopo kwa ajili ya kukopeshana wao, hawa wapewe mikopo kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi haya ambayo yanajiweza, tunaomba waunganishwe kwa wadau mbalimbali wakubwa au makampuni, viwanda na wawekezaji. Dar es Saalam ni mkoa ambao una viwanda vingi sana pale. Kuna wawekezaji wakubwa. Kazi ndogo ndogo za usafi, chakula, ku-

*supply* baadhi ya *material,* wapewe wakina mama wa vikundi ambao tayari wana mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ni Mkoa ambao umebeba sura ya Tanzania, ni jiji la kibiashara. Shughuli kubwa na ya msingi ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam ni ujasiriamali na biashara tu. Kwa hiyo, mitaji ndiyo hitaji kubwa na la msingi na la kwanza ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna makundi ya vijana wengi sana Dar es Salaam. Kuna vijana waliomaliza vyuo, vijana ambao hawakwenda shule wote, wapo; na wote hawa wanatakiwa kunufaika na fursa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yukiangalia kundi la vijana, Maafisa Usafirishaji maarufu kama bodaboda, kwa Mkoa wa Dar es Salaam asilimia nne tu ya vijana ndio wanamiliki bajaji zao wenyewe. Wengi wao wanatumia bajaji za kukodi, anapata fedha yake ya kujikimu na ya kupeleka kwa mwenye bajaji. Pia, wengi wao ni vijana ambao tayari wana familia au wanalea wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaomiliki usafiri wa bodaboda wa kwao ni 30% tu, 70% ni bodaboda za kukodi, lakini pia asilimia mbili tu ndio wanamiliki maguta yao wenyewe. Sasa vijana kama hawa tuangalie namna ya kuwawezesha vitendea kazi badala ya kuwapa fedha. Uhitaji ni mkubwa mno katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kata ninayoishi mimi, kuna vijana bodaboda 300 na Mwenyekiti wa Vijana wale ni kijana ambaye ni *graduate* wa chuo kikuu. Tulikaa tukatengeneza jukwaa la vijana wale ndani ya kata, tukakubaliana tukaenda kwa mtu ambaye ana-*supply* pikipiki akatupa masharti. Sharti la kwanza lazima kuwe na ofisi. Jukwaa lile lisajiliwe na kila mwanajukwaa lile awe na kitambulisho cha *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyote hivyo tulifanya, tukakubaliana kwamba wakati vijana wanasubiri mkopo wa

halmashauri, basi tuanze kuwekeza wenyewe. Tukaanza kuweka shilingi 40,000/= kila kijana kwa wiki kwenye mfuko ambao tulifungua kwenye Benki ya *CRDB*, ile shilingi 40,000/= kwa wiki, kwa mwezi tuna shilingi 160,000, na kwa mwaka itakuwa shilingi 1,920,000/= ambayo tukipeleka kule kwa muuza pikipiki, anatupatia pikipiki mpya kwa umiliki wa yule kijana, na iliyobaki anamalizia ndani ya miezi sita. Cha ajabu, ndani ya vijana 300 walioweza kufanya hilo ni vijana 20 tu na hao ni kati ya wale wanaomiliki pikipiki zao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vijana 280 wote imeshindikana kwa sababu anachokipata hakimtoshi yeye na kupeleka kwa mhusika mwenye pikipiki zake. Kwa hiyo, ninaomba, mikopo hii ya halmashauri tuangalie zaidi kwenye vitendea kazi. Tusiangalie zaidi kwenye fedha. Fedha tumeshatoa sana na zimeshindikana nyingi kurudi. Fedha nyingi hazikurudi, kwa hiyo, tuangalie pia na vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninatoa shukrani za dhati kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye suala la kuwasaidia watu kupata elimu ambayo itawasidia kujikwamua kiuchumi ametusaidia sana wanawake wajasiriamali wa Mkoa wa Dar es Salaam. Ametoa ufadhili wa wanawake 3,000 kwenda kusoma *VETA* mafunzo kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi kwa wanawake wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *batch* ya kwanza ya wanawake 405 wamesha-*graduate* wapo mtaani, *batch* ya pili ya wanawake 543 wamesha-*graduate* mafunzo yao, wapo mtaani, na mwezi Aprili mwaka 2026 tuna *batch* nyingine ya wanawake 400, lakini mpaka sasa walionufaika na mafunzo hayo ni wanawake 948. Wote hao wapo mtaani, wamesoma kozi tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe halmashauri, kundi hili lipate mikopo na mikopo yao wapate vitendea kazi waingie kabisa *site*. Wameshajifunza kutengeneza batiki, ku-*print*, kupamba, *salon,* na kila kitu wameshajifunza. Wanahitaji vitendea

kazi waingie kazini. Hawa waweze kuzalisha, wajikwamue wenyewe na waongeze pato la uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya kundi hili tutengeneze walipa kodi wapya. Hasa Kundi la wanawake 948 Mheshimiwa Rais ameshawapa ujuzi, wapo mtaani, hawana mikopo, haisaidii na inavunja moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya wajasiriamali wa Taifa hili. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu imeshapata shilingi bilioni 10.5 ambayo inakwenda kwa makundi ya wajasiriamali hawa hawa wadogo wadogo ambao kwa mwaka *return* yao isizidi milioni tano, lakini huku mtaani kuna wajasiriamali ambao wanasubiri hii fursa hata ukiwaambia *return* ya shilingi milioni moja hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi. Majukwaa haya mwasisi wake alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wa Rais aliyaanzisha mwaka 2016 yalienda yakafa. Mwaka 2022 yakazinduliwa tena, kukawekwa mpango mzuri sana. Ukiusoma ule mpango unaona kabisa majukwaa haya yanaenda kuwa mkombozi wa wanawake wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam tayari kila kata katika kata zote 102 zina makundi ya akina mama. Majukwaa haya yana uongozi, wamejisajili, wapo tayari wanasubiri fursa za mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe hili sharti la kuwa na *return* chini ya shilingi milioni tano kwa mwaka, hebu liangaliwe vizuri ili wanufaika wawe wengi. Kwa sababu haya majukwaa yapo tangu mwaka 2022. Sasa kwa vigezo kama hivyo watajikuta na fursa hii inawapita, na kwenye kila foleni ya halmashauri bado wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshajitahidi kutafuta wadau kuwapa semina, sasa inakuwa kama vile tunawadanganya na muda unazidi kwenda. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara ya Maendeleo, Jinsia na Maendeleo ya Jamii waliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiacha kundi hili, Dar es Salaam tuna Jukwaa la Wanawake Wajane. Wanawake wale wamepambana wale wachache ambao wanafanya shughuli zao ndogo ndogo za ujasiriamali, wamekubali kujitoa kwa ajili ya wenzao. Tumepata mashamba Kibiti ekari 20, lakini pa kuanzia ndiyo shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, awasaidie wanawake hawa wa Jukwaa la Wanawake Wajane wachimbiwe kisima. Wanataka kulima mboga mboga. Hawa hawana mradi, hawana biashara, wana mashamba. Wanasaidiwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi hata halmashauri zetu, kwa sababu jukwaa hili ni la wanawake wote wajane wa Wilaya ya Kinondoni, wakati tunaendelea kutafuta fursa na kuwakusanya na kuwaweka pamoja, wilaya nyingine walau hili la Kinondoni lianze ili kuwe na uhalisia, nao waone kweli inawezekana. Wana ari na wanatamani kulima mboga mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam pana hoteli nyingi, pana migahawa mingi, pana kila aina ya biashara, lakini wanawake hawa wakilima mboga mboga soko lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda ninashukuru sana, niishie hapa, mengine nitaweka kwenye maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth, ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja ajiandae.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii uliyonipatia na mimi nichangie kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaipongeza Serikali kwa kuja na mpango mahususi wa kiungwana kabisa kwa Watanzania wazalendo wa kimkakati wa kuhakikisha Taifa letu linatoka hatua moja kwenda hatua nyingine kwa kipindi cha miaka mitano. Ninaona hapa *projection* ya uchumi kwa maana ya *economic growth* kwa mwaka 2025 imekuwa kwa asilimia tano nukta sita, lakini pia tunatarajia mwaka huu inaweza ikaenda asilimia sita halafu mwakani ikaenda kama asilimia sita nukta nane au *around* hapo saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona malengo ya Wizara na malengo ya Mpango wetu ni kutengeneza uchumi imara, uchumi ambao utakuwa jumuishi, lakini pia wa kiushindani. Nianze na kwenye uchumi imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uchumi imara, hapa lazima maana yake kama Taifa tuwe na *base* ya Kitaifa ambayo itasababisha uchumi wetu kuwa *stable* katika kipindi chetu cha miaka mitano au kipindi cha miaka 25 mpaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri wangu, kama Taifa ni kweli tunatamani mambo yote yaende vizuri, sekta zote ziende vizuri, lakini ningetamani kama Taifa tuwe na vipaumbele vichache ambavyo kama tutajikita na halafu tujivunie kupitia vipaumbele hivyo kama Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kilimo. Ninashauri kama Taifa, tujikite sana kwenye kilimo kwa sababu kina tija kubwa sana kwa wananchi wetu mmoja mmoja na kwa Taifa kwa ujumla. Kwenye andiko hili inaonyesha kilimo, ndio wanaochangia sehemu kubwa ya pato la Taifa, wastani wa 20% mpaka 24%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeshauri kama Taifa tuwe na mikakati madhubuti ya kimakusudi ya kuhakikisha tunaki-*boost* kilimo ili angalau tusiwe na kilimo ambacho kinaweza kikayumba

kutokana na msimu. Maana yake hapa nashauri tuongeze mikakati ya umwagiliaji, mikakati ya uvuvi, mikakati ya kutumia vyanzo vyetu vya maji tulivyonavyo kama Taifa kuhakikisha wananchi wetu tunawahakikishia kilimo muda wote na mazao muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye kilimo hapa labda nizungumze, kwa mfano, Jimbo langu la Kasulu Vijijini tuna maeneo mengi sana ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji ambayo kama yakitumika vizuri kwa kweli wananchi wangu kwa kweli ni neema ya pekee na utakuwa umegusa maisha ya *almost* robo tatu ya wananchi wangu wa Jimbo la Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ushauri wangu kama Taifa tungewekeza msukumo mkubwa tuka-*boost* kilimo pengine kichangie hata 30% pengine mpaka 40% kwenye uchumi wetu au pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie upande wa masoko. Changamoto nyingine iliyopo kwenye kilimo, ni masoko. Kwenye mchango wangu uliopita kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais, nilishauri kwamba ikiwezekana tuitumie TEHAMA vizuri ili kutafuta masoko ya uhakika kwa wananchi wetu. Tuje na mifumo ambayo mwananchi wa vijijini, mwananchi wa mbali anaweza akaangalia Soko la Dar es Salaam linasemaje kuhusiana na mazao yake yaliyoko kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishauri kwamba ikiwezekana tuwe na mfumo *software* au *application* ambayo mwananchi aki-*click* kama ni Mchele, kama ni Pamba na kadhalika, ataona soko linasemaje hapa Dodoma, Kilimanjaro, au Babati na maeneo mengine. Vilevile, anaweza kuona mpaka nchi jirani kunasema nini kuhusiana na zao hilo kuhusiana na suala la bei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba uwepo pia mkakati wa kimakusudi wa kufungua maeneo ya vijijini, kwa maana ya barabara zipitike kwa kiwango cha changarawe, kwa kiwango cha lami. Nilikuwa ninaangalia kwenye ujenzi wa

mtandao wa lami waliojenga kwa barabara zilizoko *TANROADS* ni kama kilometa 100 na kidogo tu ambapo ukiangalia pale kwa kweli inasikitisha kama tuna makusudi kweli ya kuhakikisha kwamba tunafikia malengo yetu kwa kipindi cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusiana na upotevu wa mapato. Kama Taifa, nimeona hapa wanasifiwa watu wa *Local Government Authorities* kwamba wamechagiza sana *performance* ya ukusanyaji wa mapato, lakini kinachoendelea kwenye Serikali zetu za Mitaa pamoja na *performance* inayoonyeshwa hapa kwamba wamefanya vizuri kwa kweli kinasikitisha sana. Kinachotokea kule moja, kuna wakati kule wanajitengea bajeti ndogo yaani wanafanya *underestimation* ya vyanzo vyao vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano; kuna mahali fulani nilienda wameandika watakusanya pale milioni 50, lakini ukiangalia kile chanzo cha mapato yako mapato ya waziwazi kabisa ambayo wanaweza kukusanya mpaka milioni 150. Kwa hiyo, baadaye wakiweka ile kadirio la chini la milioni 50 wakishafikia milioni arobaini na kidogo wanajipongeza kwamba wame-*perform* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninafanya *Masters* yangu nimefanya utafiti kwenye *Local Government Authorities* hasa kwenye ukusanyaji wa mapato. Kule mapato mengi yanapotea ukilinganisha na kile ambacho tunakusanya yaani pengine inaweza ikawa ni nusu kwa nusu, yaani kinachopotea na kile tunachopata kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba, kama Serikali tujikite kwenye matumizi ya TEHAMA ya kisasa. Kwanza nipongeze kwamba *point of sales* imekuwa ikifanya vizuri, lakini baadhi ya maeneo haifanyi vizuri hasa kwenye stendi zetu. Kwa mfano stendi zile za Magufuli na stendi zingine kuna maeneo ukienda pale getini hali ni mbaya, ukienda vyooni hali ni mbaya, mtu anaingia hakuna chochote kinachokusanywa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilienda mbali nilijaribu kuuliza baadhi ya watu wanasema wanatumia *loopholes* iliyopo kwa sababu mtu anaingia au anaweza akapitisha gari getini ikiishapita gari au ikapita pikipiki hachani karatasi ile yaani ha-*print* kwa maana ile risiti ya *point* yaani *point of sales* kwa maana ya *POS* hampatii risiti ili mradi tu amepita kama ni chooni ameenda amerudi, kwa hiyo, unakuta tunapoteza mapato mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niishauri Serikali tuangalie namna ya kuziba mianya hasa kwa yale mapato tutakayokusanya kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri kuhusiana na uchumi wa ushindani. Tunavyoangalia uchumi wa ushindani lazima tujipime na wenzetu. Sasa kwa Afrika Mashariki inaonekana uchumi kwa mwaka jana 2026 ulikuwa wastani wa *5.3,* lakini uchumi wetu umekua kwa asilimia 5.6. Hapo hapo kuna mataifa mengine kama Rwanda yako saba lakini pia Uganda na yenyewe iko sita na kwa mujibu wa *IM*F inasema kwamba wakianza uzalishaji tu wa mafuta kama Uganda uchumi wao utakua mpaka kwa 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri hapa kama Taifa tuwe na mkakati wa kimakusudi tusijikute tunaburuza mkia kwa miaka mitano mingine inayokuja ukilinganisha pengine kwa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi atafuatiwa na Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, Mheshimiwa Regina Henry Mikenze, ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu. Niwapongeze Mawaziri waliotuonyesha *at least framework* ya mpango wa muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho kinanitia moyo katika mpango huu ninaona mpango huu unajali ustawi wa maisha ya Mtanzania. Ninawapongeza sana wanaendana na ndoto ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kusema tusilenge tu kwenye miundombinu, tusije tukaishia mpango wetu tunaona tu *SGR, flying overs* na majumba makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu kwa kulingana na dira unaonyesha kwamba ifikapo 2050 angalau Watanzania wawe na maisha bora na Mtanzania awe na miaka 75 akiwa na maisha yenye furaha. Tofauti na Biblia inavyosema umri wa mtu kuishi ni miaka 70, lakini tena iliyojaa tabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia hapo tunahitaji Watanzania wawe na lishe bora, wawe na huduma bora ya afya kila mtu aweze kufikia huduma bora ya afya ya matibabu, maji safi na salama, makazi mazuri, nishati safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu ya kufika hapo hata kwenye dira wametuonyesha, tu kwamba katika mikakati yote hii iliyowekwa kwenye sekta zote za kijamii na za kiuchumi kwamba Pato la Mtanzania litapanda kutoka dola za Kimarekani 1,275 mpaka 7,000, huo ni mkakati mzuri sana kama angalau tutafikia hapo. Ndipo ambapo tunaweza tukamudu kupata haya maisha bora ambayo yanasemwa kwa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivyo ili kufikia hizo ndoto za Tanzania kwenda kwenye uchumi wa kati na uchumi wa juu na pato la Mtanzania kuweza kupanda ili ajipatie maisha bora ndiyo maana tunasema uwekezaji uelekezwe kwenye sekta za kiuzalishaji, uelekezwe kwenye kilimo, uelekezwe kwenye mifugo, uelekezwe kwenye nishati, uelekezwe kwenye madini pamoja na maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuisemea kilimo ni halali kabisa pamoja na kwamba wachangiaji wengi wameisemea. Kilimo ndiyo ajira ya Watanzania; Watanzania wengi wako kwenye kilimo, zaidi ya 65% au 70%, kilimo ndiyo tunapata malighafi ya viwanda kwa 65%, kilimo kinachangia *GDP* kwa 26% mpaka 30%, kilimo ndicho tulitarajia kupata fedha za kigeni. Kwa hiyo, uwekezaji kwenye kilimo uzingatiwe kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo chetu kina namna ya kuweza kukitazama, kwanza kilimo cha Tanzania kwa sehemu kubwa kinafanywa na wakulima wadogo wadogo kwa 90%, hawa wakulima wadogo wadogo ndiyo wanaotosheleza chakula kwa zaidi ya 128%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha Tanzania katika mnyororo mzima wa thamani lazima kila hatua ufanyike uwekezaji mkubwa sana. Tumesema kwenye hatua ya uzalishaji sababu ya kuwa na uzalishaji mdogo, tumesema ni mvua zisizoaminika kwa hiyo tumeishauri Serikali izingatie kuwekeza kwenye miradi ya umwagiliaji, tumeongelea habari ya pembejeo bora Serikali iwekeze kwelikweli kwenye pembejeo bora, *affordable* na ambazo watu wanaweza ku-*access*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea habari ya huduma za ughani. Huduma za ughani ni muhimu sana hasa kwa wakulima wadogo. Tanzania tuna fursa kubwa sana ukiona duniani, kwanza sisi Tanzania idadi ya watu inaongezeka, lakini duniani tu tuna idadi ya watu inayoenda bilioni nane. Hii bilioni nane ni fursa ya kuilisha, lakini huku duniani pia watu wanao-*suffer* na njaa ni milioni 828 na huku Afrika milioni 249. Hizo zote ni fursa pengine sisi ni namna gani tunatakiwa kufikia hizo fursa za kuwalisha watu duniani na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema kilimo biashara kama kweli tunataka tusogee kwenye kilimo biashara, hatuna budi sasa hivi kuwekeza kwenye mashamba makubwa *large scale farming* pamoja na *block farming*. Serikali itafute mashamba ipime afya ya udongo iwe na hati na kila kitu halafu iwaalike wawekezaji waje wawekeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema *private* sekta kwenye mpango wetu watachangia 70% sehemu moja kubwa ambayo *private* sekta wanaweza kutusaidia ni kwenye kilimo na kama ni kwenye kilimo wafanye basi mashamba makubwa: mashamba makubwa ni yale ambayo unaweza ukafanya *mechanical agriculture*, uka-*mechanize agriculture*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba makubwa ndiyo yale ambayo tunaweza tukafikia *quality* ya vitu vinavyotakiwa kwenda nje. Haya mashamba madogo madogo ya wakulima heka moja, heka mbili, mkulima ni anajua kufanya *risk management* kwenye shamba moja ata-*intercrop* mahindi, maharage na kila zao. Haya mazao ya namna hiyo pengine kuyatoa nje tunakuwa hatujafikia ule ubora wa kimataifa. Sasa huu ubora wa kimataifa tutapata kwenye hii *large scale farming* ambapo sasa tayari sisi tufanye *lobbying* pamoja na mahusiano na nchi za nje tutangulize kupata soko ili tuwaambie hawa wazalishaji watuzalishie kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ninatamani katika vipaumbele vya mradi huu tuendelee kuviangalia viwanda. Nchi zote zilizofanya na zilizokua uchumi kwa kasi kubwa ni waliowekeza kwenye viwanda. Sisi viwanda kongani ya viwanda imekuwepo toka Baba wa Taifa, tunakumbuka tulikuwa na viwanda, tukapata sera ya ubinafsishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine tuliobinafsisha wakati ule viwanda labda hawakuwa Watanzania wazalendo sisi watu wameondoka na mashine na kila kitu kwa mfano *General Tire* kwetu unajua kiwanda kizuri kabisa katika Afrika Mashariki lakini tumebakiwa na magofu. Hata sasa sera yetu ya viwanda ni rafiki inashawishi wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuiangalie ili kukuza kongani ya viwanda. Ukiangalia soko la kwanza la viwanda vyetu vya ndani ni Watanzania wenyewe ni kwa kiasi gani Watanzania ni

wazalendo na wanapenda kutumia vitu vya nchini kwao? Ubora wa vitu vinavyozalishwa huku kwetu nani anapaswa kusimamia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine hatuna *skills* na *knowledge*, hatuna wataalam wa kutosha, viwanda vyetu vizalishe vitu ambavyo Watanzania watavipenda, lakini *affordability*. Vitu vinavyozalishwa huku ndani vinazalishwa kwa gharama kubwa, hebu turudi chini kwenye sera zetu kwa nini vitu vinavyozalishwa huku ndani vinakuwa gharama kubwa, kwa hiyo vitu hivi ni vya kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni malighafi. Viwanda vyote vilivyopo vya wawekezaji vinavyozalisha bati chuma, vioo, chumvi sukari vitu gani, sehemu kubwa ya malighafi inatoka nje mpaka viwanda vya bia. Kimea tu cha kutengeneza bia ukienda *breweries* tunaagiza kutoka nje. Tuangalie sisi Mungu alivyotubariki na fursa tulizonazo na rasilimali zetu. Sehemu kubwa ya malighafi inayotakiwa kama chuma na vingine vipatikane huku ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni *skills;* wataalam lazima tuwapeleke nje kuliko na viwanda vilivyoendelea ili warudi huku ndani waje waendeleze viwanda. Viwanda ni sehemu pekee itakayoweza ku-*absorb* nguvu kazi ya Taifa lakini sehemu pekee ambayo Watanzania wanaweza wakapata kipato cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ninaona mpango wetu uweke vipaumbele ni vichochea uchumi na hii inamaanisha miundombinu ya usafirishaji, nishati, teknolojia sayansi, mageuzi ya kidijiti pamoja na utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema miundombinu ya Barabara; barabara imekuwa kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi mahali. Hebu ona sehemu yoyote *marginalized* ambazo ziko pembeni, usafiri na usafirishaji siku zote uchumi wake umekuwa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara huko vijijini hazipitiki kabisa, barabara ni zote, hizi *feeder roads* zinazotoka kijijini kuja kwenye miji midogo haziwezi kupitika mwaka mzima. Kuna sehemu kama kipindi hiki mvua zimenyesha mawasiliano yamekwisha kabisa, mkulima kuchukua mfuko wa mbolea kama amechukua mjini kufikisha mpaka kwake ni zaidi ya 5000, hebu ona gharama kubwa ya uzalishaji, lakini amezalisha mazao yake jinsi ya kuyatoa kule kijijini na kuyaleta sokoni inakuwa tabu hata mnunuzi kufuata yale mazao ya mkulima kwenda kijijini ni shida vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, miundombinu ya barabara pengine tungekuwa na ubunifu, kwa huu Mfuko ambao unakusanya fedha kwa ajili ya *TARURA, TANROADS* tuone namna gani tupate vyanzo vingine, hela ziongezwe huku na barabara zote zipitike mwaka mzima, barabara za vijijini lakini na barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni nishati, tumebarikiwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia muda umeisha.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa hiyo, mpango uzingatie upatikanaji wa nishati kwa bei nzuri, lakini pamoja na sayansi na teknolojia na mageuzi ya kidijiti ili kwamba tuweze kwenda na mpango wetu na Dira ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina kwa mchango wako. Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Henry Mikenze, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, ajiandae.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii. kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema siku hii ya leo. Kingine nitoe pole kwa Chama Cha Mapinduzi hasa Wanatabora kwa kuondokewa na aliyekuwa Mjumbe wa Halmashauri kuu ya CCM Taifa Mzee Nassoro Hamdani na mpendwa wetu Dada Munde Tambwe, Mbunge Mstaafu, Viti Maalum, Mkoa wa Tabora, wapumzike kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wenye ulemavu kwenye Dira ya Taifa ambayo iko mezani inajadiliwa tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuweza kutujumuisha katika dira hii. Dira inaelekeza kuwa na Taifa jumuishi lenye ustawi haki na linalojitegemea. Nitajikita katika mambo mawili; uchumi imara jumuishi na shindani, lakini pia maisha bora na ustawi kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutujali sana sisi watu wenye ulemavu, si tu kutujali yaani anaonyesha utu na sisi wote ni mashahidi. Nikianza kwenye masuala ya afya, watoto chini ya miaka mitano. Ukienda kwenye *field* ya kawaida watoto wanatibiwa bure chini ya miaka mitano. Hata hivyo, ninaiomba Wizara, kuna watoto wa usonji na watoto wenye vichwa vikubwa, hawa watoto wasiishie tu miaka mitano waendelee kupata huduma mpaka pale watakapokaa sawa, nina imani hili liko ndani ya uwezo wa Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna ulemavu wa afya ya akili, hawa watu wanahitaji dawa maisha yao yote, ninaomba zitolewe bure ili kujenga jamii jumuishi kama dira inavyotuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, tunaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sisi watu wenye ulemavu kuendelea kuwa chini ya Waziri Mkuu, inamaanisha mambo yetu wenye ulemavu ni mambo mtambuka yana-*cut across* kwenye kila Wizara. Kwa hiyo, Waziri Mkuu ana uwezo wa kutoa maelekezo katika Wizara

tofauti tofauti ili kuleta maendeleo jumuishi kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii Awamu ya Sita tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kitendo cha kuboresha vyuo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu na hii ni namna ya kupambana na ajira kwa vijana wenye ulemavu. Ninaomba nivitaje hivi vyuo viko 10 vingine vimekarabatiwa na kutengenezwa, vingine vimejengwa upya chini ya Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu ambao uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo hivyo ninaomba nivitaje wananchi wavielewe ili waweze kuwapeleka vijana wao kwa ajili ya maendeleo ya vijana, kuzalisha ajira na vijana pia watajiajiri. Vyuo hivyo kuna Chuo cha Rwanzari, mkoani Tabora; Chuo kiko Milongo, Mwanza; Chuo cha Masiwani, Tanga na Mtapika, Masasi, Mtwara. Chuo cha Ufundi, hivi vya watu wenye ulemavu Sabasaba, Singida; Yombo, Dar es Salaam; Ruvuma; Mbozi, Songwe; Kasulu, Kigoma; na Kisesa, Mwanza. Hivi vyuo ni vya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara ya Elimu hili suala lichukuliwe kama *emergence*, kuna Chuo mfano kile cha Rwanzari havina mkalimani wa lugha ya alama ambapo wanafunzi wenye uziwi wanakosa mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Kwa hiyo, ninaomba tuangalie namna ya kupeleka wakalimani, hiyo Rwanzali nimetolea tu mfano kwa sababu nimekitembelea, lakini sijajua hivi vyuo vingine pia Wizara wanaweza wakachukua muda kuvitembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwenye Wizara ya Uchukuzi sisi watu wenye ulemavu ninaomba tuondoe *mentality* kwamba tunapenda kusaidiwa, hapana. Sisi tuondolewe vikwazo ili tuweze kupambana katika maendeleo, kwa sababu kuwa mwenye ulemavu hakuniondolei kwamba nitakuwa na nchi yangu peke yangu, hapana. Huduma wanazozipata watu wengine na sisi tunaenda huko huko. Kama kwenye mabasi tunapanda na sisi tunapanda huko huko, hakuna

jamii nyingine. Mfano, kuna usumbufu unaojitokeza kwa sisi watu wenye ulemavu kwenye Wizara ya Uchukuzi hasa *SGR,* vituo vya mwendo kasi, uwanja wa ndege na stendi za mabasi mfano pale kwa Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoka kusema kwamba na sisi ni wapambanaji tunachangia pato la Taifa, lakini kuna usumbufu ambao hauna hata, yaani usumbufu siyo wa lazima. Tumewekewa viti mwendo vile tumewekewa mazingira mazuri sawa mfano, pale kwenye *SGR,* lakini vile vitimwendo mimi mwenyewe ni shahidi unakaa pale nusu saa nzima saa nyingine unaletewa kitimwendo na vitimwendo vingi vimeharibika inamaanisha havifanyiwi *service*. Tunapotezewa muda katika hivi vituo. Huu ni usumbufu usio wa lazima. Ninaomba tusaidiwe kwa sababu tunapoteza muda mwingi na tunashindwa kuchangia maendeleo kama watu wengine. Tunapenda tufike kwa wakati twende katika maeneo yetu kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wenye ulemavu tunahudumiwa na ustawi wa jamii kwa ngazi ya halmashauri na hiki kitengo cha ustawi wa jamii kinahudumia si watu wenye ulemavu tu, wanahudumia wazee, watoto wa mitaani, kutatua migogoro ya ndoa, yaani mambo mengi hii Wizara imeyabeba; inapitia changamoto nyingi. Sisi wenye ulemavu changamoto zetu wao ndiyo wanazifahamu. Hawa ndiyo wanaofahamu idadi ya wenye ulemavu kuanzia ngazi ya kata mpaka kwenye wilaya mpaka mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba na kuishauri Wizara kama itapendeza iongeze idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii. Wawepo angalau kila kata, kwa sababu sasa hivi kazi ya ustawi wa jamii kwenye kata wanafanya pia Maafisa Maendeleo ya Jamii. Pia, ianzishwe Idara ya Ustawi wa Jamii kwenye kila Halmashauri. Kwa sasa muundo wa halmashauri hii ustawi wa jamii ni kitengo kiko chini ya Mganga Mkuu Wizara ya Afya kwenye ngazi ya halmashauri. Ndiyo maana tunakutana na changamoto utakuta vifaa saidizi hatuna, mafuta ya wenye ualbino hayatoshi kwa sababu hawana bajeti maalum ambayo inayowawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba iwe idara katika ngazi ya halmashauri na ngazi ya mkoa. Itasaidia sana kutatua changamoto zetu wenye ulemavu na hii kama ikishindikana basi wazo la pili ni kwamba bajeti ya ustawi wa jamii kwa upande wa watu wenye ulemavu basi ipelekwe kwenye Wizara inayohusu watu wenye ulemavu ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Wenye Ulemavu ili mambo yetu yaweze kutatulika kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninahitimisha kwa kusema kwamba ukimpa mtu chakula kila siku. Leo umempa chakula na kesho unampa chakula, huyu unamtengeneza awe tegemezi maisha yake yote. Tukumbuke sisi watu wenye ulemavu kwenye sensa ya hivi karibuni tuko zaidi ya milioni tano ni sawa na 11.2% ya Watanzania wote. Kwa hiyo, tuangalie tusipoweka mikakati madhubuti ya kuondoa vikwazo kwa hili kundi la watu wenye ulemavu tunatengeneza Taifa kubwa ambalo ni tegemezi na tunavyoangalia kwamba dira yetu inasema tutengeneze jamii jumuishi na yenye kujitegemea. Kwa hiyo, ndugu zangu, Wizara hizi ziwasiliane juu ya namna ya kuondoa vikwazo ili tusitengeneze Taifa tegemezi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Regina Henry Mikenze, atafuatiwa na Mheshimiwa Thomas Kampala na Mheshimiwa Saidi Salim Hamad ajiandae.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia. Nami kama ilivyo ada kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili Tukufu nianze kwa kumshukuru Mungu aliyeniwezesha kupata nafasi hii adhimu ya kuwa mwakilishi wa wanawake wa Mkoa wa Geita. Ninamshukuru sana Mungu kwa sababu aliijua siku hii kabla ya kufanyika misingi ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais, yeye ndiye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Ninaamini kwa

baraka zake alipokuwa akisimamia vikao na teuzi zote aliweza kulipitisha jina langu, ninamshukuru kwa dhati ya moyo wangu. Pia, ninawashukuru Wanawake wa Mkoa wa Geita walionichagua kwa kishindo na kunifanya leo kuwa mwakilishi wao. Ninawashukuru sana na ninawaahidi kwamba nitawatumikia kwa moyo wangu wote na kwa akili zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie pia kwa kuishukuru familia yangu. Wamekuwa wakini-*support* kwa hali na mali, wameniombea wamenitia moyo. Kwa hiyo, sina budi kuwashukuru na ninasema ahsante sana na mimi nipo kwa ajili yao sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninapoelekea katika kuchangia ninaomba niwaelekeze katika suala moja la elimu ya amali. Elimu ya Amali ni jambo ambalo ni geni. Limeletwa kwetu katika huu mtaala mpya ambao umeboreshwa, lakini jambo hili likifanyika kwa jinsi ambavyo limeratibiwa litakwenda kuleta matokeo makubwa sana katika Nchi yetu ya Tanzania. Kwa nini litakwenda kuleta matokeo makubwa katika Nchi ya Tanzania? Kwa sababu itakwenda kugusa vijana wengi wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea ninaomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa mwasisi wa kwanza na ndiye aliyetoa agizo kwamba mtaala uliokuwepo ufanyiwe marekebisho na uwekwe mtaala ambao utatoa elimu ya amali ili vijana wengi wa Kitanzania na wananchi kwa ujumla waweze kupata mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa agizo hilo alipokuwa akihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021 na leo tunaona hata tunapokuja kujadili dira lakini Mheshimiwa Rais alikuwa na maono ya mbele. Aliliona jambo hili mapema hata kabla hatujatengeza dira hii ya muda mrefu wa 2026 mpaka 2050. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais. Tunatambua mchango wake na maono yake kwa vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakubaliana kwamba taifa lolote ambalo halishirikishi vijana haliwezi kufanikiwa na kama tumeamua kuwa na uchumi jumuishi ni lazima tuhakikishe tunakwenda na vijana wetu. Sasa mtaala huu umelenga kuhakikisha watoto wanaosoma elimu ya sekondari wanaanza kupata elimu ya mafunzo na hivyo mtoto anapomaliza kidato cha nne anaweza akajiajiri au akaajiriwa endapo atakuwa amechagua mkondo wa amali. Kwa hiyo, hili ni suala muhimu sana na ambalo litakwenda kutupatia maendeleo katika Taifa letu na litakwenda kutatua changamoto ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Mheshimiwa Rais alipoiagiza Wizara ya Elimu, imetekeleza na imekwishaanza kutekeleza mtaala huu kwa kupitia vyuo vya ufundi vya *VETA*. Mkakati uliopo, Wizara ya Elimu inakwenda kujenga vyuo vya *VETA* kwa kila wilaya. Sasa kama tunakwenda kupata vyuo vya *VETA* katika wilaya, ninaamini huu utakuwa ni mwarobaini wa kutatua changamoto ya ajira kwa watoto wetu na watoto wetu wanakwenda kujiajiri na wanakwenda kupata fursa mbalimbali zikiwemo fursa za ujasiriamali, viwanda na fursa mbalimbali za ajira kwa sababu hata katika mafunzo wapo ambao wanaajiriwa na wanaajirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakubaliana kwamba mfumo wetu wa elimu ulikua ni mfumo ambao ulikuwa umekaa katika eneo la pembetatu *(pyramid)*. Watoto wengi walikuwa wakianza huku chini wanaanza wengi, lakini inaenda inawachuja. Huyu amefaulu anaingia sekondari, huyu anachujwa tena anaingia *form five na six,* anachujwa tena anaingia chuo kikuu, lakini mfumo huu unakwenda kuwajumuisha na kuwapa fursa watoto wote wa Kitanzania na watoto hawa watakapopata elimu na mafunzo haya hatutamwacha mtoto nyuma hata mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivi tunakwenda kukomesha matatizo ya dawa za kulevya, tunakwenda kukomesha changamoto za watoto kutumia mitandao ya kijamii vibaya kwa sababu watoto wetu watakuwa *busy,* watakuwa

wameji-*keep busy* katika kufanya shughuli mbalimbali za mikono na ambazo zinawapatia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kutoa mchango wangu kwa mambo machache ambayo ninaishauri Serikali iyaangalie ili kuweza kufanikisha mpango huu muhimu sana ambao utatusaidia kuendeleza na kuleta matokeo makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niombe Serikali iweke bajeti ya kutosha ili kuhakikisha kwamba shule za *VETA* zinajengwa kama walivyotuahidi katika kila wilaya nchi nzima. Kwa hiyo, litengwe fungu, lakini pia tuhakikishe kwamba tunapata walimu wa kutosha na walimu walio wabobevu. Kwa hiyo, Serikali itunze pesa za kutosha ili tupate walimu ambao watatusaidia kuwekeza ujuzi unaohitajika kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, niombe kwamba watoto hawa wanakwenda kumaliza kwa wingi sana. Ikiwa kila wilaya itapata shule ya *VETA* tutakuwa na watoto wengi sana wanaomaliza kwa muda mfupi. Tusipoweka mikakati madhubuti ya kuwawezesha kuwapatia mitaji muda siyo mrefu tutapa tena janga lingine la vijana kuwa mtaani wana ujuzi lakini hawana mitaji. Kwa hiyo, niombe Serikali iweke pia bajeti ili kuwasaidia vijana hawa wanaomaliza katika elimu hizi za mafunzo ya amali waweze kupata mitaji na waweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuishauri Serikali ni kwamba mafunzo haya yatolewe kwa kujali mahitaji ya kieneo, kwa mfano, ninatoka katika Mkoa wa Geita. Kule tuna wachimbaji, wakulima, na wafugaji. Sasa tunapoweka *VETA* pale katika Mkoa wetu wa Geita, nishauri tuangalie *course* ambazo zitasaidia kuleta manufaa katika eneo husika katika kila wilaya. Kwa mfano, pale Geita tuna Mgodi mkubwa wa *GGM* ambao unatoa fursa za ajira nyingi. Kwa hiyo, Chuo cha *VETA* kitakachokuwa katika mkoa wetu pale na katika wilaya yetu kihakikishe kwamba kinawatengeneza vijana kwa kuangalia mahitaji yanayohitajika au *course* zinazohitajika katika mgodi ili vijana waweze kujiajiri katika mgodi huo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa malizia muda wako umeisha.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwapongeza Wizara ya Elimu kwa utekelezaji mkubwa wa elimu hii ya amali na niwaombe waitangaze fursa hii ya chuo cha *VETA* kwa wananchi. *VETA* imekuwa ikidharaulika kwamba ni elimu ambayo inachukuliwa na watu ambao hawakufaulu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu waitambue na waweze kujiunga na elimu ya *VETA*. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimemwita Mheshimiwa Thomas Kampala atafuatiwa na Mheshimiwa Saidi Salim Hamad na Mheshimiwa Asha Salum Motto ajiandae.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweke mchango wangu kwenye hoja mahususi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa letu. Kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri, kaka yangu Profesa Alexander Kitila Mkumbo, kwa wasilisho zuri, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha naye kwa andiko zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika hakuna Taifa duniani liliwahi kuendelea bila kuwa na mpango. Mzee wangu Profesa Muhongo amechangia vizuri sana mchana hapa; ametupitisha tulikuwa wapi, tumetoka wapi, tumefika wapi na wapi tulianguka na akatoa suluhisho la tutanyanyukaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango huu ninataka nijielekeze moja kwa moja kwenye kilimo. Ni ukweli usiopingika

kilimo ndicho kinaajiri Watanzania wengi nchi hii. 70% ya Watanzania wameajiriwa kwenye kilimo. Ni lazima Serikali ichukue hatua za makusudi kuwekeza kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndiyo njia pekee ya kutusaidia kuweka mazingira mazuri ya kusababisha vijana wengi wanaotoka vijijini wasitoke vijijini kukimbilia mjini. Tukiwekeza vizuri kwenye kilimo na vijana wengi vijijini wakavutika na kilimo, mjini kutapunguza wimbi kubwa la vijana ambao hawana ajira. Niwaombe sana, kaka yangu Profesa Kitila Mkumbo ninamshukuru na ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameanza kwa mfano kuwekeza kwenye kilimo. Ni lazima Serikali iamue kwa makusudi kufanya *proper investment* kwenye *irrigation schemes. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Jimbo la Katavi tuna maeneo 13 ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji na imefanyika *study,* wamekuja watu wa kilimo wamefanya *study* na wakathibitisha kuwa kweli yanafaa. Ninamwomba Waziri atakapokuja wakati anafanya majumuisho atueleze ana mpango gani kwenye eneo la kilimo. Ameeleza vizuri kabisa, Mpango huu unaokwenda unakwenda kubadilisha kilimo kutoka kwenye kilimo cha kujikimu kuja kwenye kilimo cha biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana naye, sisi Katavi tuna zao la tumbaku ambalo linafanya vizuri. Leo hii ninavyoongea mwaka jana wakulima wa tumbaku wa Jimbo Katavi wamelima kwa kiwango kikubwa na wamepata fedha nyingi sana wakahamasika kulima. Hivi ninavyoongea wakulima wa tumbaku wa Jimbo la Katavi wamejipanga kulima badala yake imekuja *notice* kwenye vyama vya ushirika wapunguze kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo tunajipanga kwenda kwenye kilimo cha biashara, wakati huo huo wakulima wetu wanakatishwa tamaa, tunakwenda wapi? Niiombe Serikali sisi Katavi wale wakulima wanalima na ile tumbaku tutalima tutavuna. Wasipotengeneza mpango mzuri wajipange watwambie ile tumbaku wataikoroga *juice. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo na mpango wowote ni lazima ujielekeze kwenye miundombinu. Nimeongea mara nyingi na nimeongea na Waziri wa Ujenzi kuhusu Barabara inayotoka Inyonga – Majimoto – Kibaoni – Sumbawanga – Tunduma – Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni ya kimkakati. Barabara hii ni fupi, ambayo itarahisisha Wakazi wa Mkoa wa Mara, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Tabora wanaotaka kwenda Zambia kuliko kupita njia ndefu, ambayo itawalazimisha watoke Mwanza, waje Shinyanga, waje Tabora, waende Singida, waje Dodoma, waende Iringa, waitafute Mbeya kwenda Tunduma mpaka Zambia; badala yake barabara hii ikitengenezwa vizuri mkazi wa Mkoa wa Mwanza atatoka Mwanza – Shinyanga – Tabora, Tabora atakata Sikonge, Sikonge anaingia Inyonga, anaingia Majimoto – Sumbawanga – Tunduma – Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini faida yake? Faida yake ni itawapunguzia wananchi safari ndefu na mlolongo wa safari, ili kwenda Zambia, kwa ajili ya kujiletea maendeleo. Tutapunguza urefu wa safari na wananchi wetu watatumia muda mfupi, kwa ajili ya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichangie tena upande wa *VETA*. Kama ambavyo wenzangu wamechangia, *VETA* ni suluhisho pekee litakalowasaidia vijana ambao hawakusoma na waliosoma ili kujipatia ajira. Wakati ambapo sikuwa Mbunge niliwahi kumsikiliza Mbunge mmoja amechangia hapa, alisema mitaala ya *VETA* ibadilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna mafundi simu, mafundi wa gereji, mafundi wa pikipiki na kila kada ina maeneo yake. Wale watu wengi kule hawakusoma, lakini wakipata mafunzo mazuri ya *VETA,* wakakusanywa vizuri, wale wote watakuwa na *certificate* ambazo zitawawezesha kwenda mahali na ku-*apply* kazi wakapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba, tunalo tatizo hapa, kama ambavyo nimesema mwanzo, hakuna nchi ambayo

inakwenda bila mpango. Amechangia jana kaka yangu, Mheshimiwa King, akasema tunapopitisha mpango huu ni vizuri tukaweka na Sheria. Usipoweka Sheria maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata tatizo, alifariki Rais wetu mpendwa, Dkt. John Pombe Magufuli akaingia Mama Samia Suluhu Hassan, isingekuwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ana utashi akakuta hii miradi mikubwa, mama huyu angekuwa ni mvivu, akaacha miradi hii leo tusingekuwa tunaongelea *SGR* imeanza, leo tusingekuwa tunaongelea Bwawa la Mwalimu Nyerere limeanza, leo tusingekuwa tunaongelea Kigongo Busisi. Haiwezekani miaka yote tunayokwenda tukapata Rais kama Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, atakuja kutokea Rais hapa, wametengeneza mpango hauna sheria na kuna miradi mikubwa kama hii iliyokuwepo, anaamua kuacha anaanzisha ya kwake. Watambana na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana na ninaiomba Serikali yangu, mawazo haya yanayotolewa na Wabunge ni vizuri yakazingatiwa. Kama ambavyo ukirudi kwenye *Hansard* kule kuna michango mizuri iliwahi kutolewa na Wabunge wakati tunatengeneza *BRT Phase 1*. Wapo Wabunge waliwahi kuchangia wakasema na wakashauri kuwa, hapa tunapotengeneza, tunapopitisha Jangwani hapa hapafai kuweka *terminal* panatakiwa kuwekwa daraja, lakini watu hawakusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasipokuwa na mpango watakuwa wanakwenda na kurudi. Badala yake sasa leo Jangwani tunajenga Daraja, kwa nini? Hatukusikiliza ushauri na hatukuwa na mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saidi Salim Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Salum Motto na Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali ajiandae.

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kuwa kunijaalia miongoni mwa watu ambao wako katika nyumba hii takatifu. Aidha, kwa vile ni mara yangu ya kwanza ninapenda kuchukua nafasi hii kukishukuru kwa dhati ya moyo wangu Chama changu Cha Mapinduzi kuanzia ngazi ya Jimbo, Wilaya, Mkoa; ngazi ya Ofisi Kuu Kisiwandui, pamoja na Kamati Kuu ya CCM Taifa, chini ya Mwenyekiti wake mahiri, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Dkt. Samia kwa ushindi wa kishindo alioupata tarehe 29 Oktoba, 2025. Baada ya shukrani hiyo, ninaomba nichangie hoja iliyopo Mezani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu nitajikita kwenye mambo makuu mawili. Mambo haya yataelekea kwenye *implementation* ya bajeti yetu hii ambayo iko mezani kwa Mwaka 2026/2027. Jambo la kwanza, ili tuweze kufanikiwa katika bajeti yetu hii wachangiaji tumechangia tufanye *investment* kubwa kwenye masuala mazima ya kilimo, biashara na madini. Kwa uono wangu, ninapenda niongeze sehemu nyingine ya *investment* kubwa ambayo tunapaswa kuwekeza, ni katika vijana wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sensa vijana ni *more than 75%,* lakini rika la watoto baada ya miaka miwili au mitatu nao wana-*turn* kutoka kwenye *childhood* wanakuja katika rika la vijana, *so in general* vijana wanachukua namba kubwa ya watu katika Taifa hili. Tukiweza kuwekeza katika sekta hizi zinazowahusu vijana tutaweza kuchangia pato la nchi hii na kuchangia katika bajeti yetu hii kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuwekeza kwa vijana kupitia elimu, habari, teknolojia na michezo. Kupitia elimu vijana tunawasomesha masomo ya *physics*, *biology*, *chemistry*, *history* na masomo mengine mbalimbali, lakini kuna wimbi kubwa la vijana akili zao zimekita sana katika masuala ya michezo. Ninaishauri Serikali tuanze kuwekeza kupitia *sports academies*.

Michezo sasa hivi ni biashara kubwa sana na tayari inachangia mapato makubwa katika mataifa ambayo yameendelea kwa kuajiri wachezaji wa mipira na michezo mbalimbali duniani na kuweza kupata mapato mbalimbali katika Taifa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, iwapo tutaanzisha hizi *sports academies* kuanzia ngazi za watoto hadi vijana, vijana wetu wengi wataweza kujiajiri na kuajiriwa kupitia hii sekta ya michezo. Hata hivyo, tunapaswa kuwekeza kuanzia kwenye shina. *It means* tuajiri walimu *professional,* kwa ajili ya michezo, ambao wataweza kusomesha watoto kuanzia ngazi za *nursery*, *primary*, *secondary* na hata ngazi za vyuo vikuu kuwe kuna *syllabus* kabisa ya kusomesha haya masuala ya michezo, ili tupunguze wimbi kubwa la vijana ambao hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo litatuwezesha kupata fedha zaidi katika zoezi letu hili la bajeti ambalo tunakwenda nalo sasa hivi ni kupitia habari. Tumemwona Mheshimiwa Waziri Makonda, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenga shilingi bilioni mbili kuwawezesha *content creators*, hii ni ajira kubwa sana kwa vijana. Kama tutaweza kuwa-*facilitate* vizuri, Mama kaleta hizi shilingi bilioni mbili zikiweza kutumiwa *very effectively* basi zitakuza kipato cha vijana wetu kutoka hatua moja kwenda nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hili ninashauri kwa vile tuna benki mbalimbali hapa kwenye nchi yetu, tuna benki ya kilimo tumeianzisha. Kwa nini tusianzishe benki ya maendeleo ya vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili hizi fedha ambazo zimetengwa, shilingi bilioni mbili, kupitia Wizara ya Habari, *first* ziwe *deposited* pale kwenye benki yetu, kwa ajili ya vijana. Tumesikia Mheshimiwa Rais kupitia Waziri wetu wa Vijana ambapo katuwekea Mheshimiwa Nanauka pale, katenga shilingi bilioni 200, kwa ajili ya kuwawezesha vijana. Kwa nini fedha hizi zisiwe *first deposited* kupitia benki yetu maalum ya vijana, ili vijana waweze kwenda kutumia fedha hizi katika sehemu zao maalum na wakitaka mikopo, wakitaka kuwa-*facilitated* kwenye mambo yao mbalimbali vijana hawa waweze kwenda kuchukua pale kwenye benki yetu hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kupitia maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ili tuweze kukuza uchumi wetu na kuweza kupata fedha ambazo zitasababisha bajeti yetu kukua siku hadi siku na uchumi wetu kupanda, kama ilivyo nchi yetu uchumi wake unakua kwa kasi zaidi na tunawekeza pesa nyingi kupitia sekta ya ujenzi, uchukuzi na miundombinu. Hapa Serikali kwa mwaka tuna-*allocate billions of money* ambazo zinaenda kujenga miradi mbalimbali katika Taifa letu, lakini katika fedha hizi ambazo zinaenda kuwekwa pale tunaenda kukuza uchumi wetu *at the same time* tuna-*facilitate* uchumi wa nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapo-*compete* kampuni za *international* na kampuni zetu *local* tunashindwa kushindana na kampuni zile zinazokuja kutoka nje ya nchi kwa sababu kuu tatu; kampuni zinazokuja kutoka nje ya nchi zinatushinda *technical*, *financial* na *working experience*. Zikija tukikaa nazo mezani, tuki-*bid* nazo pamoja, hizi kampuni za ujenzi na kujenga miundombinu mbalimbali zinashinda zile tenda. *At the same time* tunatumia fedha, *billions of money* ambazo Mheshimiwa Samia ana-*allocate* kupitia Wizara hizi kujenga miundombinu ya nchi yetu, lakini tunakwenda kuchochea uchumi wa nchi nyingine kwa sababu, zile kampuni zinapopata tenda ndani ya nchi yetu zina-*take profit from these tenders and then* wanaenda kujenga kwenye mataifa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa ninaishauri Serikali, ili tupate fedha hizi ziweze kukuza uchumi wetu, lakini vilevile iwe ni sababu ya ku-*facilitate* ukuaji wa maendeleo kwa jamii yetu. Tutengeneze mazingira rafiki kwa kampuni zetu za ndani ziweze ku-*compete* kuanzia *internally* mpaka *externally*. *It means* hapa, kama Serikali, tutatenga fedha tuzi-*fund* hizi kampuni. Kama tutakaweka Sheria fulani, *let's say* imekuja kampuni kubwa kutoka China, imekuja kujenga *flyover* hapa, tukaweka Sheria kupitia kampuni hii ambayo imekuja, basi ifanye *joint venture* na kampuni yetu *local.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweke Sheria kama hii, kazi *total* ni shilingi bilioni 200, lakini *you must give sub-contract from a local*

*company,* ili kupitia *sub-contract* hii ambayo itapewa hii *local company* kuna mambo tutaweza kuya-*gain*. Tutaweza ku-*gain experience from international company,* lakini ile kampuni yetu ambayo ni *local, instead* ya kukaa bila kuipata ile kazi kubwa itakuwa nayo imepata kazi; itaweza kuajiri vijana mbalimbali na hawa *Gen-Z* ambao wako mtaani ambao wanamnyima usingizi Mama Samia, mama anapenda kuwaona vijana wake wamepata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili apate usingizi mnono basi ni lazima tuwezeshe kampuni zetu za ndani, mama aweze kulala aone vijana wake wote wamepata ajira kupitia kampuni hizi za ujenzi ambazo zinakuja kufanya miradi mbalimbali. Tutapata *experience* na ile *key personnel*, wale *technical staff* ambao tuponao wakishirikiana na *technical staff* kutoka kampuni kubwa watajenga *technics* ambazo wanazitumia ku-*complete* hizo *project* kubwakubwa na mambo mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kuchangia kwangu katika hoja hii kwa kusema maneno matakatifu kutoka katika Vitabu Vitakatifu. Ninaanza kunukuu kutoka Kitabu Kitakatifu; Ayubu 42:2 anasema; "Ninajua ya kuwa, wewe waweza kufanya mambo yote na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuiliwa." Kwenye Qurani kuna maandiko yanasema, "*Qaddara Allahu wamaa shaa fa'ala.*" Vilevile, kuna aya inasema; "*Innama amruhu idha araada Shay'an an yaquula lahu kun faya kun.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Watanzania wamwachie mama afanye kazi. Mama yupo kazini amesimamishwa kwa kadari ya Mwenyezi Mungu na hawezi kutetereka isipokuwa kwa kadari ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saidi Salim Hamad, ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Asha Salum Motto, atafuatiwa

na Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali na Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe ajiandae.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele kuchangia Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa 2026/2027. Mpango uliokuwa na dhima kubwa ya kuinua uchumi wa Nchi yetu ya Tanzania na kutimiza maono ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, ninasimama kwa mara ya kwanza, ninaungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia uzima na afya kufika siku ya leo. Pia, ninatumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuniamini mimi Asha Salum Motto kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la Kumi na Tatu, 2025 - 2030. Aidha, ninawapongeza viongozi wote waliopo ndani ya Bunge hili tukiongozwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu ninatumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Mtwara, hasa wanawake, kwa kuniamini mimi kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu. Pia, ninatumia fursa hii kuwashukuru viongozi wote wa Chama Cha Mapinduzi na wa Serikali pia, kwa kuwa pamoja na mimi kipindi chote tulichokuwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi wa kishindo wa takribani 97%. Haikuwa bahati mbaya kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kushinda, watu waliona kazi alizozifanya kwa miaka yake yote minne. Hakuna mradi ambao ulisimama, shule ziliendelea kujengwa, vituo vya afya viliongezeka kwa hiyo, hakupata zile kura kwa bahati mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitomshukuru Mwenyekiti wangu wa UWT Taifa, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda. Mama huyu ni mtu na nusu, amekuwa akimsaidia sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kutuunganisha sisi wanawake wa Tanzania, hususan wanawake wa Mkoa wa Mtwara. Unaweza ukaona ni namna gani Bunge hili la Kumi na Tatu asilimia ya wanawake imeongezeka. Hii ni kazi kubwa ya hamasa aliyoifanya Mheshimiwa Mary Pius Chatanda kutuhamasisha sisi wanawake, kutuweka pamoja na kutujengea uwezo wa kutokuogopa kugombea nafasi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijielekeze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Sekta ya Nishati. Kama inavyofahamika, Mikoa ya Kusini sisi ni matajiri; Lindi, Mtwara na Ruvuma ni matajri wa gesi na makaa ya mawe. Jukumu letu kubwa ni faida zinazopatikana na miradi hiyo zianze kwanza kufaidiwa na Wazawa wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti za Kituo cha Lindi na Mtwara zimebaini uwepo wa gesi asilia takribani 32%, mbali na ule Mradi wa *TPDC-Mtwara*. *TPDC-Mtwara* inafanya kazi kubwa ya kusambaza mtandao wa gesi majumbani na mpaka sasa kwa takwimu iliyopo imesambaza kati ya kaya 491,811. Mkoa wa Mtwara una kaya 491,811, kaya 373,172 ziko vijijini, sawa na 75.9% na kaya 118,639 sawa na 24.1% ziko mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TPDC* linaloendelea kutekeleza miradi ya usambazaji wa gesi asilia nchini hadi sasa imesambaza kaya 428, ukiangalia tofauti bado idadi ya kaya zilizobaki kufikiwa na mradi huo ni nyingi, ninaishauri Serikali kuongeza nguvu ili mtandao huu wa mabomba ya gesi uweze kufika kwenye kaya nyingi zaidi na kufikia malengo ili wananchi wa Mkoa wa Mtwara waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuona pia *TPDC* imefanikiwa kusambaza mtandao wa gesi katika taasisi nne (4) kati ya taasisi 108. Hii inaonesha kwamba bado kasi ni ndogo ya mradi huu, kwa hiyo wajitahidi ili taasisi zilizobaki na zenyewe ziweze kufanikiwa. Ukiangalia taasisi hizi ziko mjini, nasi ukiangalia

kaya nyingi zinatoka vijijini, kwa hiyo *TPDC* na Wizara husika wajitahidi wahakikishe na wale wa vijijini wananufaika na mradi huu kwa kuwa tumeshaona gesi inatoka Mtwara inaenda Dar es Salaam, inatoka Dar es Salaam inaenda na mikoa mingine, ukiangalia takwimu ya *TPDC* unaona kabisa labda mikoa ile mingine ina asilimia kubwa ya kaya walizopata hii gesi kuliko mkoa wenyewe ambao ndiyo tunazalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa *CNG*, hii ni gesi asilia iliyoshindiliwa. Hapa nchini kwa sasa kuna vituo 14 vinavyouza gesi kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya usafiri wa magari na bajaji. Mkoa wa Mtwara una kituo kimoja tu ambacho kipo maeneo ya Dangote na hiki ni kituo cha Dangote kwa shughuli yake ya kusafirisha saruji yake, wananchi wa Mkoa wa Mtwara hawanufaiki na hiki kituo. Kwa hiyo ninaiomba Serikali ione haja ya kwenda kuwekeza kituo ambacho kitawasaidia wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Kusini kwa ujumla kubadilisha mfumo wa magari kutoka kwenye *diesel* au *petrol* kutumia gesi ambapo pia itawasaidia kupunguza gharama ambazo wanazitumia sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya idadi ndogo ya kaya zilizounganishwa na gesi asilia majumbani hapa Mkoa wa Mtwara. Ninashauri Serikali kuongeza kasi ya uunganishaji wa kaya hizo pamoja na kuboresha miundombinu ya usambazaji wa mabomba ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kusini hasa Mkoa wa Ruvuma kuna makaa ya mawe, makaa ya mawe haya yanatoka Ruvuma yanakuja bandari ya Mtwara, tuna *depot* ambayo ipo kulekule bandarini na Bandari ya Mtwara iko mjini, athari tunayoipata Mtwara kwa makaa ya mawe kwa kweli ni kubwa sana na sijui kizazi kijacho itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujenga bandari kubwa kule Mgao, bandari iliyogharimu takribani shilingi bilioni 434 na bandari hii itakuwa ya kisasa na ya kwanza kwa ukubwa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana muda wako umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi ajiandae.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipatia nafasi hiyo ili niwe miongoni mwa wachangiaji. Nianze kabisa kwa kuwapongeza Wana-CCM wote kwa maadhimisho ya miaka 49 ya kuzaliwa, tuna kila sababu ya kuwapongeza. Pia ninapongeza Wizara zote za Mipango na Uwekezaji pamoja na Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambayo wamefanya kutuletea ripoti hii, hakika endapo Watanzania tutaifanyia kazi vizuri hiyo, taswira ya Tanzania huko ifikapo itabadilika kabisa Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kupongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan. Sekta ya Nishati, nina kila sababu ya kumpongeza Waziri husika kwa sababu sasa anaenda kusaini mkataba ambao unatuletea umeme katika vitongoji. Tanzania ya leo kwa uongozi shupavu wa Mama Samia tayari vijiji vyote tumeshawasha umeme. Sasa, taarifa rasmi kama Mbunge wa Ilongero, ninaomba kuwajulisha wananchi wangu kwamba nyumba 11,654 sasa katika vitongoji wanaenda kupata umeme kwa shilingi 27,000. Nina kila sababu ya kujivunia kwamba mimi ni Mwana-CCM na Rais wetu ni Mwana-CCM na anachapa kazi kwa vitendo tumeona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kwetu watu wengi wanahusika na kilimo na ufugaji, kwa hiyo ninazungumzia Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo kwetu tuna bwawa ambalo Serikali inatujengea mpakani mwa jimboni kwetu na Manyara ambako ni kwako pia. Wananchi watanufaika na umwagiliaji wa bwawa hili kwa sababu yenye thamani ya shilingi bilioni 17 imetuletea Serikali ya Awamu ya Sita, nina kila sababu ya kuwashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida tayari tuna neema, tunalo bwawa ambalo hakuna haja ya kujenga, tumepewa ruzuku na Mwenyezi Mungu, tumeshushiwa kutoka mbinguni, yako zaidi ya nane. Serikali haiwezi kuingia gharama ya mabilioni ya fedha endapo yatatumika mabwawa hayo yaliyojaa na maji na samaki pia kama walinzi watalinda. Kuunganisha tu umwagiliaji ili wananchi wakulima na wafugaji waweze kunufaika na hilo, hilo kwa kweli katika mpango kazi liangaliwe vizuri litatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo katika Sekta ya Kilimo, tuliahidiwa na Serikali kwamba tutakuja kupata soko la vitunguu ambalo ipo nafasi imetengwa nafasi katika Kata ya Merya, fedha shilingi bilioni 2.9 ilitengwa na ilipitishwa, tuko mbioni kukamilisha na Wizara tumeshawasilisha mikataba ambayo walitushauri wao, kilichobakia wao wakamilishe na waweze kutufikishia ili kazi ianze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza sana na tumesikia kilio cha wananchi, kilio cha wananchi ni soko la dengu. Soko la dengu asilimia kubwa soko la hilo zao inasafirishwa kwenda India, lakini wakulima wanalia, Wabunge wanalia wanasema kwamba soko hili linakuwaje. Hivi kweli tunaweza tukaamini kwamba nchini India Wahindi wameacha kula dengu? Ni vitu ambavyo haviingii akilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba urasimu uliopo wa kodi ndiyo kinachotuumiza. Tukiondoa urasimu huo, hizo dengu, changamoto hizo zipo na Jimboni kwako nisemee wananchi wako pia, tunamaliza mara moja. Hilo ni zao, hiyo siyo almasi, hilo ni zao, hiyo siyo dhahabu, zao linaoza almasi haiozi, ikinyeshewa mvua inaharibika. Hivi sasa wakulima wetu hawalimi tena, wanalipia maghala wamehifadhi. Kwa hiyo, Wizara iweze kuangalia upya utaratibu huo wa hizo tozo ili wananchi wetu waweze kunufaika na waweze kuuza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia upande wa mifugo, Wizara ina aina mbili ya ufugaji, kuna wale ambao ni wafugaji na kuna wale ambao ni wachungaji. Kuna wale ambao wanafuga mifugo na kuna wale ambao wanachunga mifugo. Sasa hawa

wanaochunga mifugo ndiyo unaona kwamba matatizo yanatokea kati ya hawa wafugaji ambao ni wachungaji na wakulima, kwa sababu mifugo hiyo wachungaji wanaiswaga, inatembea *kilometres*, inaenda mbali, ikirudi inakuwa imeshaharibu mashamba ya wakulima na hapo ndipo tatizo linapoanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ifike mahali ambapo kwa makusudi kabisa Wizara husika iweze kubadilisha hawa sasa wachungaji waingie katika ufugaji wa kwelikweli. Ufugaji ni pale ambapo unafuga hiyo, unaenda shambani kwako, unaweka malisho yao unawaletea pale walipo ili wanenepe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia upande wa *private sector*. *Private sector* imekidhi wafanyabiashara, nikizungumzia wafanyabiashara, ninaomba sana wahusika waangalie kwa jicho la huruma. Kuna wafanyabiashara ambao wajasiriamali, kuna wafanyabiashara ambao ni wadogodogo sana, ambao labda wanauza matunda, wanauza mboga aina mbalimbali, wanauza mihogo, hizo zinawafanya wapate kipato chao na maisha yao yaweze kuendelea. Sasa ifike mahali Serikali kwa makusudi iweze kutangaza kwamba atakayemnyanyasa au atakayempakia katika gari yoyote huyo anayeuza bidhaa zake ili aweze kujipatia kipato chake, iwe *criminal offence*, ninadhani hata Waziri Mkuu katika ziara yake alishawahi kukemea sehemu nyingi sana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *private sector*, sasa hivi mfanyabiashara akitaka kutoka nje, akitaka kwenda popote pale, anaambiwa kwamba anaruhusiwa kusafiri na dola 10,000 tu, lakini sheria inawabana hata wale wanaokuja kutoka nchi za nje, unawaambia kwamba sasa hauruhusiwi kuja na zaidi ya dola 10,000. Hii sheria ibadilike, wahusika hii sheria ibadilike. Mtu anakuletea fedha, anakuletea neema, anakuja kununua bidhaa zake hapa Tanzania, unamwekea kikomo kwamba asije na zaidi ya dola 10,000! Yaani wewe mwenyewe ndiyo unakuwa chanzo cha kuondoa na kuweka tuta katika ukusanyaji wa mapato yako. Hivyo ni vitu ambavyo haviingii akilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dola ni kitu gani? Dola siyo dawa za kulevya, ifike mahali ambapo wafanyabiashara waliopo mipakani, waruhusiwe kupokea dola na kupeleka benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Dubai leo, kwa miaka yote hiyo thamani ya dola utakuta 3.55, 3.66 haizidi hapa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Malizia Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naam?
**MWENYEKITI:** Malizia muda wako umekwisha.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tukumbushane, Bunge linapogeuzwa na kuwa Kamati ya Mipango au Kamati ya Matumizi, basi anayesimamia hapa atambulike kama Mwenyekiti, nadhani tumeelewana. *(Makofi)*
Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, atafuatiwa na Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, ajiandae.

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii kuweza kuongea ndani ya Bunge hili Tukufu kwa mara yangu ya kwanza nikisimama hapa kama Mbunge wa Viti Maalum kupitia kundi la wafanyakazi kutokea Mkoa wa Mjini Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sana kuwashukuru Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa wa UWT ukiongoza na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Taifa UWT, Mama Mary Pius Chatanda. Wajumbe hawa walisababisha mimi kuonekana na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na

Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuniteua na kuniamini kuona ninaweza kuungana na Wabunge kupitia Bunge hili la Kumi na Tatu ili niweze kuwawakilisha wanawake wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sana pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi wake wa kishindo wa 97% kupitia Chama Cha Mapinduzi. Pia ninapenda kumpongeza Spika ambaye yuko ndani ya Bunge hili pamoja nawe Naibu Spika pamoja na Wenyeviti, Waheshimiwa Wabunge wote waliomo ndani ya Bunge hili kwa ushindi wa kishindo mlioupata na kuhakikisha mmeteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Dkt. Emmanuel Nchimbi, Msaidizi wa Mama Samia Suluhu Hassan, Msaidizi wa Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu ambaye aliteuliwa na kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mtendaji Mkuu wa Serikali. Ninawapongeza pia Mawaziri na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote ambao wanamsaidia Rais katika kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa upekee kabisa, ninapenda kuwapongeza sana Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ambaye aliwasilisha Mpango Elekezi wa Maendeleo wa muda mrefu, muda wa kati na Mpango pia wa mwaka 2026/2027. Pia, ninapenda kumpongeza kaka yangu Khamis Mussa, Waziri wa Fedha naye aliwasilisha Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2026/2027 – 2028/2029. Ninapenda sana kupongeza kwa weledi waliotumia katika kuwasilisha mpango huu pamoja na bajeti hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uwasilishaji wa mwongozo huo pamoja na bajeti hiyo, ninaomba kujielekeza katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni sekta ya utalii ambapo kwenye sekta ya utalii tumeona imeendelea kuwa nguzo muhimu kwa uchumi wa Taifa na kuchangia 27% ya pato la Taifa kwa mwaka 2024. Mafanikio makubwa hayo, yametokana na ongezeko kubwa la idadi ya watalii kutoka watalii milioni 1.8 mwaka 2023 na kufikia

milioni 2.14 kwa mwaka 2024. Mapato pia kuongezeka kutoka dola za Kimarekani bilioni 3.37 kwa mwaka 2023 na hadi kufikia bilioni 3.9 kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha sekta ya utalii ina nafasi kubwa ya kuendeleza uchumi wa Taifa kufikia malengo ya muda mrefu. Kamati pia ya Bajeti imechambua shabaha mbalimbali na ikapendekeza Serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara na viwanja vidogo vya ndege katika maeneo yenye vivutio vya utalii na kurahisisha usafiri wa watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapenda kumpongeza sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa makusudi kabisa na kwa uthubutu wake mkubwa, aliamua kutengeneza filamu ya *"The Royal Tour"* katika kuongeza, kuinua uchumi wa Nchi hii ya Tanzania kutokana na sekta hiyo ya utalii. Pia ninaomba kumpongeza Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi ambaye alikuwa bega kwa bega katika kumtia moyo na kumwongezea nguvu Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutengeneza filamu hii ya *'The Royal Tour'*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona viongozi hawa waliitengeneza filamu hii, Dkt. Samia aliitengeneza filamu hii akiwa ardhini, akiwa angani, akiwa baharini kwa kushirikiana na Dkt. Hussein Mwinyi ambapo nilifurahi sana nilipowaona wakiwa baharini, walifikia hatua ya kuvutia kivutio hiki cha utalii kwa kuvua samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemwona daktari huyu uthubutu wake ulivyo mkubwa, walimtoa samaki kwenye maji wakamleta juu; ni Rais wa pekee ambaye alifanya tukio hilo, mimi sijawahi kuona. Tumpongeze sana Daktari Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema nini katika eneo hili? Katika eneo hili ninaendelea kusisitiza kwamba, Serikali ihakikishe utekelezaji wa mikakati wa kukuza na kuhamasisha aina mbalimbali za utalii ikiwemo utalii wa picha, michezo, matibabu, mikutano, fukwe za bahari, utamaduni na urithi wa kihistoria ambao haujatumika ipasavyo. Vilevile, jumuishi za hifadhi na

wanyamapori ziendelee kuimarishwa ili kuongeza thamani ya vivutio vya utalii. Hatua hizi zitasaidia kuongeza idadi ya watalii, mapato ya kigeni na mchango wa sekta ya utalii katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalotaka kuligusa ni la wakandarasi wazabuni pamoja na watoa huduma. Tumeona katika uwasilishwaji wa mpango huu umeguswa uimarishaji wa mifumo ya kidigitali. Sasa hapa katika uwasilishwaji nimeona changamoto moja kubwa inayoikabili Serikali; ni malimbikizo ya madeni ya wakandarasi; wazabuni na watoa huduma. Changamoto hizi zinatokana na mambo kadhaa ikiwemo ucheleweshaji na uhakiki wa madai, ukosefu wa fedha za kutokana na mapato ya ndani yasiyo thabiti pamoja na urasimu katika utaratibu wa malipo. Hali hii imekuwa ikidhoofisha uwezo wa wakandarasi na wazabuni kuendelea kutoa huduma bora na wakati mwingine kusababisha kusimama kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sikusimama tu kwa miradi ya maendeleo; tumeona vijana wetu wengi wamekuwa wakipata ajira kwenye eneo hili. Wazabuni na wakandarasi wanapofanya kazi basi wao wanakuwa msaada mkubwa wa kutoa ajira kuisaidia pia Serikali kuwapa vijana wetu ajira. Pale tunapokosa kuwalipa kwa wakati; kumbuka wanajaribu kulipa, wanalipa, lakini mwisho wa siku na wao wanashindwa kuwafanyia malipo vijana. Vijana wanalalamika huko mitaani. Wanapolalamika mitaani inasababisha kuonekana kuwa tatizo kubwa ni kiongozi wa juu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kwenye upande huu kwanza mifumo ya uhakiki wa madai iimarishwe katika teknolojia ya kidigitali ili kupunguza urasimu na kuongeza uwazi; Serikali ihakikishe kuwa bajeti ya miradi zinatengwa kwa uhalisia na fedha za kutosha

zinapatikana kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo; kuwe na utaratibu wa kipaumbele katika malipo ambapo wakandarasi na watoa huduma wanahusika na miradi ya mkakati ya kijamii watalipwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera na Mheshimiwa Johannes Lukumay ajiandae.

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nipate fursa ya kuchangia kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa letu. Jambo la kwanza, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha kuwa sehemu ya Bunge hili Tukufu, Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimshukuru sana Dkt. Samia chini ya uongozi wake ndani ya chama kwa kuona kuwa nami ninafaa kuwa sehemu ya kuwakilisha Wananyamagana kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Mwisho na kwa umuhimu niwashukuru sana wananchi wakazi wa Jimbo la Nyamagana kwa namna ambavyo alinipa imani na hata wanavyoendelea kushirikiana na mimi. Kwa wanavyonitia moyo inanipa faraja ya kusonga mbele katika kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo; Mpango wote huu ambao umewasilishwa kwetu na Wizara ya Mipango pamoja na Wizara ya Fedha; tunafahamu kuwa chini ya uongozi wa Wizara hii ya Profesa Mkumbo amefanya kazi nzuri sana; na katika hili ninampongeza. Wizara ya Fedha pia imejikita katika kutuandalia mambo ambayo kwa kweli kama yatatekelezwa basi tutegemee kuona uchumi wa Taifa letu unapaa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wabunge mtakubaliana nami, kwamba mpango huu tunaouzungumza

unahitaji fedha, ndipo tutapowagusa Watanzania, hususan kundi la vijana. Nimejaribu kupitia mpango huu takriban kila ukurasa kijana wa Kitanzania ameguswa. Ajira ambazo tunazungumza kwenda kuzitengeneza ni ajira kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufanikiwa kuufanikisha mpango huu ni lazima tuwe na fedha. Katika hili ninaomba nishauri katika maeneo makubwa matatu. Kwa sababu ninatoka kwenye kanda ya ziwa kwenye Jimbo la Nyamagana, wananchi wa Jimbo la Nyamagana walinituma nije niseme hapa, niishauri Serikali. Kwa muda mrefu sana kwa *nature* ya Mkoa wetu wa Mwanza tunao uwanja wetu wa ndege, ambao kama ungeweza kukamilishwa kujengwa na kupewa hadhi ya kimataifa, ninataka niwahakikishie, Serikali yetu na Taifa letu litapata fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiutazama uwanja wetu huu wa Mwanza, kutoka Mwanza kwenda Serengeti si zaidi ya kilometa 140 peke yake; lakini Uwanja wetu huu wa Ndege wa Mwanza ndiyo uwanja nambari moja unaoongoza kwa kusafirisha dhahabu kutoka kwenye Taifa letu. Uwanja huu unahudumia kanda ya ziwa yote. Hii inaonesha ni kwa namna gani kukamilishwa kupewa hadhi ya uwanja huu kuwa wa kimataifa uchumi wa Jiji letu la Mwanza na Taifa kwa ujumla utapaa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niishauri Serikali kwamba, mwaka juzi ilisaini mkataba kwa zaidi ya bilioni 29, lakini cha kusikitisha mkandarasi sasa kwa taarifa nilizonazo na kwa macho yangu tayari anaondoa vifaa *site,* maana yake hakuna matumaini. Wanamwanza wanauhitaji sana uwanja huu kwa ukuaji wa uchumi wao. Niwahakikishie uwanja huu ukikamilika na ukiwa wa kimataifa tunakwenda kutengeneza ajira nyingi sana kwa vijana wakazi wa Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili uwanja huu tukiupa kipaumbele Taifa letu litakwenda kuongeza fedha za kigeni kutokana na watalii tutakaowapata. Kwa kuonesha msisitizo, wakati Serikali inatangaza mpango wa kuupa hadhi Uwanja wetu

huu wa Kimataifa wa Mwanza wenzetu wa Shirika la *NSSF* walikuja kuweza. Tunayo hoteli pale eneo la Kapri Point ambapo Serikali ya Tanzania imelaza zaidi ya bilioni 90. Mtu pekee aliyekuwa amelengwa kulala kwenye hiyo hoteli ya zaidi ya bilioni 90 alikuwa ni mtalii, tukiamini kwamba uwanja ukikamilika watalii wengi watapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo fedha ya Serikali zaidi ya bilioni 90 imelala pale na Wanamwanza hawayaoni matumaini ambayo wangetamani wayapate. Kwa hiyo, ninaomba nishauri Serikali iweke jitihada za haraka kwamba kwenye mpango huu wa mwaka mmoja wa miaka mitano na miaka ishirini na tano iliyosalia tuhakikishe kuwa jambo hili tunalibeba kama la dharura kwa sababu tutapata fedha ambazo zitakuza Uchumi na zaidi ya yote tutatengeneza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Shirika letu la Ndege la *Air* Tanzania. Mapato linayoyapata kwa mwaka zaidi ya 75% yanazalishwa na Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Ni namna gani Serikali inaweza ikaonesha *commitment* ya kwamba hata kwa namna ambavyo shirika letu la ndege; maana bila Mwanza nina hakika haliwezi kujiendesha; kwa sababu kama ni 75% tafsiri yake ni kwamba *Air Tanzania* ipo kwa ajili ya Mwanza kabla ya kuwaza kwingine kokote kwa sababu ndipo mapato hasa yanakotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye sekta nyingine ya uvuvi. Mkoa wetu wa Mwanza na Jimbo la Nyamagana Mungu ametupa neema ya kipekee sana. Tunalo ziwa ambalo hawajapewa kwingine kokote kule. Ukiangalia ziwa hili kama Serikali hatujalitumia ipasavyo. Miaka ya 2000 wataalam wetu walikaa chini wakawaza wakaleta samaki aina ya sangara akaja akapandikizwa. Kulitokea mfumuko mkubwa sana wa ujenzi wa viwanda vya Samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza Mwanza tumebaki na viwanda saba peke yake. Kupitia viwanda vile tulitengeneza ajira, pia Serikali ilipata fedha na wananchi mmoja mmoja uchumi wao ulikuwa sana. Mimi ni shuhuda kwa sababu

niko pale mjini. Wapo watu maarufu ambao wana majina ya samaki, samaki ambao walikuwa wanatoka ndani ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niiombe Serikali kwa msisitizo mkubwa sana. Serikali yetu kwa mipango ambayo nimeisoma kwenye mpango huu, kama ikiamua kwa dhati, ikaamua kutekeleza kama ambavyo imejielekeza basi Ziwa letu Victoria linaweza likawanufaisha Watanzania wengi na tukatengeneza ajira kwa vijana wetu walioko ndani ya Mkoa wa Mwanza na Jiji letu la Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili, ninataka niiombe Serikali, kwamba tuondokane na uvuvi huu wa kizamani. Uvuvi haramu unaofanyika kule ndiyo umesababisha kupotea viwanda zaidi ya 16 kwa sababu ya kukosa malighafi ya samaki. Serikali ni lazima ije na mpango mkakati wa kuhakikisha inawaza ni kwa namna gani tunakwenda kufanya *transformation* kwenye sekta ya uvuvi ili tutengeneze ajira tupate fedha za kigeni; na zaidi ya yote Taifa letu la Tanzania lipate fedha za kutosha, fedha ambazo zitatengeneza miradi mingi ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande kingine ambacho ningependa nichangie ni kuhusu barabara. Mpango huu uliowasilishwa na Profesa Kitila Mkumbo ni wa kisayansi sana, lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa, muda umekwisha.

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia; kwa sababu ya muda; Dkt. Samia Suluhu Hassan popote alipo atembee kifua mbele kwa sababu kazi nzuri ameifanya. Miradi inatekelezwa kule kwetu Mwanza, barabara zinajengwa. Katika yote, ninaomba nimhakikishie kwamba Wanamwanza wanamuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay, Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel ajiandae.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia katika mpango huu. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri na maandalizi mazuri ya hizi nyenzo kwa ajili ya kuenda kutekeleza Dira ya 2050. Nimshukuru pia Waziri wa Fedha naye kwa mipango mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa, ninaanza kwa kuipongeza Serikali; tayari imekwishakuja na hizi nyenzo kama tatu kwa ajili ya utekelezaji wa Dira yetu ya 2050, ambapo Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Maendeleo wa Miaka Ishirini wa Tano una dhima kwamba tunataka kuwa na Taifa ambalo lina uchumi jumuishi na Taifa linalojitegemea; ambapo kipato chake cha mtu mmoja mmoja kitakuwa dola 7,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuweza kuyafanya hayo inaonekana Wizara pamoja na Tume ya Mipango wamefanya kazi nzuri ya kufanya mapitio ya mipango ile mitatu iliyokuwepo kwa ajili ya Dira ya 2025 na wamebaini baadhi ya changamoto ambazo zilipelekea baadhi ya malengo kutokuweza kutimia. Moja ya hizo changamoto inaoneka ni kwamba kulikuwa na matumizi machache ya sayansi teknolojia na ubunifu, pia uzalishaji mdogo viwandani na kilimo pia kilichangia kwa kiasi kidogo; pia kulikuwa na tatizo la kutokuwepo na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa vile tunataka kwenda kwenye Taifa ambalo linajitegemea kuna mambo mengi mazuri. Pia ilikuwa inaonekana kwamba kulikuwa na upungufu wa fedha katika kutekeleza baadhi ya mambo ambayo walikuwa wamepanga kuyafanya. Pamoja na hayo mafanikio yapo, lakini hatukufanikiwa kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi mazuri kabisa ambayo yako kwenye mipango na yameelekezwa. Changamoto inayokuja ni kwamba tunatakiwa tujitahidi sana kufanya kazi *business as usual* ili tutekeleze hayo ambayo tumeyaandika humu ili ndoto yetu iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizuri ni kwamba pia wamekwenda kujifunza kwenye zile nchi ambazo ziko *upper middle-income countries,* nchi zenye uchumi wa kati hadhi ya juu na tayari wameona ni nini walichofanya mpaka wakafanikiwa. Kwa hiyo, kama Taifa ni lazima na sisi tuzingatie hizo *core values* ambazo tummeziona na pia ni lazima tuzingatie misingi waliyokuwa nayo na zile *drivers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna mengi tunakokwenda; moja ya mambo ambayo tunaya-*aspire* ni kwamba tunataka tuwe na Taifa la watu ambao ni *educated* na *learned.* Nitajikita tu kwenye suala la elimu, kwa sababu ili tuweze kufanikiwa kwa kweli ni lazima tuwekeze sana kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba hata bajeti sasa itaongezeka, kutoka trilioni 7.31 hadi 8.19, lakini ninadhani bado inabidi kwa kweli tuongeze Bajeti ya Wizara ya Elimu. Hii ni kwa sababu mambo yote haya tunayokwenda kuyafanya wananchi lazima waelimishwe. Kuna ujuzi mbalimbali ambazo unatakiwa, hivyo ni lazima wananchi wasome waweze kuelimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kuwa na Taifa linalojitegemea tunaangalia; tangu mwaka 1974 wakati wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alielekeza; alikuwa na falsafa ya elimu ya kujitegemea ambapo hatukuweza kuwa nyenzo nzuri za kuweza kulitekeleza hilo hadi miaka ya 51 hapa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuja kuelekeza Wizara ya Elimu kupitia mitaala na ile mihtasari pamoja na maboresho ya sera na kuja na suala la elimu ya amali. Hii inaonekana itakuwa suluhisho katika kuchangia kuongeza pato la Taifa, lakini wananchi wa Tanzania kuweza kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi Profesa Mhongo amesema asubuhi kuhusu namna watakavyokwenda kupata fedha. Ukiangalia kwenye suala la *VETA;* ametoa mfano wa kujifunza kwa Nchi za China na India. China kwa mfano wao kwa mwaka watu milioni 13 wanaingia kwenye shule hizi za *vocations,* na watu milioni 10 wana-*graduate*. Katika watu ambao sasa hivi wanakwenda kwenye kuchangia katika ajira kwenye viwanda na mijini wengi wao, zaidi ya 70% China wanatoka kwenye hizi *vocations.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tanzania kwa sasa ninachoweza kushauri kwamba kwenye Wizara ya Elimu hivi vyuo vya *VETA* ambavyo vipo kwa kweli awamu ya kwanza tumeshajenga bado kuna awamu ya pili; na ukitaka kuwa na elimu ya kujitegemea ni lazima ufanye *practical* zaidi. Kwa hiyo, tunatakiwa Tume ya Mipango kushirikiana na Wizara ya Elimu na Wizara ya Fedha tuwekeze fedha nyingi ili tuweze kukamilisha hivi vyuo. Vikamilike kwa hadhi ambayo inatakiwa pia tusomeshe watu wengi kwenye masuala haya ya *vocations.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana pia; nimeona wakati wanafanya *review* kulikuwa na matumizi kidogo ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Sasa tufanye kitu ambacho nadhani Tume ya Mipango iliwahi kusema *ruleless prioritization.* Ni lazima tuamue kwa makusudi kipaumbele kwamba, tuwekeze zaidi kwanza katika kuelimisha watu ili baadaye hawa watu ndiyo waje wachangie katika sekta nyingine hizo za nchi yetu ili kuweza kuleta mabadiliko. Kwa hiyo, ninashauri sana kwamba, tuwekeze huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *VETA* hizi bado ni chache, tunatakiwa tuongeze idadi ya *VETA,* pia tuongeze *programs* nyingi na shule za sekondari za amali; tunamshukuru pia Mheshimiwa Rais; zimejengwa sasa hivi 103, lakini ninadhani bado zinahitajika; awamu ya kwanza ndiyo imekamilika. Ili tuwe na watu ambao watapata ujuzi unaohitajika ni lazima wafanye *practical* za kutosha. Kwa hiyo, tunaomba fedha ziongezwe tena Wizara ya Elimu ili kusudi awamu ya pili ya ujenzi wa hizo shule za

amali uweze kuendelea. Karakana zikamilike ili kweli watu watakapotoka kwenye mfumo huo wa amali basi wawe na ujuzi mbalimbali ambao unahitajika. kwa hiyo, nilipenda nichangie hiyo kwenye sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende zaidi tena mpaka kwenye vyuo. Tunamshukuru pia Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye mradi wake ule wa elimu ya juu kwa mageuzi, tuna kampasi kila mkoa. Tuzitumie zile *campuses* vizuri kwa ajili ya ujuzi mbalimbali katika *particular areas* huko zilipo hizo kampasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona China kwa mfano wamejenga *VETA* kwa kushirikiana na *Local Governments* za huko. Kwa hiyo, hata hapa kwetu tuangalie, zile halmashauri ambazo zina uchumi mzuri basi Wizara ya Elimu au Tume ya Mipango iweze kushauri huko kwenye hizo halmashauri basi waanzishe hizo *VETA* kwa ajili ya kupata ujuzi unaohitajika kwenye hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija harakaharaka kwenye Sekta ya Afya kwa sababu tunataka tuwe na Taifa la watu ambao wana afya ya kutosha, ukiangalia kwenye Sekta ya Afya asilimia kubwa ya Watanzania wanatibiwa kwenye afya ngazi ya msingi. Kwa mfano 97% ya akinamama mwaka 2024 waliohudhuria kliniki walipata huduma katika vituo vilivyo chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Vilevile, 93% waliojifungua Tanzania hapa walipata huduma hiyo kwenye vituo vya afya, lakini idadi kubwa ya akinamama zaidi ya 75% ya waliofanyiwa upasuaji kwa ajili ya kujifungua walifanya pia kwenye vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunakwenda kwenye suala la Bima ya Afya kwa Wote, lakini bado tuna-*operate* kwenye Sera ya Mwaka 2007. Ninadhani ile Sera nayo inabidi ifanyiwe mapitio kwa haraka kwa sababu kuna mabadiliko makubwa sana tangu ilipoanza mwaka 2007 mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa fedha nao lazima uangalie. Hili suala lisiwe suala la Wizara moja, liwe ni suala la Kisekta. Ili tuweze kufanikiwa pia, ushauri wangu katika kutekeleza

hii mipango ni lazima Wizara zikubali sasa kwamba tunakwenda kufanya kazi Kisekta zaidi badala ya kufanya kazi Kiwizara. Kwa sababu Wizara moja ikifanikiwa wakati Wizara nyingine hazijafanikiwa haina maana yoyote ile, lazima tushirikiane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, tukishirikiana hata mgawanyo wa fedha utakwenda kule ambako fedha zinahitajika kwa wakati muafaka. Kwa hiyo, hayo yalikuwa ni mawazo ambayo nilikuwa ninashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano fedha, labda ifikie mahali tuweke sheria au *formula* kabisa kwamba fedha lazima ziende kule ambako ndiko watu wanakozihitaji na wanakozitumia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine walipofanya *review* ilionekana kwamba kulikuwa na *poor linkage* kati ya *Vocational Education* au *Academic* na *industries*. Sasa, tunashukuru Wizara ya Elimu tayari wamekuja na Mpango wa *Industry Advisory Committee*. Ninadhani hii tui-*emulate* kwenye maeneo yote ili tuweze kuhakikisha kwamba watu wetu wanakwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye viwanda tuweke pia mwongozo au kanuni ya kuwabana hawa watu ili wawe wanakubali *internship*, kwa sababu wakishaenda kule ndipo ambapo tayari ubunifu utafanyika na baadaye tunaweza kusoma kiteknolojia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa malizia.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay, atafuatiwa na Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel na Mheshimiwa Dkt. Neema Majule ajiandae.

**MHE. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kuridhia mimi kusimama hapa leo. Ninachukua pia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupendekeza jina langu Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, Halmashauri Kuu ya Taifa na hatimaye kwenda kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Arumeru Magharibi kwa kumchagua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, ninawashukuru wananchi hao kwa kuwachagua Madiwani wote wa Jimbo la Arumeru Magharibi kuwa Madiwani wa Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi hawa wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi ninawashukuru sana kwa imani kubwa waliyonayo kwangu wakanichagua kwa kura nyingi sana kuwa Mbunge wao wa Jimbo la Arumeru Magharibi. Wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi ninawahakikishia imani waliyonipa sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika shukrani, ninapenda pia kuchukua nafasi hii kuishukuru sana familia yangu hususan mke wangu kwa kipindi chote cha harakati kuhakikisha kwamba yupo na mimi katika masuala mengi hususan kuniombea Mwenyezi Mungu, ilikuwa siyo rahisi. Mama ninakushukuru sana kwa jitihada zako na ninakuombea na wewe Mungu aendelee kukulinda na kuweza kwenda kuona matunda ambayo wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi wataenda kuyapata kupitia uwakilishi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sina fadhila nisiposhukuru uwekezaji mkubwa ambao Serikali ya Awamu ya Sita imewekeza katika Jimbo la Arumeru Magharibi. Zaidi ya shilingi bilioni 69.9 ziliwekezwa katika Jimbo la Arumeru Magharibi, ikilenga kwenda kushughulikia changamoto za afya, elimu (elimu sekondari na

elimu msingi), nishati (umeme) na miundombinu ya barabara. Ninajua bado tuna changamoto kubwa katika Jimbo la Arumeru Magharibi ikiwemo changamoto ya miundombiunu ya barabara, changamoto ya miundombinu ya maji na Sekta ya Umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchagua kwa umakini wasaidizi wake ambao waliendelea kufanya kazi kubwa sana. Tukianza na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamshukuru ametembelea na nimemweleza mambo mengi katika Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni alitembelea Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. Yule ni Waziri wetu wa Afya na amezindua, siyo tu bima ya afya lakini mpango au Programu ya Ongea na Waziri wa Afya, yaani Mtanzania wa kawaida unaongea na Waziri anakujibu pale pale. Ile itaenda kutusaidia katika suala la Bima ya Afya kwa Wote, watu wataelezea matatizo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwona Mheshimiwa Reuben Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI alikuja, lakini pia kuna Mheshimiwa Ulega, Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI aliyeko upande wa ujenzi. Hawa Waheshimiwa wote walipokuja niliwaeleza changamoto za Jimbo la Arumeru Magharibi na wamesema wataenda kufanyia kazi. Ninamshukuru sana sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa umakini na upendo kwa watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nichangie Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kama ilivyowasilishwa. Mpango unaelekeza kuchukua hatua 10. Kwa sababu ya muda nitachangia kidogo, kidogo sana hatua ya nne na kama utaridhia ninaomba ninukuu. Inasema hivi: "Kutokana na muda ..." ninarudia tena kunukuu. Inasema hivi; "Kulenga kuwa na kituo kinara cha Utalii wa Tiba ambacho kitaboresha ubora wa maisha

ya Watanzania wote na kitakuwa na sekta ya afya kama *engine* muhimu ya maendeleo na uchambuzi wa Kimataifa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili haya yatokee sasa, kutekeleza hii hatua ya nne Taifa liwekeze katika huduma ya kinga kuliko kuwekeza katika huduma ya tiba. Uwekezaji wa kutosha kwenye huduma za kinga una manufaa makubwa sana katika Taifa. Kinga inasaidia kupunguza gharama kubwa ya tiba. Kinga inasaidia kufanya Taifa kuwa lenye nguvu kwa sababu watu wanakuwa wanafanya kazi. Tunakuwa tuna uwezo mkubwa kushiriki shughuli za kiuchumi hususan uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinga inasaidia pia hata ile tiba kuwa rahisi, kwa sababu watakaokuwa wanaugua ni wachache. Kwa hiyo, watu wanapata huduma nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende sehemu ya pili kwenye hilo. Kuna utoaji wa huduma nchini na mgawanyiko wa rasilimali. Vituo vya kutolea huduma Tanzania hii ni vituo 13,774. Hiyo inajumuisha maabara binafsi na kliniki mbalimbali, lakini kati ya hizo, vituo vya kutolea huduma (zahanati, vituo vya afya na hospitali) ngazi mbalimbali vinafika 10,588. Kati ya hizo tena, vituo 7,689 sawa na 85% ziko chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa *(Primary Health Care)* na hizi ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ni TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mgawanyo wa rasilimali kama alivyoelezea ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mahera hapa, fedha nyingi zinabaki katika sehemu ya uratibu. Wale watu wengi ambao tumesema ni 73% wanapata sehemu kidogo. Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kuangalia namna ya kugawa rasilimali hizi kwa kufuata *formula.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendeeza labda tutumie *formula* ya Mfuko wa Pamoja ambao tunasema kwamba ni *Basket Fund* ambao unaweza ukasaidia kugawa rasilimali hizi hususan rasilimali fedha, ili wale wananchi wengi walioko vijijini waweze kupata huduma bora za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumalizia kwamba, tukiwekeza kwenye kinga hususan suala la chanjo, suala la uchunguzi tunaita *Screening* ambayo inasaidia kutambua magonjwa kabla hayajafika mbali au kwa hatua za mwanzo ambazo zinaweza zikapata tiba zinaweza kusaidia kuimarisha maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo ninaomba kusema kwamba ninaunga mkono hoja. Mungu ibariki Tanzania na Mungu libariki Jimbo la Arumeru Magharibi. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay. Nilimtaja Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Neema Majule na Mheshimiwa Benjamin Ngayiwa ajiandae.

**MHE. MAGRETH B. EZEKIEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuanza kwa kutoa shukrani ya dhati kwa ajili ya kupewa nafasi hii adhimu ya kuchangia maoni na ushauri kwenye Mpango wa Maendeleo wa Serikali, Dira ya Maendeleo *2020 – 2050, Long Term Perspective Plan* pamoja na *the Fourth and Fifth-Year Development Plan*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii adhimu kwa unyenyekevu na moyo wa shukrani wa dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa uhai, pumzi na fursa ya kusimama katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na kwa moyo wa shukrani na upendo, ninapenda kumshukuru mama yangu kipenzi changu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuniteua na kunipa dhamana ya kuwa Mbunge wa Viti Maalum nikiwakilisha mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kuwemo Bungeni miaka 24 niliyonayo ni ushuhuda tosha kwamba Mheshimiwa Rais ana mapenzi makubwa na sisi vijana. Pia, kwa nafasi hii ninaomba vijana wote watumie nafasi yangu humu Bungeni kama ushuhuda kwamba tuna nafasi kubwa ya kuchangia maendeleo ya Taifa letu la Tanzania na kwamba tuna Serikali sikivu inayotupa sikio la kutusikiliza na kutuwezesha katika yote tunayoyafikiri katika kulijenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi pia kumshukuru na kumpongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa uadilifu, kwa nguvu zake zote na kwa wivu mkubwa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Waziri Mkuu na Baraza zima la Mawaziri kwa kazi nzuri wanayofanya. Nimefanya utafiti wa kuwatembelea na kuwasalimia Mawaziri zaidi ya 70% na wote wameonyesha utashi wa kutaka kuwasaidia vijana kwa nguvu zao zote. Katika Mawaziri hawa, 40% ya Mawaziri walioteuliwa ni vijana. Kwa hiyo, dhahiri inaonyesha kuwa katika kila hatua Mheshimiwa Rais ameweka jitihada ya kutuinua, ya kutuwezesha na kutujengea uwezo, akijua kwamba kesho ya Taifa letu ipo chini ya mikono yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa ninapenda kuwashukuru wanawake wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wakiongozwa na mama yangu kipenzi Mary Pius Chatanda. Wanawake hawa ninawashukuru kwa kunilea kisiasa, kunibariki, kunikopesha imani na kunipa kura nyingi. Ninaahidi mbele ya Bunge lako Tukufu na Watanzania kiujumla kuwa nitalitumikia Taifa kwa juhudi kubwa, kwa uadilifu, moyo wa dhati na wivu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini dhahiri, uzalendo mkubwa ni kulitumikia Taifa kuhakikisha amani na uchumi endelevu. Taifa hili linajengwa na mimi, Taifa hili linajengwa na wewe na Taifa hili linajengwa na sisi sote Watanzania na katika

udongo huu tuliozaliwa ndiyo udongo huu tutakaozikwa na siku moja kuwarithisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa shukrani na unyenyekevu mkubwa ninapenda kuwashukuru wanawake wote wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuonesha wazi na dhahiri kwamba sisi wanawake tuna nafasi kubwa ya kuendelea kutenda kwa maadili mema, kwa uthubutu, na kuendeleza kuwalea mabinti na wanawake wengine katika nafasi za uongozi tukielewa kwamba kuwepo kwetu sisi inaleta chachu ya maendeleo kwa Taifa kiujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia nichukue fursa hii kutuma salamu za shukrani ya dhati kwa baba yangu Baraka Ezekiel kwa kuthibitisha kuwa uchimbaji ni kitu ambacho kinaweza kurithishwa na ni biashara kama biashara nyingine. Nimezaliwa kwenye familia ya uchimbaji, vile mnavyoniona, elimu yangu, afya yangu, mimi kuwepo humu Bungeni vyote vimechangiwa na rasilimali zilizotokana na madini na Sekta ya Madini kiujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kutuma shukrani nyingi za upendo kwa wachimbaji wote Tanzania kwa kunilea na hususan wachimbaji vijana milioni nne walionipa dhamana ya kuwa Mwenyekiti wao katika Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa kuna mambo machache yaliyozungumzwa nami ningependa kuyachangia. Ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuweka umakini na umuhimu kwa vipengele mbalimbali katika Sekta ya Madini ikiwa kwamba katika Bunge hili nimekuwa nikisikiliza mawasilisho mbalimbali na katika kila Wabunge 10 wanaosimama basi Wabunge sita au Wabunge wanne wanasimama kuiongelea Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Madini ni uti wa mgongo, ni kitovu, ni moyo wa uchumi wa nchi yetu. Ninaipongeza sana Wizara ya Mipango kwa sababu wameweka katika *flagship projects* zao, wameweka *Dodoma Central Minerals and*

*Innovations Hub*. Hii *Central Mineral and Innovation Hub* italeta chachu ya kufanya tafiti na uangalizi kwamba ni namna gani madini yanaweza kutunufaisha sisi, pale ambapo tunalenga kupata uchumi wa shilingi trilioni moja ifikapo mwaka 2050. Hatuwezi kufikia uchumi wa shilingi trilioni moja kama hatutatumia rasilimali zetu za madini kiukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea suala zima la *National Sovereignty Wealth Fund*, nilikuwa Saudi Februari ya mwaka uliopita na nimeona jinsi gani *Sovereignty Wealth Fund* zao zimefanikiwa. Leo Saudi inatoka kwenye mafuta inaenda kwenye viwanda, inaenda kwenye kutengeneza betri na magari, na kwenye uchumi mwingine wezeshi. Hii yote inatokana na uwekezaji kwenye *Sovereignty Wealth Fund*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *issue* ya Liganga na Mchuchuma; hakuna sekta itakayoendelea, si Sekta ya Viwanda, si sekta yoyote wezeshi ya uchumi bila chuma. Chuma ni kitu pekee ambacho kinaweza kukutengenezea viwanda zaidi ya 1,000 hadi 2,000. Hivyo, ninapongeza sana *Liganga and Mchuchuma Iron Complex Centre*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaenda kwenye mada maalum na mada ambayo inatulenga sisi vijana. Dira ya maendeleo ya sisi vijana, mfano mimi Magreth leo nina miaka 24, inamaanisha miaka 25 nitakuwa na miaka 50. Kwa hiyo, ninapaswa katika miaka 25 yangu nielekeze nguvu zangu, akili yangu na rasilimali zangu katika kuhoji. Je, katika mpango wa maendeleo nina nafasi gani ya ku-*play*? Kwa sababu tunapoangalia sasa hivi kwenye dunia tumeingia katika vita kubwa ya uchumi na vita kubwa ya teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaongelea suala zima la *Artificial Intelligence*. Sasa, *Artificial Intelligence* tunaongelea kazi ambazo zinafanywa na binadamu kwa sasa hivi, ndani ya miaka mitano, ndani ya miaka 10 na ndani ya miaka 20 zitakuwa zinafanywa na *robots*. Mpaka sasa hivi Kampuni ya Elon Musk imetangaza *by 2027* unaweza ukanunua *your own human robot* kwa dola za Kimarekani 75,000. Je, vijana hawa ambao sasa hivi

tunaenda kusema tunawapa ajira tumewaandaa vipi katika *global market competitiveness in Artificial Intelligence*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunaongelea mtu kwenda kupambana na *robot,* huwezi kupambana na roboti, huwezi kupambana na *AI*. *So* katika *dividend* ambayo tunaiongelea *(demographic dividend)* inaenda kuwa *demographic bomb*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *demographic bomb* ni kwa sababu gani? Kwa sababu kuna vijana wengi ambao wanategemea ajira. Ajira nyingi zilikuwa kwenye kilimo lakini sasa hivi vijana wengi hawataki kilimo kila mtu anataka *desk work*. Hivyo kwa mapendekezo yangu nilikuwa napendekeza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia. Sisi kama Tanzania kwenye Mpango wetu wa maendeleo tuweke mkakati wa kuanzisha *The Tanzanian Artificial Intelligence Framework* pamoja na *The Tanzanian Employment and Unemployment Desk* ambayo itaweka *National accountability* kwa vijana kwamba, kwenye miaka 25 ya maisha yako, wewe una mchango gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Neema Majule; atafuatiwa na Mheshimiwa Benjamin Ngayiwa; Mheshimiwa Rashid Mtima, ajiandae.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi na nimefurahi sana kumfuata kijana kuongea, maana kijana amejikita kwenye mambo ya vijana mpaka wote tumefurahi na hii ndiyo sura ya Bunge lako lina wawakilishi wa kila sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa ajili ya kutusaidia na kutuwezesha kutupa Mawaziri pamoja na Manaibu Waziri ambao wamekaa kwenye

Wizara hizi na hata kuweza sasa kutoka na Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka 25. Moja kwa moja niipongeze Wizara ya Mipango na niipongeze Wizara ya Fedha: Mpango uliopita wa miaka mitano ulikuwa mzuri umetusogeza mpaka tulipo na kweli maendeleo makubwa yamefanyika nchi za Kiafrika zinashangaa, dunia pia nayo inashangaa kwa maendeleo makubwa ambayo Tanzania imeweza kupiga kwa miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumepata Mpango mwingine ambao kama wanavyosema wenzangu na walivyounga mkono ya kwamba Mpango huu ni wa Kisayansi na Kiteknolojia: Mpango ambao unaweza kutupaisha tukaenda mahali pazuri zaidi, lakini tuna Mpango huu wa muda mrefu sasa wa miaka 25 na huu Mpango wa miaka mitano, halafu tumepewa Mpango wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wangu mimi nataka kuchangia nafasi sasa ya mwanamke katika Mpango huu. Nimeupitia Mpango na kuweza kuona nafasi ya mwanamke, Wabunge wengi wamechangia mambo mbalimbali na wamegusa kwa namna moja au nyingine mambo ya wanawake katika Mpango huu. Hata hivyo, ninataka niseme kwamba, wanawake tumepaishwa zaidi kipindi hiki cha kuwa na Rais, Mwanamke Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mpango huu ambao tumeletewa wa miaka 25, pia wanawake wamepewa nafasi kubwa sana. Lakini niseme tu kwa nini nimekuwa na *interest* hiyo, kwanza, kwa sababu mimi zaidi ya kuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, mimi pia ni Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake idadi yetu sisi ni 51% *population* ambayo tumehesabiwa mwaka jana 2025, lakini pia ndiyo wazalishaji wakubwa na ndio wanaoweza kuupeleka uchumi huu kutoka hatua hii kwenda hatua nyingine. Kwa sababu wanawake wamejikita zaidi kwenye kilimo, asilimia kubwa ya wakulima ni wanawake na pato la Taifa ambalo linachangia ni 54%, ambao watendaji wakubwa kwenye *field* ni wanawake.

Hivyo basi, hatuwezi kutenga maendeleo makubwa ambayo tunayatarajia pasipo kuwahusisha na kuwaongelea wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, wanawake wamejikita kwenye biashara ndogondogo ikiwepo biashara za kati *(SME)*, kwa hiyo ni wanawake ndiyo waliofanya. Wanawake pia wamejikita kwenye kazi za huduma za jamii, hivyo basi niseme kwamba, Mpango huu ambao tunao, tutaenda vizuri tukiwa kwenye usawa wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipendekeze moja kwa moja nisije baadaye mwishoni nikashindwa vitu vya kupendekeza. Niseme basi Mpango huu kama tutaweza kuenenda ukiwa na mlengo wa usawa wa kijinsia viwekwe moja kwa moja viashiria mahususi vya kijinsia katika Mpango mzima, lakini pia kwenye bajeti, yaani kuwe na *indicators* ambazo ni mahususi kabisa za kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, ushiriki mzima wa wanawake kuanzia kwenye Mpango, lakini pia kwenye ufuatiliaji kwa maana ya *monitoring,* lakini pia kwenye tathmini. Kuwepo na ushiriki wa wanawake kwenye *stage* zote hizo kuanzia kwenye mipango; kwenye utekelezaji mpaka kwenye tathmini. Tukienda kwa pamoja hivyo, ninaamini kwamba tunaenda kufikia haya malengo vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niseme kwamba, uchumi jumuishi ambao tumeamua kwenda nao kwa sasa hivi utaenda kuinua mapato yetu ya Taifa mpaka dola za Kimarekani trilioni moja, lakini pia pato la mtu mmoja mmoja linaenda kwenye dola za Kimarekani 7,000 ifikapo 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yatatokea tu kama tutaongeza fursa za ajira kwa wanawake: wanawake ndiyo ambao ni wazalishaji, lakini siyo hivyo, tutaweza kujikwamua tu kwa kupunguza umaskini kuanzia ngazi ya kaya au kuanzia ngazi ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini ukiuongea kati ya mwanamke na mwanaume aliye masikini zaidi ni mwanamke kwa

sababu ya mila zetu na desturi ya kwamba kwenye ngazi ya kaya mmiliki wa mali ni mwanaume na utaweza kuona haya mara mwanaume anapoondoka duniani yule mwanamke hawezi kuruhusiwa kumiliki ardhi aliyonayo pale inachukuliwa na familia ya mwanaume. Kule alipotoka kwenye familia yake hajapewa ardhi, huku alipoolewa nako hapewi ardhi, hivyo umaskini wa mwanamke ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kwenda kwa pamoja basi tulenge kuzikwamua kaya ambazo mara nyingi zinakuwa *headed* au zinakuwa zinaongozwa na wanawake, huko ndiko ulipo umaskini. Kama tutakuwa na Mpango mzuri wa kuwakwamua wanawake kwenye ngazi ya familia, moja kwa moja tutakuwa tumefanikiwa kulikwamua Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mambo ya elimu; kama tutaweza kutoa elimu kwa wasichana vizuri kabisa, tunawapanua wasichana uwezo kama unavyoona Mheshimiwa Magreth ame-*present* pale, uwezo wake umepanuka, msichana huyu amepewa elimu. Hivyo basi tunaweza kumkwamua, tunaweza kuwakwamua wanawake kuanzia kuwapa elimu ya kutosha kuanzia wakiwa wadogo. Mpango huu umeonesha tunaongeza idadi ya shule za sekondari na ushiriki wa wasichana kwenye elimu ya sekondari na tunaongeza pia hata *teacher-student ratio* kutoka 105 kwa Mwalimu kwenda wanafunzi 40 kwa Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hiyo itasaidia kuongeza fursa ya elimu kwa wasichana na tutawaongezea wasichana sasa uwezo wa kushiriki kwenye biashara za ushindani. Siyo hivyo tu, tunapoenda kuangalia mambo haya moja kwa moja tunapoongelea mwanamke tunaongea juu ya mwanamke na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tumefanikiwa sana kupunguza vifo vya wanawake na Watoto wachanga. Mpaka sasa hivi ni vizazi 104 tu katika 1,000 wanawake wanaopoteza maisha. Mpango huu unaenda kupunguza vifo hivi mpaka vizazi 85 tu kati ya vizazi 1,000, lakini inapunguza vifo vya watoto kuanzia 33 hadi 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa nini sasa? Ni kuzidi kuwekeza zaidi katika sekta ya afya ili tuendelee kuboresha maisha ya wanawake na Watoto, lakini siyo hivyo huduma za *dispensary* zinapoanzishwa na vituo vya afya zilenge kuwapa ajira nyingi zaidi wanawake kwa maana ndiyo watoa huduma za kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo tutaweza kufaulu sana kuwanufaisha wanawake kwenye huu Mpango wetu wa miaka 25, lakini Mpango wetu wa miaka mitano ambao moja kwa moja umejikita kupunguza umaskini. Pia tutaweza kufanikiwa kwa huu Mpango wetu wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoe mapendekezo yangu, zaidi ya kuongeza *indicators* kwenye kila Mpango na pia na bajeti, lakini pia fedha za mikopo za wanawake ziongezwe kwenye bajeti, ambayo itatengwa kwa ajili ya maendeleo ya wanawake…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Tunashukuru sana kwa mchango mzuri. Muda umekwisha malizia sentensi ya mwisho.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benjamin Ngayiwa na mchangiaji wa mwisho kwa leo atakuwa Mheshimiwa Rashid Mtima.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nichangie katika Mpango huu wa Taifa wa Maendeleo. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia uhai na afya njema lakini pia niendelee kuwashukuru wananchi wema wa Jimbo la

Kahama Mjini ambao walinichagua na kuniamini ili nije kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia familia yangu kwa maana ya mke wangu Happiness Kalugaba, lakini na Mama Gaudensia Ngayiwa na Mzee Ngayiwa Pascal Maziku na ndugu na jamaa wote wanaoendelea kunitia moyo katika kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Kahama Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze sasa katika kuchangia mapendekezo ya Mpango huu elekezi wa maendeleo wa muda mfupi, muda wa kati na mrefu. Niseme tu kwamba Mpango huu umetambua rasilimali zetu ambazo tupo nazo katika Nchi yetu tukufu ya Tanzania. Rasilimali hizo ni uoto wa asili; ardhi kubwa ambayo ina rutuba inayo *support* kilimo cha aina zote kwa maana ya mazao ya chakula na mazao ya biashara, lakini tuna *water bodies* ambayo ni mito; maziwa lakini na bahari ambayo yote haya yana *support* shughuli za uvuvi na kilimo lakini na matumizi mengine ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu hapa, ninaamini Serikali yetu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa mama yetu Rais mpendwa Mama Samia, ipo na nia thabiti na ya dhati katika kuwatumikia wananchi wetu. Kwa hiyo, hapa nishauri tu katika mikataba ambayo inajumuisha rasilimali zetu hizi nilizozitaja basi ipitie katika Bunge hili ili Wabunge tuweze kutoa ushauri wetu kwa sababu mikataba inayohusu rasilimali, inahusu pia kizazi chetu na dira hii ya maendeleo ya miaka 25, tunapoongelea mtoto wa miaka mitano, leo baada ya miaka 25 kufikia 2050 atakuwa ni mtoto mwenye miaka karibu 30. Sasa tunakuwa na Mpango huu wa maendeleo ambayo kwa kweli umelenga katika kuendeleza kizazi chetu ambacho kitakuja kunufaika na rasilimali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mpango huu wa maendeleo umeweka vichocheo vya maendeleo ambavyo ni imetambua kuhusu nishati, *logistics* kwa maana ya uwekezaji katika miundombinu lakini sayansi na teknolojia, mageuzi ya kidijiti, mazingira ya biashara na uendelezaji wa uwekezaji katika

kuboresha mifumo ya kisheria na kukuza ubia kati ya sekta za umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa niseme tu kama wachangiaji waliotangulia kuchangia, idadi ya vijana kwa maana hawa ndiyo wabeba maono na watekelezaji wa huu Mpango wa Maendeleo wa Muda Mfupi, Muda wa Kati na Muda Mrefu. Hawa vijana kati ya umri wa miaka 15 na 35 ni zaidi ya 60% na hawa ndiyo nguvu kazi: kwa maana wale watoto na wazee ni tegemezi kwa nguvu kazi hii. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie sera na mpango wetu katika kuwawezesha vijana wetu, waweze kuingia moja kwa moja katika kutumia hizi rasilimali nilizotaja hapa ikiwemo madini; ikiwemo rasilimali zetu za ardhi, lakini na maji ambayo tupo nayo katika mito, maziwa na bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali kupitia Wizara na ninashukuru kwamba Wizara ya Vijana imeanzishwa, kwa hiyo tuweke sera ambazo zitaenda kuwawezesha vijana wetu kwa mitaji, lakini kuwawezesha vijana wetu kwa *skills* kwa maana ya teknolojia ili waweze kuhimili ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliposema kwamba tuboreshe miundombinu…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Jimbo langu la Kahama Mjini…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benjamin, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nilitaka kumpa taarifa mchangiaji, anachangia vizuri kabisa kwenye kuishauri Serikali jinsi ya kuhakikisha kwamba vijana ambao ndiyo nguvu kazi wanawezeshwa kuhakikisha kwamba wote wanakuwa ni wazalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu za sasa hivi 87% ya *population* tuliyo nayo ni tegemezi, kwa maana watoto chini ya miaka 15 na wazee kuanzia miaka 65. Kwa hiyo, wazalishaji tu ni 13%, sasa Serikali ikichukua hizo takwimu ikazifanyia kazi kwa vile anavyosema mchangiaji pale ni hakika sasa hii *percent* ndogo ambao ndio wazalishaji ambao ndiyo wanabeba jukumu kubwa la kuwasaidia hao wengine ambao ni tegemezi itasaidia kukwamua hilo eneo ambalo linategemea sana *87%*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Benjamin, taarifa ya Mheshimiwa Matiko, unaipokea?

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea na ninaomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea hapa kuhusu uboreshaji wa miundombinu, lakini na mazingira ya kibiashara. Pale Jimboni kwangu Kahama ni jimbo zuri na lina watu ambao wanajituma sana katika kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali iwawezeshe wafanyabiashara pale ambao Mji wa Kahama ni kama lango la kuingia na kutokea katika nchi yetu ambayo inaunganisha Nchi zaidi ya nne; tunaunganisha Burundi, Rwanda, Kongo, Sudani na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale ningeomba sana wafanyabiashara wale wawezeshwe kwa mitaji, lakini na zile kodi, sipingi kwamba Serikali ikusanye kodi, lakini tuangalie namna ya kuwawezesha wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale pia kuna ujenzi wa ghala la biashara kwa maana ya kuweka kitovu cha kuuza mazao ya biashara na chakula nchi jirani. Ninaomba lile soko liweze kumaliziwa, lakini na miundombinu kama ambavyo Mheshimiwa Rais, alieleza katika hotuba yake ya ufunguzi wa Bunge, kwamba ipitike muda wote wa mwaka mzima wa kiangazi na masika, basi twende kuiboresha ili wananchi wetu waweze kusafirisha mazao yao kutoka sehemu nyingine na kufanya biashara bila bugudha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, wawekezaji kupitia *EPZ* na *SEZ* wawezeshwe wapunguziwe masharti ili waje nchini waweze kuwekeza. Pale Kahama tuna kongani ya viwanda pale katika Mgodi wa Buzwagi. Wawekezaji wapunguziwe masharti waje wafungue viwanda, waweze kuzalisha ajira kwa vijana wetu na hapo Serikali inaweza ikaanza kukusanya kodi kwa maana ya kwamba zile *raw materials* wanazozitumia, lakini na huduma nyingine kwa maana ya *service levy*, watakuwa wameweza kulipia na wakati huo huo wakiwa wameajiri sehemu ya vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waache kucheza mabonaza vijana wetu, kwa sababu mabonaza haya kwanza ninapendekeza hata Serikali iangalie kuyatokomeza kabisa, yasiwepo katika nchi yetu ya Tanzania. Mabonaza haya yamekuwa tu mufilisi kwa vijana na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benjamin.

Tutamalizia na Mheshimiwa Rashid Mtima.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa letu. Kwa sababu ni mara ya kwanza ninachangia, ninaomba kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa sehemu ya Bunge hili la Kumi na Tatu. Nishukuru tena chama changu kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kupeperusha bendera katika Jimbo la Newala Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua ni maamuzi ya viongozi wa kitaifa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama chetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninawashukuru sana.

Vilevile, ninawashukuru pia viongozi wa mkoa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Mkoa Mheshimiwa Saidi Nyengedi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana pia wananchi wa Jimbo la Newala Mjini wakiongozwa na Kamisa wa Chama chetu aliyeko pale Alhaji Mwangi Rajab Kundya na Mwenyekiti wangu wa CCM Mheshimiwa Jabir Mtanda. Vilevile ninawashukuru sana wananchi hawa kwa kutoa kura nyingi sana 98% kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nafasi ya Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie tu wakati Mheshimiwa Rais akiwa mgombea, alivyokuja Mtwara nilimwambia kwamba Wana-Newala Mjini watakupa kura nyingi ambazo kwa Kimakonde ni kura za *kumbambandija*. Kwa hiyo, kwa 98% alizopewa ni kura za *kubambandija* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuaminiwa na Watanzania wote na kupewa kura za kutosha. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuteuliwa na kupewa nafasi hiyo kubwa kabisa inayosimamia utendaji wa nchi yetu. Katika hotuba yake ya kwanza ameonesha dira kabisa kwamba nini anakitaka Watanzania na watendaji wote waweze kutumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuweza kupeperusha utendaji katika Wizara zao. Pia, niwapongeze tena Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na wewe binafsi kwa kuchanguliwa katika nafasi zenu hizo. Vilevile, niwapongeze Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati ambazo zinasimamia utendaji wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hizo pongezi niombe sasa kuanza kuchangia mipango yote mitatu na Mwongozo wa Bajeti ya mwaka 2026/2027. Ninaomba nijikite eneo moja tu, eneo la kwanza, kigezo cha maendeleo ambayo sisi wenyewe tumejiwekea katika mpango kwamba kwa miaka 25 tunataka

Mtanzania awe na kipato cha dola 7,000. Eneo hili ukiangalia kwa miaka mitano ya kwanza tumesema afike dola 1,638. Ukiangalia kwa kipato alichokuwa nacho sasa Mtanzania ni tofauti ya dola 361, sasa ukichukua hiyo dola 361 kwa awamu tano za miaka mitano hatufiki hiyo dola 7,000 kwa Mtanzania tutakapofika mwaka 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamaanisha nini hapa? Ninamaanisha kigezo tulichojiwekea ni kikubwa ambacho tunatakiwa sisi kama Watanzania tuweze kuhakikisha kwamba tunaamua kwa dhati kuleta maendeleo kwa wananchi. Maendeleo katika mpango yanabebwa na nini? Yanabebwa na sekta ya uzalishaji, lakini ukisoma mipango hii hata ile ya nyuma inasema changamoto kubwa ambayo imewahi kutokea katika mipango ya nyuma ni uhafifu wa kuchangia sekta ya uzalishaji, ndiyo imefanya mipango mingi isiende kama tulivyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa nchi yetu sekta ya uzalishaji kubwa ni ipi? Ambayo inabeba Watanzania wengi zaidi ya 54% inabeba hiyo, ni sekta ya kilimo. Kwa hiyo, ni lazima tuone kwa namna sekta ya kilimo tunaweza kuleta maendeleo makubwa ambayo yanawagusa Watanzania wengi ili wakifika mwaka 2050, basi waweze kuwa na kipato cha dola 7,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kwa nchi yetu kina maeneo tofauti tofauti na mazao ambayo yanategemea maeneo tofauti tofauti. Nikizingatia eneo ambalo mimi ninatoka eneo la Newala, zao kubwa kule ni korosho. Tunaweza tukasema kwa namna gani tunajipanga kuhakikisha uzalishaji wa zao la korosho ambao umekuwa ukiongezeka basi uongezeke maradufu ili wananchi wa Newala Mjini inapofika mwaka 2050 waweze kupata kipata hicho cha dola 7,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilitaka nione, tuwe na dhamira ya dhati ya kuona je, kama wakulima wa korosho na mashamba yao waliyokuwa nayo kwa namna gani tunaboresha yale mashamba ili upatikanaji au mvunaji wa korosho atoke

kwenye tani anazopata leo, basi aweze kupata tani zaidi, ili aweze kupata kipato cha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tulenge katika mazao yote si tu wakulima wa kubwa hata hawa wakulima wadogo, kwa nini? Kwa sababu tukileta nguvu kwa wakulima wadogo tukiwasaidia wakaweza kuongeza kipato chao tutaweza kuweka mazingira mazuri ya utofauti wa kipato kwa Watanzania. Kwa sababu hawa watakuwa wana kipato ambacho kitakuwa na uhakika tunavyoelekea mwaka 2050, kwa sababu tofauti kubwa ya kipato inaleta *risk* kwenye usalama wa nchi. Kwa hiyo, lazima wakulima wadogo wadogo tuwape nafasi, tuwasaidie na wenyewe tuwainue kwenye uchumi kuelekea hiyo dola 7,000 kwa mwaka 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatamani mpango huu twende tukaushushe kwa wakulima wadogo wadogo na namna gani tunaweza tukashusha mpango huu kwa wakulima wadogo wadogo? Ni kupitia katika halmashauri zetu kwa sababu kule ndiko wako Maafisa Ugani ambao wataweza kuwashauri wataweka *record* za wakulima wao kwenye maeneo yao na kuona je, wanajipanga vipi kumwezesha mkulima anayepata tani moja leo ili ikifika mwaka 2050 apate tani mbili, tatu kutoka katika shamba lao, hili linawezekana. Kwa hiyo, lazima Mpango huu tukashirikishe halmashauri, tushirikishe watendaji wa halmashauri kutokea Mkurugenzi, Madiwani, Wakuu wa Idara na kule chini kwa watu ambao wanaenda kusimamia kilimo chetu cha kila siku. Ninaomba sana Mpango huu uweze kuzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tunapowasaidia wakulima wadogo wadogo wakaweza kuzalisha kwa mfano kwenye korosho baada ya mavuno tuwekeze kwenye kubangua. Korosho inayobanguliwa nchini kwetu ni ndogo sana ni tofauti na nchi nyingine za Afrika. Ivory Coast wanabangua zaidi yetu sisi, sisi tunabangua asilimia isiyovuka 20. Ivory Coast wanatafuta 80% kwenye ubanguaji. Kwa sababu korosho ghafi ukiuza unapata fedha ni kama robo ya bei ambayo ungeipata ungebangua. Kwa hiyo, hili litatu-*assure* wakulima wetu kuweza kupata fedha nyingi, lakini hata tutakapouza nje kuweza kupata fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubanguaji huu ukienda Newala leo unaanza kwenye kaya, mtu mmoja mmoja ana mashine ya kubangua na watu wanakuja kununua korosho iliyobanguliwa lakini vikundi vya akinamama. Tuwekeze na viwanda vikubwa viweze kubangua tuweze kuuza korosho ambayo imekuwa *processed* ambayo inatoa fedha nyingi kutafuta hiyo 7,000 ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili tuliwekee nguvu kweli na si tu kwenye korosho, niseme mazao mengine maeneo mbalimbali tuweke kwenye *large scale* lakini vilevile, tuweke kwa mkulima mmoja mmoja ili kuwainua Watanzania wote kwa umoja wao. Tusije tukawaacha watu wenye uchumi mdogo chini huko vijijini ambao baadaye wanaweza wakahatarisha afya ya nchi hii kiusalama. Hilo nilikuwa ninataka nilichangie vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda kwenye korosho kusini, nani anasimamia korosho? Ni vyama vya msingi. Ukienda kwenye Mpango tumezungumzia kuongeza idadi ya wanachama. Nilikuwa ninaomba mpango uangalie vilevile nani anaongoza ushirika? Tuweke mifumo ambayo tutapata viongozi waadilifu ambao watalinda fedha za wanachama wao na kuwapatia fedha zao ili tuweze kufika hiyo dola 7,000. Tukiwa na viongozi ambao wao wakikaa pale wanafanya wakulima wasipate haki yao ya msingi ya kilimo walichokifanya kwa mwaka mzima itakuwa tunawanyonya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima Mpango nao uone na uweke mifumo ambayo tutapata viongozi kwa ajili ya ushirika, kwa sababu wao ndiyo wanaosimimia hili zao kule chini. Nilikuwa ninataka nishauri hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukimzungumzia Mtanzania kwenye sekta hiyo ya kilimo aweze kupata hizo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa, muda umekwisha.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba tuwekeze kwenye umwagiliaji, huko nako tufanye Mtanzania awe anafanya kazi muda wote na kuweza kupata kipato muda wote. Pia, wanaosimamia Madiwani na viongozi wa Serikali za Mitaa, tuone namna ya kusimamia haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, huyu ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo, wale ambao hawajapata nafasi wataendelea na majadiliano kesho.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linarudia.

**MWENYEKITI:** Bunge linarudia.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana mliopata nafasi ya kuchangia mapendekezo yetu ya mpango kwa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Serikali imechukua mapendekezo hayo, tayari kwa kuboresha Mpango huu kwa ajili ya manufaa ya Taifa letu.

Baada ya kusema hayo machache, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.50 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 5 Februari, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*